

**MAENDELEO YA LUGHA YA KISWAHILI NA ATHARI ZAKE KWA
JAMII YA KIARABU: MTAZAMO WA KILUGHAWIYA JAMII**

EMAD AHMED ABABAKER

**TASINIFU YA PHD. KISWAHILI
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA
2013**

**CHIMBUKO NA MAENDELEO YA LUGHA YA KISWAHILI NA ATHARI
ZAKE KWA JAMII YA KIARABU: MTAZAMO WA KILUGHAWIYA
JAMII**

EMAD AHMED ABABAKER

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KUKAMILISHA MASHARTI YA DIGRII
YA PHD. KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA
2013**

UTHIBITISHO

Aliyetia saina hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasnifu hii itwayo:
Maendeleo ya lugha ya Kiswahili na Athari zake kwa Jamii ya Kiaarabu:
Mtazamo wa Kilughawiya Jamii, na kumpendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria
cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digirii ya PHD. Kiswahili ya
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sheikh, Professa, Dkt. T.S.Y.SENGO

(MSIMAMIZI)

Tarehe -----

IKIRARI

NA

HAKIMILIKI

Mimi **Emad Ahmed Ababaker**, nathibitisha kuwaTasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Digirii yoyote.

Sahihi.....

Haki ya kunakili tasinifu hii inalindwa na mkataba wa Berne, Sheria ya haki ya kunakili ya mwaka 1999 na mikataba mingine ya sheria za kitaifa na kimataifa zinazolinda mali ya kitaaluma. Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama yote au sehemu ya Tasinifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

SHUKURANI

Kwa hakika si kazi rahisi kuwataja na kuwashukuru kwa majina wote waliochangia kukamilika kwa utafiti huu. Hata hivyo, napenda kutumia fursa hii kutoa shukurani zangu za dhati kwa wote ambao kwa njia moja ama nyingine wamewezesha kukamilika kwa utafiti huu. Wafuatao wanastahili shukurani za kipekee.

Kwanza, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu, aliyenijaalia afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu Sheikh, Professa, Dkt. T.S.Y.Sengo kwa msaada wake usio na kikomo uliowezesha kukamilika kwa utafiti huu. Kwa hakika alijitoa sana katika kuniongoza, kunishauri, kunikosoa na kunielekeza katika hatua mbalimbali za utafiti wangu huu na hivyo kunilazimu kutumia muda mwingi kutafakari na kufanyia kazi maelekezo yake yaliyosaidia kukamilika kwa utafiti huu. Nakushukuru sana Mzee Sengo na nakutakia kila la kheri katika maisha yako wewe binafsi pamoja na familia yako.

Tatu, natoa shukurani zangu za dhati kwa mfadhili wangu wa masomo ambaye ni Serikali ya Watu wa Libya kwa kujitoa, na kuniwezesha kwa kunilipia gharama za masomo yangu ya uzamivu na gharama za kujikimu katika kipindi chote cha masomo yangu.

TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa baba yangu **Ahmed Ababaker** na marafiki zangu wote ambao kwa hakika wamejitoa kwa hali na mali katika kufanikisha malengo yangu ya kitaaluma ambayo yamenifikisha hatua hii ya kutunukiwa **Shahada ya Uzamivu** katika Kiswahili.

IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza chimbuko na maendeleo ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu kupitia mtazamo wa Kilughawiya jamii. Lengo hili limeweza kufanikiwa kutokana na kukamilika kwa malengo mahususi yaliyohusu; kuchunguza chumbuko la lugha ya Kiswahili na sababu za madai kwamba Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu, kubainisha namna Kiswahili kilivyoathiri jamii ya Kiarabu katika maisha yake ya kila siku na kufafanua maendeleo ya lugha ya Kiswahili katika karne ya ishirini na moja na changamoto zake. Mapitio ya kazi tangulizi mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti yamepitiwa kwa kina kwa kuongozwa na nadharia ya Lugha kama Muundo Jamii, Kiswahili ni Kiarabu na Kiswahili ni lugha ya Vizalia yameshadidia kukomaa kwa kazi husika. kwa upande wa uchambuzi, uchakataji na usanifishaji wa data, utafiti umetumia mbinu za ushiriki, usaili, hojaji na upitiaji wa nyaraka katika kukusanya data. Mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu.

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa chimbuko la Kiswahili ni katika mwambao wa Afrika ya Mashariki. Hata hivyo zipo sababu mbalimbali zinazotumiwa na wale wanaodai kwamba Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu na hivyo kutoa hitimishi kwamba Kiswahili asili yake ni Kiarabu. Sababu hizo ni pamoja Kiswahili kujengwa na msamiati mwingi wa lugha ya Kiarabu, Kiswahili kuwa na msamiati wenye lafudhi ya Kiarabu na ushairi wa Kiswahili asili yake ni dini ya Kiislamu na fasihi ya Kiarabu. Hata hivyo, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba sababu hizo hazina mashiko ya kitaalimu katika kushadidia kile zinachoeleza. Hii inatokana na ukweli kwamba, wanataalimu waliotafiti na kutoa madai hayo walikuwa ni wageni ambao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusiana lugha ya Kiswahili na utamaduni wake. Kwa matokeo haya Kiswahili kimeendelea kuonekana kuwa ni lugha yenye asili yake katika mwambao wa Pwani ya Afrika ya Mashariki na si Kiarabu wala lugha ya Vizalia. Kutokana na ukweli huo Kiswahili kimeendelea kuwa lugha ya matumizi mapana na kuiathiri jamii ya Kiarabu inayoishi mwambaoni mwa Pwani ya Afrika ya Mashariki katika maisha yake ya kila siku. Athari hizo zinaonekana katika masuala ya kidini, kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi. Kutokana na Kiswahili kuwa ndiyo

lugha ya matumizi mapana katika nchi mbalimbali za Afrika ya Mashariki kimeweza kuvuka mipaka na kutumika pia kimataifa. Kiswahili kimekuwa ni lugha inayotumika katika ngazi mbalimbali za kielimu, lugha ya kupashana habari kitaifa na kimataifa na lugha ya kuwasilishia fasihi ya kitaifa na kimataifa. Haya ndiyo maendeleo yaliyofikiwa na lugha ya Kiswahili katika karne hii ya ishirini na moja. Mwisho, tumetoa hitimisho kuu la utafiti ambalo kwalo tumeainisha maeneo mbalimbali ya kiutafiti yanayoweza kuibuliwa kuhusiana na lugha ya Kiswahili na masuala ya kinadharia kwa ujumla.

YALIYOMO

Uthibitisho.....	i
Ikirari na Hakimiliki	ii
Shukurani	iii
Tabaruku	iv
Ikisiri.....	v
Yaliyomo.....	vii

SURAYA KWANZA: UTANGULIZI 1

1.1 Mada ya Utafiti	1
1.2 Usuli wa Mada	1
1.3 Tatizo la Utafiti	2
1.4 Usuli wa Tatizo la Utafiti.....	2
1.4.1 Maendeleo ya Kiswahili.....	2
1.4.2 Mahusiano baina ya Kiswahili na Kiarabu	5
1.5 Lengo la Utafiti	7
1.5.1 Madhumuni Mahususi	7
1.6 Maswali ya Utafiti.....	7
1.7 Umuhimu wa Utafiti	8
1.8 Mipaka ya Utafiti	9
1.8.1 Vikwazo vya Utafiti.....	9
1.8.2 Utatuzi wa Vikwazo.....	9

SURA YA PILI: TAHAKIKI YA NADHARIYA NA UTEUZI..... 10

2.1 Kiunzi cha Nadhariya	10
--------------------------------	----

2.2.1	Lugha kama Mfumo wa Kiishara na Kimuundo.....	10
2.2.2	Lugha kama Nyenzo ya Kiuamilifu	11
2.2.3	Lugha kama Muundojamii	12
2.3	Nadharia ya Lugha za Kipijini	12
2.4	Nadhariya kwamba Kiswahili ni Krioli	13
2.5	Kiswahili Asili yake ni Kongo.....	16
2.6	Kiswahili ni lugha ya Vizalia.....	16
2.7	Kiswahili ni Kiarabu	18
2.8	Uteuzi wa Nadhariya.....	20
SURA YA TATU: KAZI TANGULIZI		21
3.1	Lahaja za lugha ya Kiswahili	21
3.2	Mahusiano baina ya Kiswahili na Kiarabu	26
3.3	Suala la Lugha Kukopa Msamiati Kutoka Lugha Nyingine	28
3.4	Fasihi ya Kiswahili na Kiarabu.....	31
3.5	Kiswahili na Uislamu.....	32
SURA YA NNE: MBINU ZA UTAFITI		34
4.1	Njia za Kufanyia Utafiti.....	34
4.2	Usanifu wa Utafiti.....	34
4.3	Maktabani	35
4.4	Maskanini.....	35
4.5	Vyanzo vya Data.....	36
4.5.1	Data za Msingi	36
4.6	Mbinu za Ukusanyaji wa Data.....	37

4.6.1	Mbinu ya Ushiriki	37
4.6.2	Mbinu ya Mahojiano	38
4.6.3	Upitiaji wa Nyaraka	39
4.6.4	Uchambuzi wa Kimaudhui (Content Analysis)	39
4.7	Uteuzi wa Watafitiwa.....	40
4.8	Usahihi (validity) na Kuaminika (reliability) kwa Mbinu za Utafiti	41
4.8.1	Usahihi wa Data	41
4.8.2	Kuaminika kwa Data.....	42
4.9	Maadili ya Utafiti	42
SURA YA TANO: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA		43
5.1	Uchambuzi wa Data	43
5.2	Chimbuko la Lugha ya Kiswahili	44
5.3	Sababu Zilizowafanya Wanataalimu Mbalimbali Kudai Kwamba Kiswahili Kimeathiriwa Sana na Kiarabu	49
5.3.1	Utangulizi.....	49
5.3.1	Watafiti wa Mwanzo wa Kiswahili.....	50
5.3.3	Kiarabu Kufundishwa katika Madrasa.....	52
5.3.4	Kiswahili Kimekopa Msamiati Mwingi Kutoka Kiarabu	54
5.3.5	Lafudhi ya Matamshi ya Kiswahili	56
5.3.6	Ushairi wa Kiswahili Asili yake ni Uisilamu na Uarabu	58
5.3.7	Hitimishi	61
5.4	Athari ya Lugha ya Matumizi Mapana (Kiswahili) kwa Waarabu Waishio katika Pwani ya Afrika Mashariki	62

5.4.1	Utangulizi.....	62
5.4.2	Athari za Kidini.....	62
5.4.3	Athari za Kiutamaduni	65
5.4.4	Athari za Kisiasa na Utawala.....	67
5.4.5	Athari za Kiuchumi.....	69
5.4.6	Hitimishi	71
5.5	Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili Katika Karne ya Ishirini na Moja na Changamoto Zake	72
5.5.1	Utangulizi.....	72
5.5.2	Kiswahili katika Elimu	73
5.5.3	Sekta ya Habari na Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili	76
5.5.4	Fasihi na Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili.....	77
5.5.5	Hitimishi	80
5.6	Changamoto Zinazokabili Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili Duniani	81
5.6.2	Upungufu wa Vitabu vya Kufundishia Wageni.....	81
5.6.3	Upungufu wa Wataalamu wa Kufundisha Lugha ya Kiswahili kwa Wageni	83
5.6.4	Sera ya Lugha ya Taifa	85
5.6.5	Utashi wa Kisiasa katika Masuala ya Lugha	87
5.6.6	Kukosekana kwa Chombo Rasmi cha Kusimamia Uendelezaji wa lugha ya Kiswahili katika ukanda wa Afrika ya Mashariki.....	90
5.6.7	Hitimishi	92

SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO, MATOKEO NA

MAPENDEKEZO	94
6.1 Utangulizi.....	94
6.2 Muhtsari	94
6.3 Matokeo ya Utafiti	97
6.4 Mapendekezo	102
AREJELEO	103
VIAMBATISHO	111
KIAMBATISHO NA. 1	111
KIAMBATISHO NA.2.....	113

SURAYA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Mada ya Utafiti

Maendeleo ya lugha ya Kiswahili na Athari zake kwa Jamii ya Kiaarabu: Mtazamo wa Kilughawiya Jamii

1.2 Usuli wa Mada

Mada iliyoshughulikiwa katika utafiti huu ni “**Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili na Athari zake kwa Jamii ya Kiarabu: Mtazamo wa Kilughawiya Jamii**”. Mada hii imechaguliwa kutokana na kuwepo kwa pengo la kitaalimu linalohitajiya kujazwa. Pengo hilo linajibainisha katika utafiti kadhaa uliyokwishafanyika. Taarifa zimedai kwamba Kiarabu pekee ndicho kilichokiathiri Kiswahili, madai ambayo yapo hewani bila ya ushahidi. Hali hii imewafanya baadhi ya wanataalimu kudai kwamba Kiswahili ni Kiarabu (Owhida, 2006; Mohamed, 2006; Ghanem, 2005). Kwa msingi huo, Kiswahili kimeonekana hakijakiathiri Kiarabu kutokana na kutofanyika kwa utafiti wa kina katika taalimu hii. Ni jambo lililo bayana kwamba, jamii mbili zenye lugha tafauti zinapokutana ni lazima lugha zao ziathiriane kwa namna moja ama nyingine. Kuathiriana huku si suala la hiyari, utashi, hadhi ya lugha, hadhi ya jamii bali mazingira ya kukutana kwa jamii hizo na lugha zao, ndiyo hulazimisha lugha hizo kuathiriana. Kwa msingi huu, utafiti huu ulilenga kuchunguza maendeleo ya lugha ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu ili kupata ukweli wa majibu ya maswali ya utafiti. Mada ya utafiti huu si pana kama baadhi ya wanataalimu wanavyoweza kuitathimini kwa kuwa mambo yaliyochunguzwa ni yale ya msingi tu na si kila kitu.

1.3 Tatizo la Utafiti

Lugha za Kiarabu na Kiswahili zina historia ndefu sana katika kukuwa na kuenea kwazo. Ni katika karne ya saba Waarabu kutoka Omani, Yemeni na Uajemi walizuru katika Pwani ya Afrika ya Mashariki kwa minajili ya kufanya biashara na kuenea dini ya Kiislamu. Lugha za Kiarabu na Kiswahili zilitumika sambamba katika mawasiliano hayo ya kibiashara na yale ya mafundisho ya dini ya Kiislamu. Kutumika kwa lugha hizi kwa pamoja ni dhahiri ziliathiriana sana katika mifumo ya Kilughawiya, Kilughawiya Jamii na kadhalika. Cha ajabu na kushangaza, tafiti nyingi zilizofanyika zinaonesha kwamba Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu huku kutokuwepo tafiti juu ya Kiswahili kukiathiri Kiarabu au jamii ya Kiarabu. Hali hii inaonesha kwamba upande mmoja ni dhaifu na unaweza kuathiriwa tu kuliko kuathiriana kwa lugha husika. Swali ambalo utafiti huu ulilenga kulijibu pamoja na mengine ni; Hivi inawezekana jamii mbili zenye lugha tafauti zikakutana na kuishi pamoja kwa miaka mingi halafu lugha au jamii moja tu iathiriwe na nyingine isiathiriwe, hali ya kuwa zote zinatumika sawia? Kulijibu swali hili nimelazimika kufanya utafiti kuchunguza maendeleo ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu: mtazamo wa kiisimu jamii ili kuziba pengo hili la kitaalimu.

1.4 Usuli wa Tatizo la Utafiti

1.4.1 Maendeleo ya Kiswahili

Kuzungumza juu ya maendeleo ya Kiswahili katika usuli wa utafiti ni jambo muhimu sana kwa kuwa ni katika maendeleo hayo ndiyo tunapata kuathiriana baina ya Kiswahili na Kiarabu. Kiswahili ni lugha mojawapo inayozungumzwa katika nchi nyingi Ulimwenguni. Awali, lugha hii ilitambulika na kuanzwa na kutumika na watu

wachache walioishi mwambaoni, Afrika Mashariki. Idadi ya watu walioishi humo ilikuwa ndogo kwa wakati huo. Ni kawaida ya lugha zote kuanza padogo na kusambaa. Hivi leo lugha ya Kiswahili imekuwa na matumizi yake kuenea kwa haraka katika Bara la Afrika, Ulaya, Marekani, Asia na Australia. Ghanem (2005) anaeleza kwamba, lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa Barani Afrika. Kwa ukubwa wake, inafaa kabisa kuwa lugha ya kidiplomasia. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika masuala ya kidiplomasia yata kifanya Kiswahili kuenea kwa kasi kubwa zaidi na kupata wazungumzaji wengi kuliko hivi sasa. Mohamed (2006) anataja lugha kubwa katika bara la Afrika kuwa ni Kihausa, Kifulani, Kizulu, Kilingala, Kiarabu na Kiswahili. Hata hivyo, Kiswahili kinazishinda lugha za Kihausa na Kifulani katika kuvuka mipaka na kutumiwa katika sehemu kubwa ya Bara Afrika ikilinganishwa na lugha hizo. Lugha za Kihausa na Kifulani huzungumzwa katika nchi ya Nigeria na karibu nchi zote za Afrika Magharibi. Kiswahili kinazungumzwa katika nchi zote za Afrika ya Mashariki (Kenya, Rwanda, Burundi, Tanzania na Uganda), Afrika ya Kati hasa nchini Kongo (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), Zambia, Malawi, Msumbiji, Somalia, Sudani ya Kusini na sehemu mbalimbali za Bara la Afrika na nje (Amir, 1994; Sherrif, 1994 katika Owhida, 2006).

Kiswahili, kuwa lugha kubwa duniani, kumekifanya kitumike katika maendeleo ya maisha ya mwanadamu ya kila siku. Mohamed (2006) anaeleza kwamba, Kiswahili nchini Tanzania, Kenya na Uganda kimetangazwa kama lugha za Taifa kwa maana ya kutumika katika shughuli za kila siku za kiserikali, kisiasa, kidini na kijamii. Katika kukienzi na kukikuza Kiswahili, mfano nchini Tanzania, Kiswahili

kinafundishwa kama somo kuanzia ngazi ya elimu ya msingi mpaka chuo kikuu. Vile vile kinatumika kama lugha ya kufundishia elimu ya msingi. Katika nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi Kiswahili kinafundishwa kama somo katika ngazi ya elimu ya msingi mpaka chuo kikuu. Mohamed (2006) anaendelea kueleza kwamba, hivi sasa Kiswahili kinafundishwa kama somo katika viwango mbalimbali vya elimu katika nchi za Libya, Afrika ya Kusini, Nigeria, Ghana, Sudani, Marekani, Uingereza China, Japan Korea Kusini, Omani, Mexico na kadhalika. Hali hii huifanya lugha ya Kiswahili kukuwa na kuenea zaidi katika sehemu mbalimbali duniani.

Mohamed (2006) anaongeza kwamba, kwa sasa ipo mikakati maalumu ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Dalili za kufanikiwa kwa mikakati hiyo zimeshaanza kuonekana kutokana na lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha maalumu zinazotumiwa katika mikutano ya Umoja wa nchi za Afrika. Raisi mstaafu wa Msumbiji Bwana Chisano na Raisi wa Tanzania Dakta Jakaya Mrisho Kikwete, ni miongoni mwa viongozi wakubwa wanaotumia lugha ya Kiswahili katika vikao/mikutano ya mataifa ya Afrika. Mohamed (2006) anashadidia kwamba, kiongozi wa Libya Kanali Mohamed Al-Qaddafi (kwa sasa ni marehemu) ameonesha dhamira ya dhati kabisa kukifanya Kiswahili kuwa ndiyo lugha kuu barani Afrika. Niya yake njema juu ya Kiswahili inaonekana pale serikali yake ilipoamua kutowa fedha za kuwasomesha wanafunzi wa Libya, lugha ya Kiswahili katika ngazi mbalimbali ili wapatikane Walibya ambao ni walimu wa Lugha ya Kiswahili (Ghanem, 2005; Mohamed 2006; Owhida, 2006). Wanafunzi hao kutoka Libya wanasoma katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya Libya. Kwa mfano, wapo wanafunzi wanaosoma nchini Tanzania, Misri, Kenya na kadhalika. Hata baada ya

mapinduzi ya Libya, sera ya kukieneza Kiswahili bado imeshikiliwa na viongozi wanya wa serikali.

1.4.2 Mahusiano baina ya Kiswahili na Kiarabu

Kama nilivyokwisha kueleza kwamba, Kiswahili ni lugha yenye asili yake katika Bara la Afrika. Iitokea katika karne ya saba pale Waarabu kutoka Omani, Yemen na Uajemi walipofika katika Pwani ya Afrika ya Mashariki kwa ajili ya shughuli za kibiashara na kukutanisha lugha za Kiswahili na Kiarabu. Waarabu walipofika Pwani ya Afrika Mashariki walitawala eneo hilo na kuanzisha mfumo wa utawala wa Kisultani (Hallet, 1975 katika Owhida,2006). Shughuli zao zilikuwa ni kufanya biashara ya kuchukuwa watumwa, karafuu, nazi na bidhaa nyingine kutoka Pwani na sehemu za bara na kuzipeleka nchini mwao. Biashara hii ilifanywa kwa kubadilishana bidhaa kwa bidhaa, ambapo bidhaa zilizotajwa zilibadilishanwa kwa vitu kama shanga, nguo, mapambo mbalimbali, visu, sukari na kadhalika (Hallet, 1975 katika Owhida, 2006). Hivyo kuanzishwa kwa utawala wa Kisultani katika Pwani ya Afrika Mashariki kulienda sawia na ufundishaji wa dini ya Kiislamu kwa kuanzisha madrasa zilizofundisha Qur-an tukufu. Qur-an ilifundishwa kwa lugha ya Kiarabu inayojulikana kama lugha ya Qur-an (Quranic-Arabic).

Katika Pwani ya Afrika Mashariki hali haikuwa kama huko Kaskazini mwa Afrika, lugha ya Kiswahili haikufutwa kutokana na matumizi ya lugha ya Kiarabu bali zilitumika sawia huku Kiswahili kikitumika zaidi ya Kiarabu (Adam, 2004 katika Ghanem, 2005). Kutumika sambamba kwa lugha hizi mbili kulifanya lugha hizo kuchukuwa msamiati na kuutumia katika mawasiliano. Kwa bahati mbaya sana,

tafiti nyingi zilizokwishafanywa zinadai kwamba Kiswahili ndicho kilichoathiriwa na Kiarabu kimsamiati (Steere na Taylor, 1870; Masebo na Nywangine, 2002). Kibaya zaidi, wanadai kwamba, Kiswahili kimekopa 30% ya msamiati wake kutoka lugha ya Kiarabu (Chimerah, 1995). Kimsingi si sahihi kudai kwamba lugha huwa ina tabia ya kukopa maneno kutoka lugha nyingine; lugha huchukuwa maneno kutoka lugha nyingine na kuyatumiya. Kinachopwa ni sharti kirudishwe, swali la kujiuliza, ni lini Kiswahili kitarudisha maneno kiliyoyakopa kutoka Kiarabu? Jibu la swali hili litapatikana pale ambapo utafiti huu utakapokamilika na kuonesha kumbe hata Kiarabu nacho kina maneno kutoka lugha ya Kiswahili. Kwa ufupi, ninaweza kusema kwamba suala la lugha kukopa halipo bali lugha huchukuwa na kutumiya maneno kutoka lugha mbalimbali ili kukidhi haja ya mawasiliano katika jamii.

Kihore (1984) anasema, lugha hizi mbili (Kiswahili na Kiarabu) zinatofautiana katika mambo mengi. Hazikaribiani hata kijamii. Zilitokea tu kukutana wakati Waarabu walipohamiya na kuishi katika maeneo ya Waswahili toka karne nyingi zilizopita. Historiya ya miaka mingi ambapo jamii hizi ziliishi pamoja iliruhusu kushirikishwa kwa mambo mbalimbali ya Kiarabu katika mazingira ya Kiswahili. Lakini hata pamoja na jumla ya mawasiliano hayo yote, Kiswahili, na Kiarabu zimedumu kujitambulisha kama lugha tofauti. Kwa kuwa lugha hizi zimeendelea kubaki kama lugha tofauti, ni ukweli usiopingika kwamba kila lugha ina mchango katika kuiathiri lugha nyingine na hivyo kuathiriana. Utafiti huu ulilenga kutafuta dalili za kuthibitisha kwamba, lugha ya Kiswahili iliathiri jamii ya Kiarabu katika maisha ya kila siku na si kweli kwamba Kiswahili pekee ndicho kilichoathiriwa na Kiarabu kwa kuwa Kiarabu ni lugha ya mabwana na Kiswahili ni ya watwana.

1.5 Lengo la Utafiti

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza maendeleo ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu iishio Pemba na Unguja kupitia mtazamo wa Kilughawiya jamii.

1.5.1 Madhumuni Mahususi

1.5.1.1 Kuchunguza chimbuko la Kiswahili na sababu za madai kwamba Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu.

1.5.1.2 Kubainisha namna Kiswahili kilivyoathiri jamii ya Kiarabu iishio Pemba na Unguja katika maisha yake ya kila siku.

1.5.1.3 Kufafanua maendeleo ya lugha ya Kiswahili na changamoto zake katika karne ya ishirini na moja.

1.6 Maswali ya Utafiti

1.6.1 Nini chimbuko la Kiswahili na sababu zinazotumiwa katika kutoa madai kwamba Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu?

1.6.2 Jee, Kiswahili kimeathiri vipi jamii ya Kiarabu iishio Pemba na Unguja katika maisha yake ya kila siku?

1.6.3 Nini mustakabali wa maendeleo ya Kiswahili na changamoto zake katika karne ya ishirini na moja?

1.7 Umuhimu wa Utafiti

1.7.1 Utafiti huu utatoa mchango mkubwa wa kitaalimu, kinadhariya na kiutamaduni. Kwanza, katika upande wa taalimu utafiti utaziba pengo la kiutafiti juu ya maendeleo ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu, ambalo kwa ufahamu wangu hakuna utafiti uliofanywa katika mada hii.

1.7.2 Utafiti huu utatoa mchango mkubwa kinadhariya kwa kutengua nadharia zilizopo zinazokieleza na kukichambua Kiswahili kama lugha ya kuja isiyo na wenyewe. Utafiti huu utaibua mawazo mapya ambayo yatatumika kuunda nadharia mpya au kuzipa uhai na ubora zilizopo katika kudadavua na kuchambua masuala yahasuyo lugha ya Kiswahili na mahusiano yake na lugha nyingine duniani.

1.7.3 Kijamii na kitamaduni, utafiti huu utasaidiya kuweka mambo sawa kwa kuonesha kwamba ingawa jamii za Waarabu na Waswahili zilikutana na zinaendelea kukutana na kuishi pamoja lakini bado kila jamii inao utamaduni wake, miiko, mila na desturi zake. Hali hii itasaidiya pia kuonesha kwamba, zipo dalili lugha hizi ziliathiriana na siyo moja kuiathiri nyingine ndiyo maana zote zimeendelea kuwepo na misingi yake ya kiisimu jamii pamoja na tamaduni zake.

1.7.4 Utafiti huu utabaki kama kumbukumbu ya matini ya kilughawiya jamii ambayo itathibitisha kuwa lugha huchukuwa msamiati wa lugha nyingine na kuutumiya na ikabaki kuwa ni lugha iliyotafauti na lugha ambayo msamiati ulichukuliwa kwayo.

1.7.5 Utafiti utawasaidiya wanataalimu wa kilughawiya jamii, wanazuoni na wanafunzi wanaojifunza lugha kujuwa na kuelewa kwa undani zaidi juu ya

kuathiriana kwa lugha za Kiswahili na Kiarabu. Utafiti huu utatengua mtazamo na mawazo ya baadhi ya wanazuoni kwamba, Kiswahili ndiyo kimeathiriwa sana na Kiarabu na Kiswahili hakikukiathiri Kiarabu.

1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kuchunguza kuathiriana kwa lugha za Kiarabu na Kiswahili peke yake. Ninafahamu kwamba lugha ya Kiarabu imeathiriana na lugha kadhaa kama vile; Kihausa, Kifulani, Kisonghai na lugha nyingi za Kiafrika, ila mimi nitashughulikiya Kiswahili peke yake. Hii inatokana na kutokuwa na muda pamoja na rasilimali za kutosha kuwezesha kufanyika kwa utafiti mkubwa kiasi kama hicho.

1.8.1 Vikwazo vya Utafiti

Kikwazo cha utafiti huu ni kasumba waliyonayo wanaadamu kwamba Kiarabu ndicho kilichokiathiri Kiswahili na hivyo kusababisha kutopata data muafaka za kuwezesha kujibu maswali ya utafiti husika. Kasumba hii imesababisha kuwepo kwa marejeleo mengi yanaeleza juu ya lugha ya Kiarabu kuiathiri lugha ya Kiswahili kuliko kuathiriana kwa lugha hizi mbili.

1.8.2 Utatuzi wa Vikwazo

Kuhusiana na kasumba potofu juu ya kwamba lugha ya mabwana ndiyo huathiri lugha ya watwana nilitoa ufafanuzi kwa watafitiwa juu ya kuathiriana kwa lugha bila kujali utabaka katika masuala ya lugha.

SURA YA PILI

TAHAKIKI YA NADHARIYA NA UTEUZI

2.1 Kiunzi cha Nadhariya

Massamba (2004) kama anavyonukuliwa na Msanjila (2006) anafafanua nadhariya kuwa ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kiolezo cha kuelezea jambo. Kwa kuzingatia fasili hii ya nadhariya ambayo ninaikubali nitaeleza juu ya nadhariya kadhaa ambazo zitaongoza utafiti huu. Suala la kuathiriana baina ya lugha moja na nyingine ni suala la kilughawiya jamii zaidi kuliko kilughawiya. Ili niweze kueleza kwa ukamilifu juu ya nadhariya zitakazoongoza utafiti huu ni vema nieleze kwa ufupi juu ya fasili ya lugha ambayo kwayo imetoa mwangaza wa nadhariya bora ya kutumika katika utafiti huu.

2.2.1 Lugha kama Mfumo wa Kiishara na Kimuundo

Lugha siyo tu ni mfumo wa ishara zilizoteuliwa na kukubaliwa na jamii ili zitumike kuwasilisha vitu au dhana fulani bali pia ni mfumo wa ishara ambao hauna uhusiano wa moja kwa moja kati ya ishara hizo (vitaja) na vitu vitavyotajwa kuvihakikisha (Msanjila, 2006). Kwa mantiki hii hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya neno **mbuzi** na mnyama mwenyewe. Kutokana na fasili hii ya lugha, ninaweza kusema kwamba, lugha moja huweza kuchukua ishara mbalimbali kutoka lugha nyingine na kuzitumiya katika mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Kiswahili na Kiarabu vyote vimeathiriana katika ishara mbalimbali ambazo hutumika katika mawasiliano ya kila siku kwa jamii husika na bila ajizi nitaonesha kuathiriana huko. Fasili hii juu ya lugha imechangia sana katika kuibuka kwa nadhariya mbalimbali za kilughawiya

jamii kama zilivyoielezwa na Chomsky 1965; Massamba 1996; Kihore na wenzake, 2003 katika Msanjila, 2006).

2.2.2 Lugha kama Nyenzo ya Kiuamilifu

Fasili hii huitazama lugha kwa kuzingatia msingi wa dhima na uwamilifu wake bila kuwa na uhusiano wowote na fasili nyingine za lugha ambazo huzingatia mfumo wa ishara na muundo jamii. Fasili ya lugha kama nyenzo inachukulia lugha kama chombo kinachotumiwa na binadamu katika kuwasiliana, kufikiri, kuhifadhi na kuelezea uhalisiya wa mambo kama unavyosemekana na wanajamii wenyewe bila chombo hicho kuwa ni sehemu ya uhalisiya huo katika jamii. Mekacha (2000) anasema kwamba, lugha si tu sehemu ya mahusiano ya kijamii bali pia ni nyenzo huru ambayo haifungamani na nguvu zozote za kisiasa, kiuchumi, au za kiitikadi zinazotawala katika jamii hiyo.

Mawazo haya ya Mekacha (2000) yanasukuma mbele utafiti huu na ninakubaliana naye kwamba; itikadi, nguvu za kisiasa na kiuchumi za watu au jamii fulani haziinyang'anyi lugha yoyote ile uhuru wake. Kwa mantiki hii Kiswahili hakikuathiriwa na Kiarabu kwa kuwa Kiarabu ni lugha ya watawala bali ni kawaida ya lugha kuathiriwa na kuiathiri nyingine kulingana na mazingira na muktadha wa matumizi yake. Utafiti huu unathibitisha hoja hii kwa kuchunguza maendeleo ya lugha Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu ili kutengua nadhariya zilizopo zinazodai kwamba Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu huku Kiswahili kikashindwa kukiathiri Kiarabu na jamii ya Waarabu.

2.2.3 Lugha kama Muundojamii

Hapa msingi uliotumika kufasili lugha ni jamii (Mekacha, 2000). Kwa mtazamo huu lugha hufungamana na jamii na bila jamii hakuna lugha. Kinachosisitizwa hapa ni kwamba haiwezekani kutenganisha lugha na jamii. Madai kwamba, Kiswahili ni Kiarabu kwa kuwa kimeathiriwa sana si sahihi. Hii inatokana na ukweli kwamba kabla ya ujio wa Waarabu katika pwani ya Afrika Mashariki tayari Waswahili walikuwepo na walikuwa na lugha yao ya Kiswahili. Hivyo ni sahihi kueleza kwamba, lugha hizi mbili ziliathiriana na si moja iliathiri nyingine hali ya kuwa zote zilitumika sambamba.

Wazo la pili linaloibuliwa katika fasili hii ya lugha ni kwamba, jamii ya Waswahili na Waarabu zilipokutana katika mwambao wa pwani waliunda jamii moja. Katika jamii hii Kiswahili na Kiarabu zilitumika kama vyombo muhimu vya mawasiliano. Kwa muktadha huu ni wazi kwamba lugha hizi mbili ziliathiriana katika vipengele mbalimbali ambavyo utafiti huu unalenga kuvibainisha. Baada ya maelezo haya ni vema sasa tuzungumzie nadharia, kadhaa zilizoongoza utafiti huu.

2.3 Nadharia ya Lugha za Kipijini

Lugha ya Kiswahili inadaiwa kwamba ni lugha ya Kipijini. Madai haya ni mwendelezo wa mawazo ya kikoloni na ukoloni mamboleo na ni harakati za kuendelea kuishusha hadhi lugha ya Kiswahili kama linguafranka muhimu zaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (Swaleh, 1999:92). David Decamp (1975:15 katika Swaleh, 1999) anaeleza kuwa, Pijini ni lugha ya mawasiliano na ambayo kwa hali za kawaida, si lugha asiliya ya watumizi wake. Hivyo basi, madai

kwamba Kiswahili ni pijini ya Kiarabu yanatoa mantiki kwamba asili ya Kiswahili ni Kiarabu. Kama hivi ndivyo; Kiswahili kitakuwa kimeathiriwa sana na Kiarabu huku Kiswahili kikikuwa hakina mamlaka na nguvu ya kukiathiri Kiarabu. Madai haya hayana mashiko ya kitaalimu na nitathibitisha hivyo baada ya kuchunguza kuathiriana baina ya Kiswahili na Kiarabu. Chimerah (1995) anasema kwamba, iwapo lugha hii ni pijini ya Kiarabu kingekua kimechangia zaidi ya 50% ya msamiati wa lugha ya Kiswahili.

Nadhariya hii inasukuma mbele utafiti huu kwa kuwa imenipatia mwanga wa kuelewa kuwa kuna mawazo kama haya (Kiswahili ni pijini) na yametawala tafiti tangulizi kadhaa. Nimeyatazama kwa kina mawazo haya na kuyatengua kutokana na data kutoka maskanini na maktabani kwamba, Kiswahili kimeathiriana na Kiarabu na si kweli kwamba Kiswahili tu ndiyo kilichoathiriwa.

2.4 Nadhariya kwamba Kiswahili ni Krioli

Bickerton (1998:4 katika Swaleh,1999) anasema kwamba, lugha za kikrioli zinaweza kuibuka kutokana na miktadha au mazingira yafuatayo:-

Pijini zilizopata wazungumzaji wazaliwa

Katika jamii ambamo 20% ya waongejaji ni wenyeji na 80% ya matumizi ya lugha zingine za kigeni

Krioli huwa na miundo iliyoimarika ya kisarufi, msamiati mpana na kadhalika na hazitumii ishara (kwa wingi) wala uigizaji ili kufafanua maana kama pijini

Sifa hizi zinazifanya krioli kuwa na hadhi ya lugha kama lugha zingine asilia (zisizoibuka katika mazingira tuliyotaja) na hutumika rasmi katika elimu biashara, kuandikia fasihi na hata huweza kuwa linguafranka (Swaleh, 1999:95).

Ninakubaliana na maelezo haya juu ya dhana ya Krioli ila sikubaliani na mawazo kwamba Kiswahili ni Krioli iliyoanza kama pijini na baadaye kukomaa na kuwa lugha kamili. Polome (1967:13) anasema:

Kiswahili ni lugha ya Kibantu, yaani ni miongoni mwa lugha zinazoongewa kusini mwa eneo linalotanda kuanzia sehemu za mlima Cameroon hadi kufikia maeneo ya Kaskazini mwa ziwa Victoria na kuelekea pwani hadi kufika Meru katika sehemu ya mlima Kenya (na kusini zaidi kujumuisha kikundi cha lugha za kusini (Kizulu, Kihosa, Kishona, na kadhalika).

Rocha Chimeral (1995:03 katika Swalehe, 1999) anasema lau lugha ya Kiswahili ingelikuwa ni pijini au krioli basi ingelidhihirisha sifa zifuatazo:

Kama ingekuwa ni pijini inayotokana na lugha ya Kiarabu na lugha za Kibantu, basi sintaksia yake ingelitawaliwa na ile ya Kiarabu.

Lau Kiswahili kingelikuwa ni pijini, kingelikuwa na nusu au zaidi ya nusu ya msamiati wake, ungelitoka katika lugha hiyo ya Kiarabu (ya wenye nguvu, watawala). Kinyume na hali hii inathibitishwa kwamba, lugha ya Kiswahili ina msamiati uliogawanyika ifuatavyo:

Asilimi 60 ya msamiati wenye asili ya Kibantu, asilimia 30 ya msamiati wenye asili ya Kiarabu na asilimia 10 ya msamiati kutoka lugha za Kiingereza, Kireno, Kiajemi, Kihindi, Kiundu na lugha nyingine

Polome (1967) anasema kwamba japo lugha ya Kiswahili imeathiriwa kimsamiati na Kiarabu (na lugha nyingine) inabakia kuwa ni lugha ya kibantu kimuundo. Ninakubaliana na maelezo ya Polome (2007) kwa mantiki kwamba, ni tabia ya lugha kuchukua msamiati kutoka lugha nyingine na kuutumia na hali hii haifanyi lugha hiyo kuwa lugha huru. Mawazo haya yanaungwa mkono na Mcrum na wenzake (1986:47, katika Swaleh, 1999) wanasema lugha ya Kiingereza imesalia na 20% tu ya msamiati asilia (Germanic) na 80% ya msamiati wake, ni wa mkopo (kutoka makundi mengine ya lugha). Wanataalimu hawa wanaendelea kusema, ni jambo hili lilioipa lugha hiyo uhai na huenda limechangia kutumiwa kwake na watu wengi ulimwenguni (Swaleh, 1999).

Nadharia hii imenisaidia katika kuchunguza na kubainisha kuathiriana baina ya Kiswahili na Kiarabu ili kutengua mawazo kwamba Kiswahili ni Krioli iliyotokana na Kiarabu bali Kiswahili ni lugha huru iliyo na asili yake katika upwa wa pwani ya Afrika mashariki na ndio maana ikaweza kuathiri jamii ya Waarabu katika maisha yao ya kila siku. Hata hivyo, **nadharia hii ina udhaifu ambao ni:** Hutumiya kigezo cha msamiati tu bila kuzingatia vipengele vingine vya isimu kwa jumla; kama vile matamshi, maumbo ya maneno na muundo wa sentensi za Kiswahili na Kiarabu. Aidha hakuna mifano waliyoitoa kuthibitisha hoja yao. Uchunguzi wa vigezo hivi umeonesha kwamba Kiswahili ni lugha ya Kibantu, kama ilivyo fafanuliwa na Malcom Guthrie (1970).

2.5 Kiswahili Asili yake ni Kongo

Kongo ambayo zamani iliitwa Zaire na sasa inaitwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya watu wa Kongo ina nafasi yake katika dai kwamba asili ya Kiswahili ni Kongo. Dai hili linaimarishwa na wazo jingine linalodai kwamba katika vipindi kongwe vilivyopata kuwako sehemu za Pwani ya Afrika Mashariki hazikuwa zinakaliwa na watu. Kutokana na hali ya vita, uchungaji na biashara, inadaiwa kuwa wabantu walitoka sehemu za Kongo wakasambaa na kuja pwani ya Afrika Mashariki kupitiya Kigoma. Baadhi ya wabantu hawa walipitiya sehemu za Uganda wakati wa kusambaa kwao, walioeneza pia lugha zao ikiwemo hii ya Kiswahili.

Udhaifu wa Nadhariya hii ni kwamba madai ya kuwa asili ya Kiswahili ni Kongo hayana msingi kuanzia mpaka sasa wataalamu wanaodai hivi hawajaweza kueleza na kuthibitisha kisayansi ama kihistoria juu ya wapi hasa watu walianza kuishi.

2.6 Kiswahili ni lugha ya Vizalia

Mchungaji Edward Steere na Bwana Taylor (1870) katika Masebo na Nyangwine (2002) hudai kuwa Kiswahili ni lugha ya watu wa jamii ya vizalia waliotokana na mwingiliano kati ya Waarabu na wanawake Waafrika wa Pwani, yaani Wazenji (Weusi). Kutokana na kuingiliana huko palizaliwa watoto wenye mchanganyiko wa damu, watoto ambao hawakuwa Waafrika wala Waarabu kwa hiyo wakitwa Waswahili.

Waarabu waliohamia Afrika ya Mashariki walioa wanawake wa Kiafrika, watoto wao walijifunza maneno ya Kiarabu kutoka kwa baba zao na maneno ya Kibatu kutoka kwa mama zao. Katika jitihada za kujirekebisha kutoka kwenye tamaduni za

wazazi wao, vizalia hawa walianza kutumiya lugha mpya ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa ni upotoshaji wa lugha ya Kiarabu. Lugha hii ndiyo baadaye ikaitwa Sahel, yaani pwani, na kwa hiyo lugha husika ikaitwa Kiswahili yaani lugha ya watu wanaoishi pwani, (Kipwani) hususan Pwani ya Afrika Mashariki.

Wanatalimu wanaounga mkono nadharia hii ni kama vile: Mchungaji Edward Steere na Bwana Taylor (1870) wao humuona Mswahili kama mtu mwenye mchanganyiko wa damu ya mwafrika na mwarabu ambaye baadaye akawa muumini wa Uislamu na yeye mwenyewe kujiita Mwislamu. Humohumo katika lugha za kibantu wakayaingiza maneno ya Kiarabu, Kishirazi na Kihindi. Kwa mfano; dua, sala, zaka, sadaka, mahari, inshaala, salamu aleikum na kadhalika. Naye Rensch katika Masebo na Nyangwine (2002) licha ya kukubaliana na akina Edward Steer na Taylor (1870) yeye alitoa ufafanuzi zaidi kwa kuhitimisha kwamba:

Waarabu na Waajemi waliokuja Pwani ya Afrika Mashariki waliwaoa wanawake wa Kibantu. Kwa njia hii watu wa Mseto walijitokeza katika Pwani ya Afrika Mashariki kwa kuwa watu hawa wa mseto hawakuwa na kabila lao, watu hawa wakaitwa watu wa Pwani, yaani Waswahili.

Udhaifu wa Nadhariya

Kwa mtazamo wa nadhariya hii ni wazi kwamba Kiswahili ni lugha ya vizalia vya Waarabu na wabantu. Lakini nadharia hii imeshindwa kuthibitisha kihistoria na Kilughawiya kuwepo kwa lahaja mbalimbali za Kiswahili katika mwambao wa Afrika Mashariki na visiwa vya jirani: Pate, Lamu, Pemba, Unguja, Mafia na Ngazija, lahaja ambazo zinafanana na kibantu katika matamshi, msamiati na sarufi kwa ujumla kwa mfano:

Kiswahili	Kindali	Kizigua	Kijita	Kikuriya
Mtu	umundu	mntu	omunu	omunte
Moto	umulio	moto	omulilo	omoro

2.7 Kiswahili ni Kiarabu

Kuna hoja kuu tatu ambazo baadhi ya wana nadharia hii huzitumiya kuteteya madai yao kuwa Kiswahili asili yake ni Kiarabu.

Maneno yenye asili ya Kiarabu, inadaiwa kuwa maneno yenye asili ya Kiarabu yaliyomo katika Kiswahili ni ishara tosha kwamba lugha hii ilianza kama kipijini cha Kiarabu kwa mfano:

Kiarabu	Kiswahili
Duaa	Dau
Salaa	sala
Khasara	Hasara
Sifa	sifa, na kadhhalika

Neno lenyewe Kiswahili asili yake ni Kiarabu. Neno Kiswahili linatokana na neno “Sahel (umoja) na “Swahel” (wingi) lina maana ya “Pwani”

Kiswahili, Pwani Uislamu na Uarabu

Inadaiwa kwamba kwa kuwa Kiswahili kilianza pwani, kwa kuwa idadi kubwa sana ya wenyeji wa pwani ni waislamu na kwa kuwa uislamu uliletwa na Waarabu basi Kiswahili nacho kililetwa na Waarabu.

Udhaifu na Nadhariya hii

Tukianza na la kwanza kuhusu maneno yenye asili ya Kiarabu, ni kwamba, madai yao hayana mashiko. Lugha ya Kiswahili imetokea kuwa na maneno ya mkopo yenye asili ya Kiarabu, kama vile adhabu, kaburi, mjadala, asubuhi na kadhalika. Na kwa hakika yapo yenye asili ya Kiajemi, kama vile bandari, dirisha, kodi, pilau, na kadhalika. Kireno, kama vile meza, bibo, roda, kopa na kadhalika. Kihindi kama vile achari, bima, gati, laki na kadhalika. Kiingereza kama vile shati, trekta, jiografia na kadhalika. Wasemaji wa lugha mbili tofauti wanapokutana hawaachi kuathiriana kilugha. Kwa hiyo, lugha kuwa na maneno mengi kutoka lugha nyingine hayathibitishi kuhoji kwamba, lugha ya Kiswahili imetokana na hizo lugha nyingine kadhaa. Ili kuthibitisha hoja hii muundo wa sentensi za Kiswahili aghalabu haulingani na muundo wa Kiarabu; kwa mfano

Kiswahili

A -li – m – pig- i – a

Kiarabu

Itasala-bih

Katika neno “itasala-bih” wala haifuati utaratibu unaonekana katika Kiswahili japokuwa maana ni moja.

Dini nayo haikubaliki kuwa kigezo cha madai kama haya kwani lugha haiwi lugha kwa sababu ya imani. Hata hivyo, lugha ya Kiarabu yenyewe ilikuwepo karne nyingi kabla ya kuhubiri Uislamu kwa wenyeji wa Afrika Mashariki kama ambavyo lugha nyingine za Kimagharibi zilivyokuwepo karne nyingi kabla kuhubiri Ukristo. Kiingereza au Kijerumani siyo Ukristo, wala Kiarabu si Uislamu ila tunaweza kutumia lugha yoyote kufasili dini, lakini hatuwezi kutumiya dini kufasili lugha.

2.8 Uteuzi wa Nadhariya

Niliteua nadhariya tatu zilizoongoza utafiti wangu. Nadhariya hizo ni lugha kama Muundo Jamii, Kiswahili ni Kiarabu na Kiswahili ni lugha ya Vizalia. Nimechagua nadhariya hizi kwa kuwa zimeonesha namna Kiswahili kilivyoathiriwa na Kiarabu na hiyo kuwezesha kutumia nadhariya hizo hizo kutafuta dalili kwamba Kiswahili nacho kimeathiri jamii ya Kiarabu katika maisha yao ya kila siku.

SURA YA TATU

KAZI TANGULIZI

3.1 Lahaja za lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa inayotumiwa katika mawasiliano na jamii mbalimbali za Bara la Afrika na kuvuka mipaka ya kutumiwa na mabara mengine duniani (Amir, 1994; Sherrif, 1994). Asili hasa ya lugha hii adhimu ni mwambao wa pwani ya bahari ya Hindi kuanzia Kaskazini mpaka Kusini (Massamba 2002; Nabhany, 1998; Adamu, 2000). Kwa minajili hiyo basi, Kiswahili kimekuwa na lahaja mbalimbali kulingana na maeneo ya Kijiografia ya wazungumzaji wake. Miongoni mwa lahaja za lugha ya Kiswahili ni Chimwiini, Kiunguja, Kibajuni, Kipate, Kisui, Kiamu, Kimvita, Kitukuu Chichifundi, Kimwali, Kivumba, Kimtang'ata, Kimrima, Kipemba, Kimakunduchi, Kitumbatu, Kingwana/Kilungwana, Kinganzija/Kikomoro, Ki-Kilwa, Kivyomvu, Ki-Kisiju/Ki-Mafia (Nabhany: 1998).

Kufuatiya kuwepo kwa lahaja mbalimbali za lugha ya Kiswahili, wanazuoni kadhaa wamezifanyia tafiti kwa kiasi fulani ambacho hatuwezi kusema ni cha kutocheleza. Hata hivyo, tafiti zao ni muhimu sana katika kusukuma mbele utafiti wetu ambao unalenga kuchunguza maendeleo ya lugha ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu katika maisha yake ya kila siku. Tafiti hizo tulizipitia kwa kina kama ifuatavyo:

Whiteley (1969) alitafiti kuhusu lahaja ya Kimtang'ata na kubainisha kwamba, kuwepo kwa lahaja anuai katika lugha ya Kiswahili kunaonesha tofauti za

Kilughawiya kutoka lahaja moja na nyingine. Tofauti hizo la Kilughawiya ni pamoja na tofauti za kimsamiati katika lahaja za lugha ya Kiswahili. Kimsingi tunakubaliana na mawazo ya Whiteley (1969) kwa asilimia mia moja kwa kuwa utofauti wa Kilughawiya katika lahaja za Kiswahili unaonesha kwamba, Kiswahili si Kiarabu. Vilevile, inaonesha kwamba, Kiswahili hakikuathiriwa na Kiarabu pekee bali nacho kimekiathiri Kiarabu. Kama hali ingekuwa sivyo basi tofauti za Kilughawiya na Kilughawiya Jamii tunazoziona katika lahaja za Kiswahili zisingekuwapo. Hivyo basi, utafiti huu unalenga kubainisha namna Kiswahili kilivyoathiri jamii ya Kiarabu kupitia mtazamo wa Kilughawiya Jamii katika maisha yao ya kila siku.

Mohamed (1994) alifanya utafiti juu ya lahaja za Kipemba na Kiunguja. Utafiti huu ulibaini kwamba lahaja hizi mbili zinatofauti za Kilughawiya kama vile Kifonolojia, Kimofolojia na Kisintaksia. Matokeo ya utafiti huu ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti ulio mbele yangu. Ninasema hivi kwa msingi, kwamba kama Kiswahili kingekuwa kinatokana na Kiarabu na kwamba, Kiarabu ndicho kilichokiathiri sana Kiswahili ni wazi tafauti hizi zisingekuwepo. Maana ya maelezo haya ni kwamba, kama Kiswahili kingekuwa kimeathiriwa sana na Kiarabu basi lahaja zote zingekuwa sawa Kilughawiya. Mawazo haya yanatoa hoja madhubuti inayonipa nguvu ya kitaalimu kuchungua maendeleo ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu katika maisha yake ya kila siku.

Maganga (1991) katika tasinifu yake ya uzamivu, amechunguza lahaja tatu; Kipemba, Kimakunduchi na Kitumbatu kwa kuzihusisha na Kiunguja. Lengo la utafiti wake lilikuwa ni kuchunguza mofolojia ya lahaja hizo na kuhusianisha na ile

ya Kiunguja. Utafiti wake ulibainisha kwamba, mofolojia ya lahaja tajwa inatafautiana na kufanana katika vipengele kadhaa vya Kilughawiya. Tafauti hizo zipo katika viambishi awali, mzizi na viambishi tamati, pamoja na masuala ya alomofu na alofoni mbalimbali zinazojitokeza katika mofolojia ya maneno katika lahaja tajwa. Utafiti wa Maganga unatoa mwanga wa kutosha kusukuma mbele utafiti wetu ingawa haukujihusisha sana na kuchunguza kuathiriana baina ya Kiswahili na Kiarabu. Kumbe lahaja za Kiswahili zimeathiriana kwa kiasi kikubwa basi si jambo la ajabu kwamba Kiswahili nacho kimekiathiri Kiarabu kama kilivyoathiriwa pia. Utafiti huu unalenga kulichunguza suala hili kwa undani na umakini mkubwa ili kutengua athari kwamba Kiswahili ndiyo kimeathiriwa na Kiarabu huku chenyewe hakikukiathiri Kiarabu kwa kutumia taalimu ya isimu jamii.

Masebo na Nyangwine (2002) nao wamezungumzia lugha ya Kiswahili pamoja na lahaja zake japo kwa muhtasari. Katika ufafanuzi wao wa maana ya lahaja wameonesha kuwa licha ya Kiswahili kuwa na lahaja zake, bado kuna tafauti kadhaa zinazojitokeza baina ya lahaja hizo. Tafauti hizo ni kama vile lafudhi, fonolojia (matamshi) na msamiati. Maelezo haya yana umuhimu mkubwa katika kufanikisha utafiti huu. Masebo na Nyangwine (2002) wanatoa mwongozo kwamba, katika kutafiti juu ya kuathiriana baina ya lugha za Kiswahili na Kiarabu kumakinikia vipengele vya lafudhi fonolojia na msamiati. Hata hivyo, si vipengele hivi vilivyoshughulikiwa katika na badala yake ni masuala ya kilughawuya jamii ndiyo hasa yaliyoshughulikiwa.

Mbaabu (2003) amezungumzia kwa upana historia na usanifishaji wa Kiswahili. Kazi yake hii imeweka msisitizo zaidi juu ya uteuzi wa lahaja iliyosanifiwa na sababu za kuteuliwa lahaja hiyo. Katika ufafanuzi wake Mbaabu (2003) anaeleza kwamba lahaja ya Kimvita na ile ya Kiunguja ndizo zilikuwa katika ushindani mkubwa na hatimaye baada ya vigezo mbalimbali lahaja ya Kiunguja ikateuliwa na kupewa hadhi ya kusanifiwa na kuwa Kiswahili Sanifu (Massamba 2004). Sengo (2012 tarehe, 26 June) katika mazungumzo na mimi anaeleza kwamba,

Lahaja ya Kiunguja inayodaiwa kuteuliwa na kusanifiwa ni suala la kughushi tu na halina mashiko yoyote ya kitaalimu. Hiyo inayosemwa ni lahaja ya Kiunguja ni kishangani cha kanisani walipofikiya maaskofu na madaktari Stere na Krapf. Hivyo kudahili kwamba lahaja ya Kiunguja ilisanifiwa na kuwa Kiswahili sanifu si sahihi.

Mawazo ya Sengo (2012 tarehe, 26 June) na Mbaabu (2003) yanatoa mwangaza kwa mtafiti katika kufahamu historia ya lugha ya Kiswahili japo kwa muhtasari. Hii imesaidia katika kuchunguza juu ya maendeleo ya lugha ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu katika maisha yake ya kila siku kwa kutazama historia ya mahusiano ya lugha hizi mbili.

Kitala (2006) akizungumziya juu ya ripoti ya semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu (UWAVITA) ameeleza kuwa nafasi nyingine ya utamaduni uliyo ndani ya lugha ya Kiswahili hubainika katika lahaja zake. Katika kuzisifia lahaja za Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi anasema kuwa, zimehifadhi utajiri mkubwa wa msamiati unaoafikiana na shughuli za kila siku za jamii husika. Katika kuthibitisha hilo Kitala (2006) ameitaja kamusi ya Kitumbatu ambayo ina misamiati mingi ihusuyo uvuvi na mazao ya baharini.

Ninakubaliana na mawazo ya Kitala (2006) kwamba, lugha ndicho chombo cha kubebea na kuhifadhiya utamaduni wa jamii yoyote ile duniani (Mlacha, 1984; Ohly, 1977 Senkoro, 1976; Mlacha, 1996). Kihore (1984; 2003) wanasema kwamba, utamaduni wa lugha ya Kiswahili na Waswahili umeathiriwa sana na utamaduni wa Kiarabu na lugha ya Kiarabu. Harris (1962) akathubutu kueleza kwamba, asili ya ushairi wa Kiswahili ni fasihi ya Kiarabu na dini ya Kiislamu kwa kuwa kuna vipengele vingi vya Kiarabu vinavyojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Kimsingi maelezo haya si sahihi sana kwa kuwa yameegemea upande mmoja tu na kusahau kwamba hata Kiswahili nacho kimekiathiri Kiarabu na utamaduni wake. Mulokozi na Sengo (1995) waliipinga vikali hoja ya Harris (1962) na kuonesha kwamba asili ya ushairi wa Kiswahili ni fasihi na ngoma za Waswahili wenyewe na kuchangiwa na makabila mengine ya Afrika. Vilevile walikubali kwamba zipo athari kadhaa za fasihi ya Kiarabu katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu umeonesha namna pia Kiswahili kilivyoathiri utamaduni wa jamii ya Kiarabu iishio katika ukanda wa Pwani ya Afrika ya Mashariki.

Mwansoko (1991) amesisitiza sana juu ya kuifanyia utafiti zaidi lugha ya Kiswahili ili iwe ni miongoni mwa dhamira za makusudi za kuikuza na kuieneza lugha hiyo. Ingawa msisitizo wake upo katika lahaja zaidi, bado unatoa mwamko wa kuitafiti lugha ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali kama ninavyofanya katika utafiti huu. Awali alieleza kuwa lugha ni mseto wa vilugha mbalimbali. Kama Kiswahili kimejengwa na lahaja mbalimbali yamkinika pia ndani yake zimo lugha nyingine kadhaa zilizoimarisha lugha hii adhimu. Suala la kushangaza na kustaajibisha hapa ni kwamba, lugha mbalimbali kama vile Kiingereza, Kijerumani na Kiarabu nazo pia

zimeathiriwa na lugha mbalimbali duniani lakini hazishadidiwi kuwa zimekopa kama ilivyo kwa Kiswahili. Hali hii ilitoa msukumo kwangu kufanya utafiti wa kina ili kuainisha namna Kiswahili na Kiarabu zilivyoathiriana ili kutengua nadharia kwamba, Kiswahili tu ndiyo kimeathiriwa na Kiarabu bali Kiswahili nacho kimeathiri jamii ya Kiarabu iishio katika Pwani ya Afrika ya Mashariki katika utendaji wao wa maisha ya kila siku.

Mapitio niliyoyapitia katika sehemu hii ni muhimu sana katika kusukuma mbele utafiti wangu. Mapitio yameonesha pengo la kiutafiti ambalo lilihitaji kujazwa/kuziba pale utafiti huu ulipokamilika. Lugha ya Kiswahili ina lahaja mbalimbali na lahaja hizo hutafautiana baina yake na nyenzake katika vipengele vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantikia. Kwa msingi huu, imebainika kwamba, Kiswahili ni lugha huru na inapokea athari kutoka lugha mbalimbali bila kunyang'anywa uhuru wake. Kama ingenyang'anywa uhuru wake basi lahaja zote zingefanana kwa kuwa zimeathiriwa au zimetokana na lugha ya Kiarabu. Vile vile, tumeona kwamba, Kiswahili nacho kinaathiri lugha nyingine kama vile Kiarabu lakini mpaka sasa hakuna utafiti wa kina uliofanywa katika uwanja huu. Utafiti huu ulikusudia kujaza pengo hili la kiutafiti kwa kuchunguza maendeleo ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu iishio katika ukanda wa Afrika Mashariki katika maisha yao ya kila siku.

3.2 Mahusiano baina ya Kiswahili na Kiarabu

Inasemekana kwamba lugha ya Kiarabu imeathiri sana lugha ya Kiswahili tangu zamani kuliko vile ilivyoathiri lugha nyingine (Safari, 1980:vi katika Mohamed,

2006) kiasi cha baadhi ya wanalughawiya kudai kuwa Kiswahili ni Kiarabu. Hata hivyo, Kiswahili na Kiarabu hazimo katika kundi au familia moja yaani hazina mzazi mmoja (Bosha, 1994:15 katika Mohamed, 2006). Lugha ya Kiarabu si lugha asiliya ya Afrika bali ni katika karne ya saba ambapo Swahaba Umar Ibn Khattabi alipotuma jeshi la kuivamia nchi ya Misri ndipo Kiarabu kilipoingia katika Bara la Afrika lililokuwa na lugha zake nyingine ikiwemo Kiswahili. Ni katika karne hiyo hiyo Waarabu kutoka Oman na Yemen walipofika Afrika ya Mashariki kwa niya za kufanya biashara na Waswahili.

Kwa msingi huu basi, Waswahili walichanganyika na Waarabu na kuoleana na kuunga undugu wa damu baina yao. Uzurupo maeneo ya mwambao wa pwani ya Afrika Mashariki utaona namna Waswahili walivyo na ufanano wa rangi na Waarabu watokao sehemu tulizozitaja. Kwa kuwa lengo la Waarabu lilikuwa ni kufanya biashara na Waswahili, lugha za Kiarabu na Kiswahili zilitumika kama chombo cha kufanikisha biashara baina yao (Nabhany 1998; Abdulazizi, 1992; Sengo, 1985). Ni katika kutumika sambamba kwa lugha hizi mbili ndipo maathiriano yalipotokea. Hata hivyo, wanazuoni kama vile Kihore (1984; 2003) Harris (1962) na Massamba (2002) wanazungumza juu ya Kiswahili kuathiriwa na Kiarabu, Kifonolojia, Kisintakisia Kimofolojia, Kisemantikia na Kimsamiati bila kuonesha namna Kiswahili nacho kilivyokiathiri Kiarabu. Utafiti huu ulilenga kuziba pengo hili la kiutafiti kwa kuchunguza maendeleo ya Kiswahili na namna kilivyoathiri jamii ya Kiarabu katika maisha yake ya kila siku.

Lugha za Kiswahili na Kiarabu zina historia ndefu sana kiasi kwamba hati za mwanzo kabisa katika kuandikiya Kiswahili zilikuwa ni hati za Kiarabu (Abdulazizi 1992; Abdul –Latif 1998). Kihore (2003:167) anamnukuu Ali (1966:13-21) kwamba,

Maandishi ya Kiswahili yaliyoandikwa kwa Kiswahili yaliyokuwa na namna fulani ya maendeleo ya lugha hii. Anasisitiza kwamba Kiswahili katika historia yake yote ya kuandikwa, maneno yake yameandikwa kama yanavyotamkwa na hali hii anaona haikufuatwa vyema katika uandishi wa Kiswahili Sanifu. Hali hii imesababishwa na tofauti zilizotokana na Kiswahili kubadilishwa hati ya uandishi, toka hati za Kiarabu zilizotumika hapo mwanzo hadi zile za kilatini zinazotuika mpaka hivi leo.

Maelezo haya yanatoa ushahidi kwamba, Kiswahili kilianza kuandikwa katika hati za lugha ya Kiarabu na baadaye kuandikwa kwa hati za Kirumi kutokana na ughushi ulioitwa wa kusanifisha Kiswahili (Sengo, 2012 katika mazungumzo). Maelezo haya yanaonesha bayana kwamba, ipo nafasi kubwa ya kuathiriana kwa lugha hizi mbili hasa kuzingatiwa kwamba, hati za lugha moja zilitumika kuandikiya lugha nyingine. Hata hivyo wanataalimu wengi hawajaona hoja hii kuwa ni ya msingi kwa kuwa imezoeleka kwamba, lugha ya mtawala ndiyo bora kuliko ya mtawaliwa. Hivyo lugha ya mtawaliwa haiwezi kuathiri ile ya mtawaliwa (Krapf, 1850:7-11). Mtazamo huu ni finyu na utafiti wangu umeshughulikia kwa kina na kisha kuukanusha/kuutegua. Nilifanya hivyo kwa kuchunguza maendeleo ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu katika maisha yake ya kila siku.

3.3 Suala la Lugha Kukopa Msamiati Kutoka Lugha Nyingine

Lugha ya Kiswahili kama zilivyo lugha nyingine duniani huchukua maneno kutoka lugha mbalimbali na kuyatumia katika mawasiliano ya shughuli za kila siku za wazungumzaji wake (Massamba, 2002). Kwa wanataalimu wengi kama hawa

tuliyowataja huiita hali hii kuwa ni ya kukopa maneno/msamiati kutoka lugha mbalimbali . Mawazo haya hatukubaliani nayo hata kidogo ila kwa sasa tuachie hapa kwanza halafu tutaeleza zaidi baadaye. Kwa mujibu wa Massamba (2002) anasema kwamba, Kiswahili kimekopa msamiati kutoka lugha mbalimbali duniani lakini zaidi katika Kiarabu. Kiswahili kina jumla ya asilimia 60 ya msamiati wa kibantu, asilimia 30 ya msamiati wa Kiarabu na asilimia 10 ya lugha nyingine kama vile Kiingereza, Kijerumani na Kireno kwa kutaja lugha chache. Hivyo, Kiswahili kinaonekana kuchukuwa msamiati wa lugha ya Kiarabu kwa asilimia kubwa kiasi kwamba wanazuoni kuhitimisha kwamba Kiswahili hakina msamiati wa kutosha na hivyo ni Kiarabu na siyo Kiswahili. Nabhany (1978:13) anasema,

Nasikitishwa na usemi wa baadhi ya watu kuwa Kiswahili ni lugha ambayo haijitoshelezi kwa upande wa msamiati. Mimi sikubaliani na dai hili. Naamini Kiswahili kina msamiati wa kutosha kama lugha nyinginezo kubwa za ulimwengu. Na ikiwa hakuna maneno ya kueleza mambo mapya yaliyozuka, Waswahili waweze kubuni maneno bila taabu. Hivyo ndivyo hapo kale Waswahili walivyo kuwa wakikijenga Kiswahili kwa kubuni maneno mapya palipokuwa na haja ya kufanya hivyo.

Maelezo ya Nabhany (1978) yana umuhimu mkubwa katika kusukuma mbele utafiti huu na tunakubaliana nayo kwa asilimia mia moja. Lugha ya Kiswahili haijapata kuwa na upungufu wa msamiati na pale jamii mbili zenye lugha tafauti zinapokutana ni lazima kutatokea maathiriano ya Kilughawiya na Kilughawiya Jamii baina ya lugha hizo. Maathiriano haya hufanya msamiati wa lugha moja kuchukuliwa na kutumiwa na wazungumzaji wa lugha nyingine. Kwa mtazamo wangu, hali hii haiwezi kuitwa ni kukopa maneno kama wanavyoita akina Massamba (2002). Abdulazizi (1992:80) anatoa muhtasari juu ya maarifa ambayo pia yanashadidiwa na Williamson (1947) kwamba;

Chanzo kikuu cha mkopo wa msamiati wa lugha ya Kiswahili ni Kiarabu. Tena ni Kiarabu cha mwambao wa pwani ya Kusini mwa nchi za Kiarabu. Kiarabu hicho ni kile kilichopo katika Qur-an, hadithi na katika kazi mbalimbali zihusuzo taalimu ya dini ya Kiislamu. Vilevile Kiarabu kimekopesha msamiati mwingi katika lugha za Hausa na Fulani, (Tafsiri yangu).

Maelezo haya yanatoa mtazamo kwamba, lugha ya Kiswahili imechukuwa msamiati wa maneno kutoka Kiarabu na kuyatumia. Hili sina tatizo nalo, ila napenda kuuliza swali; hivi mkopo si makubaliano baina ya mkopaji na mkopeshaji kwamba, baada ya muda uliopangwa mkopo utarudishwa aidha kwa riba au pasipo riba? Hivyo basi, lugha ipi italipa nyingine nini na kwa riba ipi? Kwa hakika huu ni upotoshaji wa mambo ambao mwisho hujenga hisiya kwamba, Kiswahili ni lugha iliyotokana na Kiarabu. Sengo (2005, katika Mohamed, 2006) anasema kwamba, lugha hazikopi kutoka lugha nyingine bali zinakula katika sahani moja. Lugha haikopi maneno bali huchukua maneno na kuyatumiya katika mawasiliano ya watumiaji wake. Mawazo ya Sengo (ameshatajwa) yanasukuma mbele utafiti wangu kwa msingi kwamba, kama lugha zinakulana tena katika sahani moja; Kiswahili na Kiarabu zimekulanaje? Nitajibu swali hili kwa kuangalia kuathiriana baina ya Kiswahili na Kiarabu. Ali (1966:16) anasema,

Sehemu kubwa ya watu waliotia maneno ya Kiarabu katika Kiswahili ni watu wa pwani na katika sehemu za bara ni watu wa miji kama vile Tabora na Kigoma – Ujiji kwa kuwa watu hawa waliwapenda Waarabu na ustaarabu wao, kama hivi leo watu wanavyopenda ustaarabu wa wazungu hata wakawaoza binti zao waliipenda lugha yao. Kwa kupenda lugha yao, waliyachukuwa maneno yao na kuyatia katika Kiswahili. Kwa kuwa waliyapenda matamshi yao, maneno waliyoyachukuwa na kuyatia katika Kiswahili walijaribu walivyoweza kuyabakisha maneno yao kama yalivyo.

Kimsingi, hatukubaliani na maelezo ya Ali (1966) kwani mawazo haya ni ya kikoloni kwamba, cha mtawala ndio bora kuliko cha mtawaliwa. Ninasema hivi kwa kuwa sijapata kuona kuwa Waarabu nao walipenda lugha ya Kiswahili na kuchukuwa maneno ya Kiswahili na kuyaweka katika Kiarabu. Nijuavyo mimi ni kwamba, lugha hujikuta tu inatumiya maneno ya lugha nyingine kulingana na mazingira na muktadha na siyo suala la kupenda. Utafiti huu ulilenga kutengua maelezo na nadhariya zenye mwelekeo wa Ali (1966) kwa kuchunguza maendeleo ya lugha ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu iishio katika Pwani ya Afrika ya Mashariki katika maisha yao ya kila siku.

3.4 Fasihi ya Kiswahili na Kiarabu

Itakuwa si jambo la busara kwa mtafiti yeyote awaye kuzungumziya juu ya kuathiriana baina ya lugha za Kiswahili na Kiarabu bila kugusia mahusiano baina ya fasihi za lugha hizo. Kihore (2003:173) anasema “Ushairi katika Kiarabu umeitwa Kioo cha kweli cha maisha Uarabuni”. Mashairi ya Kiarabu yanaonyeshwa kuwa yalianza kabla ya Uislamu. Nicholson (1969:xxii) anasema “Kabla ya kuanza Uislamu (500-622AD) haya mashairi yalikuwa yamekwishafikia ukamilifu wa kisanaa unaofanya ushairi ufikiriwe kuwa ulianza mapema mno.

Ninakubaliana na maelezo kwamba, ushairi ulianza mapema kabla ya kuteremshwa Qur-an tukufu. Hii itanisaidia kupangua hoja kwamba ushairi wa Kiswahili asili yake ni Uislamu na Uarabu (Mulokozi na Sengo, 1995; Mulokozi 1996; Njogu na Chimera 1999. Wamitila, 2002; 2008). Wanatalimu hawa wanaeleza kwamba, ushairi ulianza pale tu binadamu walipoanza kuwasiliana kwa kutumia lugha na

kufanya kazi mbalimbali (Omary, 2011). Kwa maelezo haya ni dhahiri kwamba, Waswahili kama walivyo Waarabu na jamii mbalimbali duniani wanao ushairi wao ambao Waarabu waliwakuta nao walipokuja katika Pwani ya Afrika Mashariki. Kama hivyo ndivyo, ushairi wa Kiswahili uliathiriana na ule wa Kiarabu na siyo tu ushairi wa Kiarabu uliathiri ushairi wa Kiswahili. Owhida (2006) amefanya utafiti juu ya kufanana na kutofautiana baina ya ushairi wa Kiswahili na ule wa Kiarabu na kuonesha kwamba fani hizi zimeathiriana sana katika fani na maudhui.

Kihore (2003) na Owhida (2006) wanaonesha kwamba, ushairi wa Kiswahili na Kiarabu umeathiriana katika miundo ya mashairi (beti/mistari, vina na mizani na katika maudhui. Hata hivyo, zipo tofauti pia katika vipengele hivyo ambavyo kwavyo hutanabahisha kwamba, Kiswahili na Kiarabu ni lugha mbili tofauti na hivyo si sahihi kudai kwamba, Kiswahili kimetokana na Kiarabu. Hivyo basi, kwa msaada wa fani ya ushairi wa Kiswahili na Kiarabu nimefanikisha kuchunguza maendeleo ya Kiswahili na athari zake kwa jamii ya Kiarabu iishio katika Pwani ya Afrika ya Mashariki katika maisha yao ya kila siku. Vilevile, kwa kuwa ushairi huzungumza masuala ya utamaduni wa jamii husika ilikuwa muafaka kwangu kubaini kuathiriana baina ya lugha hizi katika taalimu ya lughawiya jamii.

3.5 Kiswahili na Uislamu

Kiswahili ni miongoni mwa lugha mbalimbali zilizotumika katika kueneza dini ya Kiislamu katika mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki na sehemu za bara katika Tanganyika. Ziad (1998:13) anaeleza kwamba, ustaarabu wa Kiislamu uliwaunganisha pamoja Waarabu na Waswahili kiimani na kitamaduni (Abdulazizi,

1992:70; Wiliamson, 1947; Abdullatif 1998; Affrifah, 1998:65; Chomi, 1988: 360-372; Sherrif and Mazrui, 1993:130-142; Sengo, 1985; 2000 katika Mohamed,2006). Kwa kuwa Kiswahili kilitumika katika kueneza uislamu ambao ulikuja kupitia lugha ya Kiarabu ni ukweli usiopingika kwamba lugha ya Kiswahili na Kiarabu zimeathiriana kwa namna moja ama nyingine.

Mawazo haya yanausukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, Kiswahili kililazimika kutumia maneno na kanuni za Kilughawiya za Kiarabu kueneza Uislamu. Vivyo hivyo kwa yale ambayo hayakuwa rahisi kueleweka kwa wazungumzaji wa Kiswahili kwa Kiarabu, Kiswahili kililazimika kutumia kaida zake kufafanua suala au jambo husika ili lieleweke zaidi. Hali hii ilisababisha lugha hizi kuathiriana kimsamiati na kilughawiya jamii kwa ujumla. Hivyo basi, utafiti huu ulilenga kuchunguza namna Kiswahili na Kiarabu vilivyoathiriana ili kutengeneza nadharia kwamba, Kiswahili nacho kimeathiri jamii ya Kiarabu iishio katika Pwani ya Afrika Mashariki kupitia mtazamo wa kilughawiya jamii.

SURA YA NNE

MBINU ZA UTAFITI

4.1 Njia za Kufanyia Utafiti

Utafiti ni taalimu yenye mpangilio, taratibu na kanuni maalumu ya kutafuta ujuzi na maarifa juu ya jambo fulani (Cohen, 2000). Kothari (2008) anasema kwamba, utafiti ni nyenzo muhimu inayosaidia kufahamu tabia, mahusiano na mwenendo wa makundi mbalimbali ya wanajamii katika sehemu mbalimbali duniani. Utafiti wa aina hii huitwa utafiti wa sayansi za jamii.

4.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti huu ni uchunguzi kifani (case study) ambapo lugha mbili za Kiswahili na Kiarabu zilichunguzwa ili kubainisha namna zilivyoathiriana na zinavyoendelea kuathiriana Kilughawiya Jamii. Pia utafiti huu ulifanywa Zanzibar na Dar es Salaam. Kothari (2008) ameubainisha uchunguzi kifani kama ni mpango au mpangilio unaonesha jinsi na namna data zitakavyokusanywa na kuchambuliwa kwa kutumiya gharama nafuu. Isaack na Michael (1981) na Creswell (2009) wanasema kwamba, uchunguzi kifani hutoa fursa ya kuchunguza jambo kwa undani zaidi na kuhusisha vipengele mbalimbali vinavyounda ama kujenga jambo hilo. Robson (2007) na Yin (1994) wanahitimisha kwamba, mbinu ya uchunguzi kifani husaidiwa kupatikana kwa majibu ya maswali kama vile: Nini? kwa nini? Kwa vipi? Na kwa sababu gani? Na kadhalika. Kothari (2008) anakazia kwa kusema kuwa uchunguzi kifani humuwezesha mtafiti kuelewa muktadha na mahudhuriyo mazima ya utokeaji na utendekaji wa jambo fulani katika jamii. Kuathiriana kwa lugha za Kiswahili na

Kiarabu Kilughawiya jamii kulichunguzwa kwa mafanikio makubwa kupitiya mbinu ya uchunguzi kifani.

4.3 Maktabani

Makatabani ni mahali maalumu palipohifadhiwa nyaraka vitabu, majarida, magazeti, yenye taarifa mbalimbali kwa wasomaji na watafiti wa kada tofauti tofauti za taalimu (Ewan na Calvert 2000). Maktaba zilizotumika katika utafiti huu ni ile ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (sehemu ya East Africana), maktaba na makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, maktaba ya Taasisi ya Lugha za Kigeni Zanzibar, Maktaba kuu ya Taifa, maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar, Chuo cha Kiislamu Zanzibar na Chuo Kikuu cha Chukwani. Katika maktaba hizi nilipitia na kusoma vitabu, makala, tasnifu, magazeti na tafiti tangulizi zinazoendana na mada ya utafiti wangu.

Mtalaa huu uliniwezesha kufahamu watafiti wengine wamesema nini juu ya mada yangu na kuweza kubainisha pengo la kiutafiti nitakalolishughulikiya. Vilevile mapitio niliyopitia yalinisaidia kupata data na taarifa za kujaliziya zile zilizokusanywa maskanini na kisha kukamilisha madhumuni ya utafiti huu.

4.4 Maskanini

Utafiti huu ulikusanya data na taarifa mbalimbali zihusuzo mada ya utafiti katika maskani mbalimbali. Berg (2007:78) anasema kwamba, maskanini ni mahali ambapo watu wanaishi na mtafiti anapokwenda kutafiti hupata data na taarifa ambazo ni mpya, halisi, ghafi ambazo kwazo hazikuwahi kukusanywa na mtu mwingine yeyote kwa minajili ya utafiti kama wake. Hivyo basi, nilikutana na wasomi mbalimbali

hususani walimu wa somo la Kiswahili na Kiarabu wanaosomesha Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Kiislamu Zanzibar, Chukwani na wanataalimu waliopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaofahamu masuala ya Kiswahili na Kiarabu. Vilevile nilikutana na wanafunzi wa chuo hicho wanaojifunza masomo ya Kiswahili na Kiarabu ili kupata data na taarifa zilizokamilishana na zile tulikazokusanya kutoka maskanini kwa kufanya hivyo, niliweza kukamilisha malengo ya utafiti huu. Hivyo basi, maktaba kuu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Taasisi ya Lugha za Kigeni Zanzibar na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar ndizo zilizotumika katika ukusanyaji data za upili.

4.5 Vyanzo vya Data

4.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni data halisi kwa maana kwamba, zinakusanywa maskanini moja kwa moja tena kwa mara ya kwanza (Kothari 1992:95). Data hizi za msingi zilikusanywa kupitiya mbinu za mahojiano, hojaji, ushiriki na uchambuzi wa kimaudhui. Lengo la kuchagua mbinu hizi ni kusaidia kukusanya data na taarifa muafaka zenye kuonesha kuathiriana baina ya Kiswahili na Kiarabu. Maandiko na machapisho mengi yaliyopo yameonesha kwamba Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu lakini si Kiarabu kuathiriwa na Kiswahili. Data za msingi tulizokusanya ziliweza kuziba pengo hili la kiutafiti.

4.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Katika utafiti huu nilitumiya mbinu kadhaa za utafiti ambazo kwazo nilikusanya data na taarifa zilizojibu maswali ya utafiti. Miongoni mwa mbinu hizo ni hizi zifuatazo.

4.6.1 Mbinu ya Ushiriki

Ushiriki ni mbinu ya utafiti ambayo humlazimu mtafiti kushiriki katika shughuli au matendo mbalimbali yanayohusiana na utafiti wake (Yin, 1994). Wakati mtafiti anashiriki katika matendo au shughuli hizo, anakuwa anakusanya data na taarifa zinazojibu maswali ya utafiti husika (Nichols 1991). Kwa kuwa utafiti huu unahusu masuala ya kuathiriana kwa lugha ya Kiarabu na Kiswahili ni dhahiri mimi kama mtafiti nilishiriki katika kuzungumza lugha ya Kiarabu na watafitiwa ili kuona kama kuna athari zozote kutoka Kiswahili. Vilevile nilihudhuria katika mihadhara kadhaa ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili na Kiarabu katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Kiislamu Zanzibar na Chuo Kikuu cha Chukwani. Nilipohudhuria mihadhara hiyo ni wazi kwamba nilibaini maathiriano baina ya Kiswahili na Kiarabu kutoka kwa mwalimu na wanafunzi wake. Pia nilishiriki katika mazungumzo na mijadala mbalimbali katika vikundi vya marika mbalimbali maskanini Zanzibar ili kuona ni namna gani lugha hizi mbili zinaathiriana.

Kothari (2008) anasema kwamba, mbinu ya ushiriki ni bora katika kumpatiya mtafiti data hai na halisi kwa kuwa naye ni sehemu ya uzalishaji wa data hizo. Hivyo ushiriki husaidia kupatikana kwa data za kuaminika na za uhakika kuwezesha kujibu maswali ya utafiti (Young,1984). Hata hivyo, Kothari (2008) anaonya kwamba, mbinu ya ushiriki humfanya mtafiti kutumia muda mwingi sana na hivyo asipokuwa

makini hatamaliza utafiti wake katika muda uliopangwa. Ili kukabiliana na upungufu huu wa mbinu hii nilitumiya mbinu nyingine pia kama mahojiano na hojaji katika kukusanya data.

4.6.2 Mbinu ya Mahojiano

Mahojiano ni mbinu ya utafiti inayomkutanisha mtafiti na watafitiwa wake ana kwa ana na kufanya mazungumzo. Mazungumzo au mahojiano hayo hufanywa kwa utaratibu maalumu (Babbie 1991). Utaratibu huo ni mtafiti anaandaa maswali ambayo humuuliza mtafitiwa na kumpa nafasi ya kujibu maswali hayo (Berg, 2007:89). Kadiri mtafitiwa anavyojibu maswali/anavyojieleza ndivyo huibua maswali zaidi yanayosaidia upatikanaji wa data zinazojibu maswali ya utafiti husika. Druckman (2005:68) anasema kwamba, watafitiwa hutoa ushirikiano zaidi katika ukusanyaji wa data kwa kutumiya mbinu ya mahojiano kuliko mbinu nyingine.

Hivyo basi, mtafiti alitumiya mahojiano ya siri na ya wazi katika ukusanyaji wa data. Maswali funge yalitumiwa pale ambapo zinahitajika data au taarifa maalumu, huku maswali si funge yakitumiwa kumpa mtafitiwa nafasi ya kutosha kujieleza awezavyo juu ya mambo mbalimbali yahasuyo mada ya utafiti. Mahojiano yalifanywa baina ya mtafiti na walimu wa masomo ya Kiarabu na Kiswahili, wanazuoni maarufu wa Kiswahili na Kiarabu Zanzibar na Dar es Salaam. Mbinu hii kwa hakika ilisaidia kukamilisha data na taarifa zilizokusanywa kupitiya mbinu za ushiriki na upitiaji wa nyaraka mbalimbali.

4.6.3 Upitiaji wa Nyaraka

Mosha (2004) anasema kwamba, upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambapo taarifa hukusanywa kutoka katika machapisho mbalimbali yanayohusiana na utafiti husika. Data zinazohusiana na mada hii ya utafiti zilikusanywa katika maktaba kuu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Maktaba kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Maktaba ya Taasisi za Taaluma ya Kiswahili na Makavazi yake, Maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na Maktaba kuu ya Taifa, Chuo cha Kiislamu Zanzibar na Chuo Kikuu cha Chukwani. Katika maktaba hizi nilipitiya vitabu, makala, magazeti, tasinifu na ripoti mbalimbali zenye taarifa zinazohusiana na mada yangu ya utafiti.

Mbinu hii ya utafiti iliniwezesha kubaini maathiriano yaliyopo baina ya Kiswahili na Kiarabu yaliyokwishaandikwa. Maathiriano hayo yanaweza kuwa ni ya Kimsamiati, Kilughawiya, kimaandishi, kimazungumzo nakadhalika. Vilevile maandiko hayo yanaweza kubainisha chanzo na asili ya maathiriano hayo. Pia, ilisaidia kubaini mitazamo mbalimbali juu ya kuathiriana kwa lugha hizi mbili kwamba, Kiswahili kimeathiriwa tu au nacho kimekiathiri Kiarabu, kwa nini na kwa vipi? Mbinu ya upitiaji wa nyaraka ilisaidia kujibu swali hili.

4.6.4 Uchambuzi wa Kimaudhui (Content Analysis)

Uchambuzi wa kimaudhui ni mbinu ya kukusanya data aidha zile za msingi au za upili kwa namna ya kusoma matini zihusianazo na mada husika kwa umakini mkubwa na kuzifanyia uchambuzi ili ziweze kujibu maswali ya utafiti husika (Newman, 2006:222 na Babbie, 1999:205). Mbinu hii iliniwezesha kuteuwa

maandiko na machapisho kadhaa yahusianayo na mada ya utafiti na kuyapitiya ili kuona namna lugha za Kiswahili na Kiarabu zinavyoathiriana. Yapo maandiko kadhaa yaliyoandikwa juu ya kufanana na kutofautiana baina ya ushairi wa Kiswahili na ushairi wa Kiarabu (Owhida, 2006); Ufundishaji wa Kiswahili nchini Libya (Mohamed, 2006) na kadhalika. niliyasoma maandiko haya kwa kina ili kubaini namna Kiswahili na Kiarabu zinayoathiriana kilughawiya jamii. Niya ya watafiti hawa haikuwa kuonesha kuathiriana kwa lugha mbili tajwa ila kwa kuzitafiti kwa kina tuliweza kubaini maathiriano baina ya lugha husika.

Kimsingi ili kufanikisha kufanikiwa kwa mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui niliandaa shajara maalumu kwa ajili ya kunukuu data na taarifa mbalimbali ambazo zinaonesha kuathiriana baina ya Kiswahili na Kiarabu. Data zilizokusanywa zilihifadhiwa vizuri na kuwekwa katika makundi maalumu kwa zile zinazofanana ili kurahisisha zoezi la uchambuzi wa data.

4.7 Uteuzi wa Watafitiwa

Babbie (1999) na Kigume (2010) wanaeleza kwamba, uteuzi wa watafitiwa ni kitendo cha kuteua watu au kitu maalumu kitakacho fanyiwa utafiti. Utafiti kama huu ambao ni wa miaka isiyozidi mitatu hauwezi kufanywa kwa kuwashirikisha wanajamii wote wa Zanzibar na Dar es Salaam. Hivyo niliteua watafitiwa 70 katika utafiti huu. Watatafitiwa 10 walikuwa ni walimu wa lugha ya Kiswahili na Kiarabu ambao waliteuliwa kwa kutumia sampuli lengwa (purposive sampling) watafitiwa 5 ni wazee mashuhuri na magwiji katika Kiswahili na Kiarabu ambao nao waliteuliwa kwa kutumia sampuli lengwa na tajwa (snowball). Watafitiwa 20 ni wanafunzi

wanaojifunza Kiswahili na Kiarabu katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA) ambao niliwateuwa kwa kutumiya sampuli nasibu. Watafitiwa 35 walikuwa ni wananchi wanaozungumza Kiswahili na Kiarabu katika mji wa Unguja, ambao waliteuliwa kwa kutumiya sampuli lengwa. Jedwali lifuatalo linaonesha muhtasari wa uteuzi wa watafitiwa.

Jedwali la 4.1:Uteuzi wa watafitiwa

Na	Aina ya Populesheni	Aina ya Watafitiwa	Jumla	Mbinu ya uteuzi
1.	Chuo Kikuu cha SUZA	Walimu wa Kisw & Kiarabu	10	Lengwa
2.	Chuo Kikuu cha SUZA	Wanafunzi	20	Nasibu
3.	Maskanini	Wazee	35	Lengwa na tajwa
4.	Maskanini	Wananchi	35	Lengwa
	Jumla	Jumla	100	

4.8 Usahihi (validity) na Kuaminika (reliability) kwa Mbinu za Utafiti

4.8.1 Usahihi wa Data

Cohen, na Wenzake (2000) wanatuambia kuwa, usahihi wa mbinu za kukusanyia data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data sahihi na za kuaminika. Ili kufanikisha upatikanaji wa data sahihi nilitumiya mbinu zaidi ya moja katika kukusanya data. Mbinu hizo ni; Ushiriki, Mahojiano, Uchambuzi wa Kimaudhui na Upitiaji wa Nyaraka. Usahihi wa mbinu hizi unatokana na ukweli kwamba mapungufu ya kila moja hukamilishwa na ubora wa mbinu nyingine. Vilevile,

usahihi wa mbinu zilizotumika katika utafiti huu zilijadiliwa katika mjadala baina ya mtafiti na msimamizi wake.

4.8.2 Kuaminika kwa Data

Kuaminika kwa data za utafiti kunatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa/kuzalisha matokeo yaleyale pale utafiti unaporudiwa kwa kutumia mbinu zile zile (Best na Khan, 2006). Kuaminika hujitokeza pale ambapo kunakuwa na uhusiano/ulingano katika taarifa zilizotolewa na watu wale wale kwa muda tofauti (Furlong na Lovelace, 2000). Katika utafiti huu, kuaminika kwa data kulihakikiwa kwa kutumia mbinu nne za ukusanyaji wa data zilizoainishwa katika sehemu ya njiya za ukusanyaji wa data hapo awali.

4.9 Maadili ya Utafiti

Kumar (1999) anaeleza kwamba miongoni mwa vitu muhimu anavyotakiwa kuzingatia mtafiti ni maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha kufanya utafiti pamoja na kutunza siri za watafitiwa. Hivyo basi katika utafiti huu, maadili ya utafiti yalizingatiwa kabla na baada ya kukusanya data.

SURA YA TANO

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

5.1 Uchambuzi wa Data

Baada ya kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji wa data, nilitakiwa kuchambua, kujadili na kuwasilisha data zilizokusanywa. Kothari (2008) anaeleza kwamba, uchambuzi wa data ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Uchambuzi wa data ni hatua muhimu sana katika kutafuta majibu ya tatizo la utafiti (Bogdan na Biklen, 1992).

Kwa msingi huu basi, niliongozwa na mbinu ya uchambuzi wa kinaelezo katika uchambuzi wa data za utafiti wangu. Mbinu hii ni muafaka katika uchambuzi wa masuala yanayohusu lugha kama anavyosema Omari (2009) alipomnukuu John (1997) kwamba, mbinu ya uchambuzi wa kinaelezo humruhusu mtafiti kusikiliza au kusoma machapisho mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti, kisha kuelewa mantiki yake na kuhusianisha na malengo ya utafiti husika.

Mbinu hii ya kiuchambuzi, huruhusu utolewaji wa maelezo ya kina juu ya data zilizokusanywa na mtafiti kwa namna ambayo itawezesha kujibu maswali ya utafiti husika. Naomba ieleweke kwamba, ninapozungumziya mbinu ya uchambuzi wa kinaelezo ninamaana kwamba nitachambua data kwa kuzitolea ufafanuzi wa kinaelezo usiohusisha kanuni mbalimbali za kimahesabu.

Data zilizokusanywa zilipangwa vizuri katika makundi mbalimbali yanayofanana (zikafanyiwa *coding*) ili kurahisisha uchambuzi wa data. Uchambuzi wa data

ulifanywa kwa kuzingatiya malengo na maswali ya utafiti. Kutokana na malengo hayo niliunda mada kuu na ndogondogo ambazo kwa hakika zilikidhi mahitaji ya malengo ya utafiti wangu. Katika mada hizo nilitoa maelezo ya kina kulingana na data zilikazo kusanywa.

5.2 Chimbuko la Lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili kama zilivyo lugha nyingine zote duniani ina asili na chimbuko lake. Hata hivyo, chimbuko na asili ya lugha ya Kiswahili imeelezwa na wataalamu mbalimbali kwa njia ya upotoshaji (Maganga, 1997). Kwa mfano, ananukuu gazeti la Sunday Nation, Nairobi 11/12/1977 kwamba:

Historia inaeleza waziwazi kwamba, Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha zaidi ya moja, na lugha kuu hasa si nyingine bali ni Kiarabu. Waarabu walipokuja kwenye pwani ya Mashariki mwa Afrika kabla ya enzi za unyonyaji na wakitawala, hawakuwa na njia yoyote ya kuwasiliana na wenyeji waliowakuta. Polepole, na ilibidi wafanye hivyo wakaunganisha kijanja baadhi ya sifa za lugha yao (kadiri ilivyowezekana) na lugha za kienyeji zilizokuwa zinazungumzwa pale mahali. Zilikuwapo lugha nyingi na bado zingalipo... Kigiriama, Kibanjuni, Kidigo, n.k. bila ya kuzitaja zile nyingine zilizoko Kaskazini na Kusini zaidi ya Pwani ya Mashariki mwa Afrika. Matokeo yake... Kiswahili. Baadhi ya maneno maarufu katika lugha hii yana asili ya Kiarabu; Salamu, Salama, chai, lakini n.k.”

Dondoo hili linadai kwamba, lugha ya Kiswahili ilianza pale Waarabu walipokuja katika Pwani ya Afrika ya Mashariki ambapo bila shaka huu ni upotoshaji mkubwa. Kwa hakika haiingii akilini kwamba, mgeni kutoka nje ambaye ana lugha tofauti na ile inayozungumzwa na wenyeji wake ajaribu kuingiza maneno ya lugha yake ngeni katika lugha ya wazawa na kisha kuifuata lugha ya awali na kuzalisha lugha mpya. Kinachowezekana ni kwamba, msamiati wa lugha ngeni unaweza kuathiri msamiati wa lugha zawa na hivyo lugha hiyo zawa ikawa na sehemu ya msamiati kutoka lugha

ya kigeni. Msamiati huo hautasemwa ni msamiati wa lugha ya kigeni tena bali ni msamiati wa lugha zawa kwa sababu ndio unaotumika katika lugha hiyo.

Upotoshaji mwingine unaotokeza katika dondoo hapo juu ni ule wa kuziita lugha za Kigirima, Kibanjuni, Kidigo n.k kwamba ni lugha za kienyeji. Ni dhahiri kwamba, nafasi ya lugha katika jamii yoyote iwayo ni kwa ajili ya kuwasiliana na inapokidhi mahitaji hayo basi hakuna shaka hiyo ni lugha kamili. Sasa suala la uenyeji na usasa wa lugha unatokea wapi? Profesa Sengo (2012 katika mazungumzo) anasema:

Utumizi wa neno lugha za kienyeji katika kueleza historia ya lugha ya Kiswahili ni makusudi kwa ajili ya kushusha hadhi ya lugha za jamii za Kiafrika na kutukuza zile za kigeni. Na hii kwa kawaida ndio tabia ya mtawala hasa mtawala wa Kikoloni. Mtawala huyu alitaka kila jambo alilolikuta katika jamii kuwa baya na la kishenzi na lile lake ndiyo bora ili aweze kutawala vizuri.

Mawazo ya Sengo (ameshatajwa) ni muhimu sana katika kusukuma mbele utafiti huu. Hatua ya kuziita lugha za jamii ya Waswahili kuwa ni za kienyeji tayari kisaikolojia Mswahili ataona lugha yake si chochote si lolote mbele ya lugha ya mabwana. Pili kwa kuziita lugha za jamii ya Waswahili kuwa ni lugha za kienyeji kunatoa uhalali wa lugha zao ama yao kuonekana kwamba imeathiri lugha ya Kiswahili na Kiswahili hakina hadhi ya kuiathiri lugha ya Kisasa. Huu ni upotoshaji mkubwa wa historia ya lugha ya Kiswahili.

Upotoshaji mwingine wa historia ya lugha ya Kiswahili ni pale anapodai kwamba, lugha ya Kiswahili ilitokana na kuungana kwa lugha za Kigirima Kibanjuni, Kidigo, Kipemba, Kiunguja n.k. Dai hili halina mashiko yoyote ya kitaaluma na kihistoria kwa sababu kila lugha katika hizo ina watumiaji wake na wazungumzaji wake na hii

inayoitwa imezaliwa kutokana na lugha hizo wazungumzaji wake ni akina nani?

Tulipofanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Unguja alieleza kwamba:

Sisi Waunguja lugha yetu ni Kiunguja, Wangazija lugha yao ni Kingazija ambazo zote ni sehemu ya lugha ya Kiswahili. Hili ni jambo la kawaida kabisa kwa lugha kuwa na matawi yake kutokana na wazungumzaji wake kuishi katika maeneo tofauti tofauti kijiografia, kiuchumi na kadhalika ambayo husababisha kutofautiana aidha kwa msamiati ama lafudhi ya msamiati.

Mtafitiwa huyu anaonesha kwamba, lugha za jamii zina nguvu ile ile katika jamii yake kama zilivyo lugha zinazoitwa za kisasa kwa jamii zao. Anasema kwamba, lugha yake yeye ni Kiunguja ambacho ni sehemu ya lugha kubwa iitwayo Kiswahili. Kwa mawazo haya ni dhahiri kwamba, hata huo unaoitwa usanifishaji wa lugha ni suala dhahania tu na halipo kabisa katika uhalisia.

Suala lingine la kiupotoshaji ni lile linalodai kwamba, Kiswahili ni Kiarabu kwa sababu baadhi ya msamiati wake una asili ya Kiarabu. Wazo hili halina mashiko kwa sababu kiasi cha msamiati wa lugha ya Kiarabu uliochukuliwa na lugha ya Kiswahili ni kidogo sana (Maganga 1997). Maganga (1997:5) anasema:

Wazo hili limeenea sana katika maandishi ya watu wa kawaida na ya wanataaluma nalo huchukua sura nyingi. Ni sawasawa na kusema kwamba, Kiingereza ambayo ni lugha yenye asili ya Kijerumani hasa ni lugha yenye asili ya Kirumi kutokana na athari ya Kifaransa iliyoingizwa katika karne zilizofuatia uvamizi wa Waromani. Wazo hili limevurugwa kwa sababu limeshindwa kutofautisha kile kinachorithishwa katika lugha na kile kinachoingizwa baadaye.

Dondoo hili linashadidia hoja kwamba, historia ya lugha ya Kiswahili imepotoshwa kwa makundi kabisa. Hii inatokana na ukweli kwamba, lugha ya Kiingereza kama ilivyokwisha elezwa hapo juu ina msamiati mwingi kutoka Kijerumani lakini haijawahi kuelezwa hata siku moja kwamba ni lugha ya Kijerumani.

Kimsingi, upotoshaji wa historia ya lugha ya Kiswahili unajitokeza pia katika jina lenyewe la lugha ya Kiswahili. Inadaiwa kwamba, Kiswahili ni jina linalotokana na neno la Kiarabu “Sahel” lenye maana ya pwani. Waarabu walipokuja katika pwani ya Afrika ya Mashariki walivutiwa sana na watu wa Pwani na utamaduni wa lugha ikiwemo katika kupendezwa huko na mambo hayo ndipo walipoamua kuita lugha ya watu hao kuwa ndio lugha ya “Sahel” yaani lugha ya Kiswahili (Khalidi, 2005). Kwa mtazamo ule ule, Sengo katika mazungumzo anahoji kwamba:

Waarabu ni watu wanaotoka katika mwambao wa bahari huko kwao. Vile katika Afrika kuna sehemu nyingi tu zenye mwambao ikiwemo Afrika Magharibi, Kaskazini na Kusini. Kwa nini huko kote kusitwe “Sahel” na lugha ya wale wanaozungumza lugha zao katika maeneo hayo nao waitwe “Waswahel”. Huu ni upotoshaji tu wa mambo ambao pia unajitokeza katika historia za vitu vingine kama vile utasikia mgunduzi wa mlima Kilimanjaro ni Mzungu, ziwa Victoria pia ni Mzungu.

Kimsingi, lugha ya Kiswahili ilikuwepo tangu kale kabla ya ujio wa wageni hao na wanajamii walikuwa wanaitumia lugha hii katika mawasiliano yao ya kila siku. Walichokifanya wageni ni kutoa majina ya vitu na majina hayo yakachukuliwa na siyo kukopwa na kuwa sehemu ya utamaduni wa jamii husika. Kwa mfano, tunaelezwa kwamba, Wachagga waishio mkoani Kilimanjaro waliuita mlima Kilimanjaro kama unavyojulikana leo “Kilima Kyaaro” na Wazungu walipopata taabu ya kutamka jina hilo ndio wakauita mlima huo Kilimanjaro. Hii haimaanishi kwamba, Wazungu ndio wagunduzi wa mlima Kilimanjaro. Na hivi ndiyo ilivyo kwa lugha ya Kiswahili.

Historia ya lugha ya Kiswahili na maendeleo yake inatokana na Waswahili wenyewe. Waswahili ni watu wanaoishi mwambaoni mwa Pwani ya Afrika

Mashariki tangu karne na karne wakishughulika na shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa huku lugha yao kuu ikiitwa Kiswahili. Itakumbukwa kwamba, lugha ya Kiswahili ina lahaja mbalimbali ambazo ndizo hasa kwa pamoja huunda lugha ya Kiswahili. Lahaja zinazozungumzwa hapa zilitokana na utofauti wa kimaeneo na kijiografia uliokuwepo katika ukanda wa Pwani ya Afrika ya Mashariki. Ukanda huu wa Pwani una maeneo kama vile Pate, Lamu, Mombasa, Pemba, Unguja, Sofala, Mafia, Malindi na kadhalika ambapo lugha ya Kiswahili ilizungumzwa kwa msamiati wa lafudhi tofauti huku msamiati mwingine ukifanana katika sehemu zote.

Kimsingi, Kiswahili kuwa ndio lugha ya mawasiliano katika ukanda mzima wa Pwani ya Afrika ya Mashariki ni dalili kwamba, Kiswahili ni lugha kubwa na pana ambayo haiwezi kuathiriwa na kuwa asili yake inatokana na Kiarabu. Mtafitiwa mmoja kutoka Pemba anasema:

Lugha ya Kipemba (Kipemba) ilianza pale Wapemba walipoanza kuwasiliana katika shughuli zao za kiuchumi na kijamii pamoja na utamaduni ambapo mazingira ya Kipemba ndiyo yaliyochangia kuundwa kwa msamiati wa Kipemba ambao ndio tunaoutumia na kila siku msamiati mpya unaibuka ili kuweza kukidhi mahitaji ya wazungumzaji.

Dondoo hili linaeleza kwamba, msamiati wa lugha huibuka ili kukidhi mahitaji ya jamii kiutamaduni kiuchumi na kijamii. Kiutamaduni kila jamii ina masuala yake ya mila, desturi, ndoa, matambiko, miiko, misiba, jando na unyago na kadhalika. Ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano katika vipengele tajwa vya kiutamaduni jamii hulazimika kuunda msamiati wake na hivyo ndivyo chimbuko la lugha hutokea. Vilevile, kiuchumi; kila jamii ina shughuli zake za kiuchumi, kama vile kilimo,

ufugaji, uvuvi, biashara na kadhalika ambapo msamiati wa lugha huibuka katika harakati za wananchi kuendesha vema shughuli zao za kiuchumi.

Kwa msingi huu, hakuna sababu ya kutafuta chimbuko la lugha ya Kiswahili nje ya jamii ya Waswahili. Lahaja zote za Kiswahili tulizozitaja na ambazo hatujazitaja zimetokana na harakati za jamii katika kuwasiliana na si vinginevyo. Suala la Waarabu kuja na kutawala katika upwa wa Afrika ya Mashariki kumechangia kusukuma mbele maendeleo ya Kiswahili katika kukiongezea msamiati na kukikuza zaidi. Hata hivyo, hii haikifanyi Kiswahili kuwa asili na chimbuko lake ni Kiarabu. Kiarabu kina kwao na kina watumiaji wake kama ilivyo Kiswahili kina kwao na kina watumiaji wake (Sengo, 2010).

5.3 Sababu Zilizowafanya Wanataalimu Mbalimbali Kudai Kwamba Kiswahili Kimeathiriwa Sana na Kiarabu

5.3.1 Utangulizi

Katika sehemu hii ninaeleza sababu mbalimbali zilizofanya wanataalimu mbalimbali kudai kwamba, Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu huku kulikosekana machapisho na utafiti wa kina juu ya namna Kiswahili nacho kilivyokiathiri Kiarabu. Nimeamua kuzibainisha sababu hizo ili kuonesha kwamba, si kweli kuwa Kiarabu ndicho kilichokiathiri sana Kiswahili bali pia hata Kiswahili nacho kimeathiri jamii ya Kiarabu iishio Pwani ya Afrika Mashariki na utamaduni wake. Ninaanza na sababu ya kwanza ambayo ni wataalamu wa mwanzo kutafiti na kuandika juu ya Lugha ya Kiswahili na fasihi yake walikuwa ni wageni wasiokuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu lugha ya Kiswahili na utamaduni wake.

5.3.1 Watafiti wa Mwanzo wa Kiswahili

Miongoni mwa sababu kubwa zilizofanya Kiswahili kusemekana kwamba kimeathiriwa sana na lugha ya Kiarabu na kwamba Kiswahili ni Kiarabu ni kutokana na watafiti wa mwanzo kutafiti kuhusu lugha ya Kiswahili kwanza kuwa ni wageni na pili kukosa maarifa ya kutosha kuhusu lugha ya Kiswahili na utamaduni wake. Mulokozi (2000) anaeleza kwamba:

These studies were of course, undertaken by Europeans (one may add colonialist) scholars for their own purposes. Such people came with distorted views about the African. They were not interested in studying Swahili Language and its Literature as Language and Literature of a given people at a given time and place, a people with its own history cultural values, feelings and emotions, but rather as one of the numerous jungle curiosities.... decided to spend all their lives trying to prove that Swahili Language and its poetry originated in Arabia and Persia..... Swahili is not a Bantu language per se but a product of a certain mythical intermarriage between Arabic and Bantu.

Tafiti hizi zilizofanywa na wa wazungu (wakoloni) ambao walikuwa na malengo yao binafsi. Watu hawa walikuwa na mtazamo hasi juu ya Waafrika na utamaduni wao. Hawakuwa na lengo la kutafiti lugha ya Kiswahili na fasihi yake kama lugha na fasihi ya watu kwa muda na makundi maalumu wenye historia yao, mila zao, mihemko yao... Watu hawa (Wazungu) waliamua kutumia maisha yao yote kujaribu kuthibitisha kwamba lugha ya Kiswahili na Ushairi wake vinatokana na lugha Kiarabu na Kipersia... Lugha ya Kiswahili si lugha ya Kibantu bali inatokana na kuoana baina ya Waarabu na Wabantu (Tafsiri yangu).

Maelezo haya yanaonesha kwamba, watafiti wa mwanzo kutafiti lugha ya Kiswahili hawakuwa na lengo la kuitafiti lugha ya Kiswahili kama lugha ya watu na utamaduni wao. Badala yake, walifanya utafiti wakiongozwa na mtazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili kuwa ni lugha ya kishenzi na utamaduni wake ni wa kishenzi. Mawazo haya yaliwafanya kuidharau lugha ya Kiswahili na hivyo kutofanya tafiti za kina na kisha kuishia kudai kwamba, Kiswahili kinatokana na lugha ya Kiarabu.

Lugha ya Kiarabu ilionekana kuwa ni lugha bora ya mabwana na Kiswahili ni lugha ya watwana kwa hali hiyo, lugha ya mabwana ndiyo inayoweza kiathiri lugha ya watwana haiwezi kuiathiri lugha ya mabwana kwa vyovyote vile. Mtazamo huu ndio uliowasukuma watafiti wengi kuishia kudai kwamba Kiswahili kinatoana na Kiarabu huku kikiwa hakuna tafiti zielezazo kwamba lugha ya Kiswahili nayo imeathiri lugha ya Kiarabu. Nilipofanya usaili na mtafitiwa mmoja huko Zanzibar alinieleza kuwa:

Waarabu na Wazungu waliokuwepo hapa Unguja waliona kwamba lugha yao ilikuwa ni bora kuliko Kiswahili ingawa waliruhusu Kiswahili kiendeleo kutumika katika shughuli mbalimbali kama chombo cha mawasiliano. Hawa watu walikuwa waajabu sana, wanaitumia lugha ya Kiswahili kunyonyea rasilimali zetu na kujitajirisha halafu tena wanaidharau lugha hiyo. Dharau kuhusu Kiswahili ziliwafikia watafiti ambao walitafiti Kiswahili kwa mtazamo hasi.

Kimsingi, sababu hii ndiyo hasa iliyochangia kutokuwa na tafiti kuhusu Kiswahili kukiathiri Kiarabu kwa kuona ni jambo lisilopingika kwamba, lugha mbili au zaidi zinapotumika kwa pamoja zote mbili huathiriana na si moja tu ndiyo huathiriwa (Mekacha, 2000). Kutokana na mkondo huu wa mawazo Knappert anaeleza kwamba, utamaduni wa Waswahili ni wa kigeni na si utamaduni wa Kiafrika na katika kuthibitisha mawazo yake haya alikusanya mashairi yenye maudhui ya Kiislamu na Kiarabu. Hivi ndivyo namna wale waliokuwa na mtazamo hasi juu ya lugha ya Kiswahili na Waswahili kwa ujumla walivyoamua kuishusha hadhi lugha hii adhimu na kuiita kuwa ni lugha ya Vizalia, Krioli na Pijni ya Kiarabu. Baada ya kutoa maelezo kuhusu sababu ya kwanza iliyofanya Kiswahili kuelezwa kuwa kimeathiriwa sana na Kiarabu na hivyo kuwa ni lugha iliyo na asili yake kutoka Uarabuni ni vema sasa tuangalie sababu nyingine.

5.3.3 Kiarabu Kufundishwa katika Madrasa

Dini ya Kiislamu iliingia katika ukanda wa Afrika Mashariki kunako karne ya saba ambapo Waarabu kutoka Oman walifika katika Pwani ya Afrika Mashariki kufanya biashara pamoja a kueneza dini ya Kiislamu na utamaduni wa Kiarabu. Kwa msingi huo basi, zilianzishwa madrasa katika maeneo ya Lamu, Mombasa, Pemba, Unguja, Kilwa, Bagamoyo na sehemu mbalimbali za Bara katika Tanzania na Afrika ya Kati. Ni katika madrasa hizo ndio wanafunzi wa kwanza kufundishwa kuandika kwa kutumia hati za Kiarabu. Zhukov (2004) anaeleza kwamba:

After Islam had been adopted, the traditional forms of transmission of social experience and education, that is oral traditions ceased to satisfy the spiritual needs of the ruling elite. Written traditions took the place of the oral ones and become the main instruments of cultural and ideological influence on the literate part of the society in the first place on its upper social strata, including representatives of a new layer of Muslim teachers (Shehe, walimu) that is the intellectuals of that time.

Baada ya dini ya Kiislamu kupokelewa, njia ya kuhifadhi na kuwasilisha elimu na uzoefu wa kitaaluma na kitamaduni ilibadilika kutoka ile ya masimulizi na kuwa ya maandishi. Lugha ya maandishi ilichukua nafasi ya lugha ya masimulizi ya mdomo kuwa ndiyo lugha ya kuhifadhi na kuwasilisha masuala ya kitamaduni na kifasihi kwa jamii husika. Tabaka la juu katika jamii ndiyo hasa waliokuwa wakitumia lugha ya maandishi (Kiarabu). Watu hao ni mashehe na walimu wa madrasa (Tafsiri yangu).

Maelezo haya yanaonesha kwamba, lugha ya maandishi ambayo ilikuwa ni Kiarabu ilichukua nafasi ya lugha ya masimulizi ambayo ilikuwa ni Kiswahili. Watu walianza kuvutiwa kujifunza lugha ya Kiarabu kupitia madrasa ili nao waingie katika kundi la watu bora katika jamii kutokana na hali hiyo hati za Kiarabu zilitumika kueleza masuala mbalimbali ya utamaduni wa Mwafrika. Kuandikwa na kuwasilishwa kwa masuala ya utamaduni wa Kiswahili kwa Kiarabu kuliwafanya wataalamu wa lugha

wa wakati huo kudai kwamba, Kiswahili ni Kiarabu kwa kuwa hati za Kiarabu zinatumika kueleza masuala ya Kiswahili.

Kimsingi, suala la lugha fulani kutumika kueleza utamaduni au masuala mbalimbali yahasuyo lugha nyingine ni jambo la kawaida na limekuwepo duniani kwa miaka mingi sasa. Kwa mfano, Kilatini kilitumika kwa miaka mingi sana kueleza tamaduni za mataifa mbalimbali ya Ulaya na hata siku moja hatujawahi kusikia kwamba, lugha kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kitaliano na Kijerumani kwamba, asili yake ni Kilatini. Lugha hizi zimeendelea kuitwa kwamba, ni lugha zenye asili yake kutokana na wanajamii wa nchi zilimoanza kuzungumzwa lugha hizo. Kwa mfano, Kiingereza asili yake ni katika nchi ya Uingereza na wanaozungumza lugha hiyo ambao ni wananchi wa Uingereza wanaitwa Waingereza. Kwa maelezo haya ni dhahiri kwamba, lugha moja kutumika katika kuelezea lugha nyingine hakuifanyi lugha elezewa kuwa asili yake inatokana na lugha inayotumika kuelezea. Nilifanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Dar es Salaam nilielezwa kuwa:

Ninavyofahamu mimi kwamba, kwa miaka mingi sasa, Kiingereza kimetumika kueleza masuala ya Kiswahili. Kwa mfano, wapo wanafunzi wa shahada za uzamili na uzamivu ambao wanaandika tasnifu zao kwa Kiingereza kueleza taalimu za Kiswahili. Walipomaliza walipewa shahada za Uzamili na uzamivu katika Kiswahili. Hata siku moja haijatokea kusikia kwamba Kiswahili asili yake ni Kiingereza kwa sababu Kiingereza kimetumika kueleza masuala mbalimbali ya lugha ya Kiswahili.

Maelezo haya yanaonesha bayana kwamba, lugha ya mabwana kama ilivyo Kiingereza hata kama imechukua maneno mengi kiasi gani kutoka Kilatini na lugha nyingine duniani asili yake itabaki kuwa ni ile ile na sio kutoka lugha ilimochukua maneno ama msamiati husika. Hata hivyo, lugha ya watwana kama ilivyojulikana

enzi hizo, Kiswahili kinaonekana kuwa ni lugha yenye asili yake kutokana na lugha ya Kiarabu kwa sababu imechukuwa maneno/msamiati mwingi kutoka lugha ya Kiarabu. Maelezo haya yanathibitisha kauli ya Mulokozi kwamba, wanaotoa mawazo haya hawakuwa na nia njema kwa lugha ya Kiswahili na Waswahili kwa ujumla na kwamba, walikuwa na nia yao ya kuidhoofisha lugha ya Kiswahili na Waswahili kwa ujumla. Hivyo basi, ni dhahiri kwamba, wataalamu mbalimbali wa lugha na fasihi ya Kiswahili wa Zamani kama vile Harris (1962) na Knapert (1971) wameitumia sababu hii kuthibitisha kwamba, Kiswahili pamoja na fasihi yake zina asili ya lugha ya Kiarabu na kuhitimisha kwamba, Kiswahili ni Kiarabu. Hata hivyo, tumeweza kuonesha kwa undani kwamba, sababu hiyo haina mashiko ya kitaaluma kuweza kuaminiwa na hivyo Kiswahili si Kiarabu bali ni lugha ya Waswahili wapatikanao katika upwa wa Pwani ya Afrika ya Mashariki. Baada ya kufafanua sababu kwamba Kiswahili ni Kiarabu kwa sababu hati za Kiarabu ndizo zilizotumika kueleza utamaduni wa lugha ya Kiswahili na kuikanusha ni vema sasa nitazame sababu nyingine. Nayo si nyingine bali ni ile isemayo: Kiswahili ni Kiarabu kwasababu kimekopa msamiati mwingi kutoka katika lugha ya Kiarabu. Yafuatayo ni maelezo ya kina kuhusiana na sababu hii.

5.3.4 Kiswahili Kimekopa Msamiati Mwingi Kutoka Kiarabu

Tafiti mbalimbali zilizotangulia kama ilivyooneshwa katika mapitio ya kazi tangulizi yanaonesha kwamba, Kiswahili kimekopa msamiati kutoka Kiarabu kwa asilimia 30, Kibantu asilimia 60 na lugha nyinginezo asilimia 10 (Massamba, 2002; Masebo na Nyangwine 2002). Katika utafiti huu inaonesha kwamba, Kiswahili kinadaiwa msamiati mkubwa na lugha ya Kiarabu, na siku msamiati huo ukirejeshwa

Kiswahili kinaweza kupwaya katika mawasiliano. Mfano ufuatao unaonesha maneno ya Kiswahili yenye asili ya Kiarabu. Khalid (2005) anaorodhesha msamiati kwa kichwa cha habari kisomekacho: *Maneno ya Kiarabu yaliyokopwa na Kiswahili*. Msamiati huo ni: *Hatari, safari, mahali, vitabu, msumari, kata, habari, huru, dhamiri, kamusi, baridi, rafiki, tafadhali* na *furahi*. Msamiati mwingine ni *asubuhi, dakika, saa, wakati, alasiri, magharibi, alfajiri, karne, alhamisi, ijumaa*. Msamiati mwingine ni *nusu, robo, sita, saba, tisa, ishirini, thelathini, arubaini, hamsini, sitini, sabini, thamanini, tisini, mia* na *elfu*.

Msamiati huu ni sehemu tu ya jumla ya maneno yaliyochukuliwa kutoka lugha ya Kiarabu na kutumiwa na lugha ya Kiswahili. Tunakubaliana na Khalidi (2005) kwamba msamiati huu umechukuliwa na kwamba haujakopwa. Kwa mujibu wa Sengo (2012 tarehe, 26 June) katika mazungumzo anaeleza kwamba:

Mawazo ya kwamba lugha ya Kiswahili imekopa msamiati mwingi kutoka Kiarabu au lugha yoyote ile si sahihi na kwamba ni mawazo ya Kikoloni. Lugha haikopi msamiati bali huchukuwa msamiati kutoka lugha nyingine na kuufanya kuwa ni wake na kisha kuutumia. Kitu cha kukopa hurudishwa kwa mwenyewe kwa kipindi maalumu kilichokubaliwa baina ya mkopeshaji na mkopaji. Kama hivyo ndivyo, Kiswahili kitarejesha lini msamiati kiliokopa kutoka Kiarabu na lugha nyinginezo?

Mawazo ya Sengo (2012 tarehe 26, June) hapo juu yana mchango mkubwa sana katika kusukuma mbele utafiti wetu. Ni dhahiri kwamba, lugha mbalimbali ulimwenguni huchukuwa msamiati kutoka lugha nyingine ili kukidhi mahitaji ya watumia lugha wake. Kuchukuwa maneno kutoka lugha nyingine hakuifanyi lugha hiyo kupoteza asili yake kama wanavyodai akina Harries (1962) na Knappert (1971). Lugha mbalimbali ikiwemo Kihausa kimechukua msamiati mwingi kutoka lugha ya

Kiarabu na kamwe haijatokea kuelezwa kwamba Kihausa asili yake ni Kiarabu. Si Kiarabu kwa sababu Kihiausa kilikuwepo hata kabla ya ujio wa Waarabu na kilichotokea ni kwamba Kihausa kilichukua msamiati wa Kiarabu ili kukidhi mahitaji ya wazungumzaji wake wakiwemo hao Waarabu waliokuwa wameingia katika ardhi ya Wahausa.

Kimsingi ni dhahiri kwamba kusema lugha fulani imekopa msamiati kutoka lugha nyingine si sahihi, vilevile kukopa huko kunaifanya lugha fulani kuwa na asili ya lugha iliyoikopesha msamiati pia si sahihi. Bali lugha huchukua msamiati na kuutumia katika mawasiliano ya watumiaji wake. Kudai kwamba, Kiswahili ni Kiarabu kwa sababu kimekopa msamiati kutoka lugha ya Kiarabu na kwa kukopa huko kimeathiriwa sana si sababu sahihi kwa kuwa Kiswahili hakikuathiriwa na Kiarabu bali ni kawaida ya lugha kuchukua msamiati kutoka lugha nyingine na kuutumia katika mawasiliano ya wazungumzaji wake. Baada ya kuzungumzia sababu hii ni vema sasa niangalie suala la lafudhi ya matamshi ya lugha ya Kiswahili.

5.3.5 Lafudhi ya Matamshi ya Kiswahili

Mufwene (2007) anaeleza kwamba, lugha ya Kiswahili inaonekana kuwa na lafudhi ya msamiati wa lugha ya Kiarabu kwa kiasi kikubwa. Kwa msingi huu ni wazi kwamba, Kiswahili ni Kiarabu na hii ina thibitishwa na athari ya matamshi ya Kiswahili kusikika kama Kiarabu pale Mswahili azungumzapo. Mawazo ya kwamba, Kiswahili kina msamiati wenye lafudhi ya Kiarabu halipingiki hata kidogo ninakubaliana nalo kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, sikubaliani na madai

kwamba, lafudhi hiyo inaifanya lugha ya Kiswahili kuwa ni Kiarabu. Nilifanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Unguja ambaye nilimnukuu akisema:

Waswahili tumekuwa na lafudhi kama ya Kiarabu tutamkapo msamiati wa lugha ya Kiswahili hasa ule uhusikanao na masuala ya Ibada za dini ya Kiislamu kama vile, sala, rakaa, hijjah, saumu, Ramadhani, dua, zakka na kadhalika. Waswahili na Waafrika kwa ujumla ni watu tunaoheshimu sana masala ya dini na hivyo tunafika mahali kwamba, tunaamini kuwa, ili ibada zetu zipokelewe na Mwenyezi Mungu ni lazima tufanye maombi yetu kwa kutumia lafudhi ya lugha ya yule aliyetuletea mafundisho ya dini husika.

Maelezo ya mtafitiwa huyu yanasukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, yametaja baadhi ya maneno/msamiati unaotamkwa kwa lafudhi ya Kiarabu. Msamiati wote uliotajwa na mtafitiwa una asili ya Kiarabu hivyo haishangazi kuona Mswahili kuutamka msamiati huo kwa lafudhi ya lugha ya Kiarabu. Pia maelezo haya yanaonesha kwamba, Mswahili huyatamka kwa lafudhi ya Kiarabu ili Mwenyezi Mungu ampokelee maombi yake kwani kutamka msamiati huo kwa lafudhi isiyo yake Mwenyezi Mungu hatoelewa anaomba nini na hivyo kutompatia kile alichokiomba. Kama hivi ndivyo, si sahihi kudai kwamba, Kiswahili kimeadhiriwa sana na Kiarabu ndiyo maana hata lafudhi ya maneno yake ni ya Kiarabu. Jambo hili ni la kawaida mno na hufanyika hata makanisani pale Padri anapoendesha Misa kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa lafudhi ya Kilatini. Hata hivyo, haikuwahi kusemwa kwamba, Kiswahili kimeathirika sana na Kilatini kwa sababu lafudhi ya Kilatini inatumika kutamka msamiati wa lugha ya Kiswahili kanisani.

Vile vile, baadhi ya Waswahili walipenda kutamka msamiati wa Kiswahili kwa lafudhi ya Kiarabu kwa sababu ilikuwa ni lugha ya bwana na mtwana daima hupenda

kumuiga bwana wake katika kila jambo akiamini kwamba, kwa kufanya hivyo, anamridhisha bwana wake. Pia hafanyi hivyo kwa minajili ya kumridhisha bwana wake tu bali anaamini kwamba, kila afanyacho bwana wake ndicho bora na anapaswa kukiiga na kufanya kama afanyavyo bwana wake. Kwa minajili hiyo basi, ni makosa makubwa kutoa hitimishi kwamba Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu na hivyo, Kiswahili ni Kiarabu kwani kama Kiswahili ndicho kingekuwa ni lugha ya mabwana enzi hizo za utawala wa Waarabu ni dhahiri Kiswahili kingekuwa kimetoa msamiati pamoja na lafudhi yake kwa lugha ya Kiarabu. Lafudhi ya lugha moja kusikika kutumika katika lugha nyingine si sababu ya msingi kumfanya mwanataalimu wa lugha kuhitimisha kwamba, lugha iliyochukuwa lafudhi ya lugha nyingine basi asili yake inatokana na hiyo lugha lafudhi yake iliyochukuliwa. Baada ya maelezo haya sasa nizungumzie ushairi wa Kiswahili kuwa asili yake ni Uislamu na Uarabu.

5.3.6 Ushairi wa Kiswahili Asili yake ni Uislamu na Uarabu

Mawazo kuhusu asili ya ushairi wa Kiswahili kuwa ni Uislamu na Uarabu yamekuzwa sana na Harris (1962) na Knappert (1982). Wanataalimu hawa wanadai kwamba; ushairi wa Kiswahili unaeleza maudhui ya dini ya Kiislamu, unatumia istilahi za lugha ya Kiarabu, una mianzo na miisho ya kuanza na dua na kumaliza na dua na kadhalika vitu ambavyo huupa ushairi wa Kiswahili sura ya Uislamu na fasihi ya Kiarabu. Tujuavyo sisi ni kwamba, ushairi tena simulizi ndiyo utanzu wa kwanza kutendwa na mwanadamu katika fasihi duniani ikiwemo ile ya Kiswahili. Kwa mawazo ya Harris (1962) na Knappert (1982) ni sawa na kusema kwamba, Waswahili walianza kutumia utanzu wa ushairi pale Waarabu walipoingia Afrika ya

Mashariki kwa mara ya kwanza katika karne ya 7. Kabla ya hapo hawakuwa na ushairi wa wao. Mawazo haya yanapingana na yale ya Mulokozi (2000) kuwa, fasihi simulizi ilianza pale tu binadamu alipogundua lugha na kuanza kuwasiliana na wenzake.

Mawazo ya Mulokozi (2000) hapo juu naungana nayo mkono na kwa kuwa yanasukuma mbele utafiti huu. Waswahili kama walivyo watu mbalimbali duniani walitumia lugha yao ya Kiswahili kuimba na kughani mashairi simulizi wakieleza utamaduni, historia, fikra na mawazo yao juu ya vitu mbalimbali vihusavyo maisha yao ya kila siku. Kueleza kwamba, ushairi wa Kiswahili asili yake ni Uislamu na Uarabu si jambo sahihi kwani kuelezwa kwa utamaduni wa Kiislamu katika ushairi wa Kiswahili ni njia ya kuonesha kwamba, jamii ya Waswahili na Waarabu zilikutana na kuishi pamoja kwa muda mrefu kiasi cha kuathiriana kimila, desturi na taratibu mbalimbali za maisha ya jamii. Hata hivyo, Mulokozi (2000) anaeleza kwamba:

Swahili poetry can be identified not so much by its formal aspects but rather by its historical determinants, the language medium, and the cultural and social values that it expressed. It is these and not the “Vina” and “Mizani” which differentiate Swahili Poetry from other world Poetries.

Ushairi wa Kiswahili haufahamiki sana kutokana na mundo wake bali kwa historia yake lugha yake pamoja na mila, desturi na utamaduni inaoueleza. Ni mambo haya na siyo “Vina” na Mizani” ndivyo hutofautisha ushairi wa Kiswahili na ushairi mwingine duniani (Tafsiri yangu).

Maelezo ya Mulokozi (2000) hapo juu yanaonesha kwamba, ushairi wa Kiswahili ulikuwepo tangu enzi kabla ya ujio wa Waarabu na ulitumiwa na Waswahili katika kueleza na kuhifadhi mila na desturi za jamii husika. Kulihusisha suala la vina na

mizani na asili ya ushairi wa Kiswahili na kisha asili Ya lugha ya Kiswahili ni makosa makubwa sana. Ushairi wa Kiswahili ulikuwepo tangu kale na vina vilikuja na ujio wa Waarabu katika pwani ya Afrika Mashariki. Hivyo ni sawa na kusema kwamba, lugha ya Kiswahili ilikuwepo na ilikuwa inatumika kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa jamii ya Waswahili tangu kale kabla ya ujio wa Waarabu.

Madai kwamba, ushairi wa Kiswahili unaeleza maudhui ya dini ya Kiislamu na utamaduni wa Waarabu na hivyo kuufanya ushairi wa Kiswahili kuwa na asili ya Uarabuni si sahihi. Knappert (1982) na Harris (1962) wanataja ushairi wa *Mwanakupona* kuwa umesheheni maudhui ya dini ya Kiislamu pale “Mwanakupona” anapomtaka binti yake kumheshimu Mume wake kwa kumwandalia kila kitu anachotaka na asitoke nyumbani bila ruhusa ya mume wake. Nilifanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Pemba ambaye alinieleza kama ifuatavyo:

Kwa maoni yangu, sidhani kwamba suala la kumheshimu mume ni suala la dini ya Kiislamu na Uarabu peke yake bali ni la jamii mbalimbali duniani. Jamii ya Waafrika imekuwa hata kabla ya ujio wa wageni (Waarabu) ikimtaka mke na mume wote kuheshimiana kama njia ya kuonesha ustaarabu wao na utu wa kibinadamu. Hata hivyo, sishangai kusikia hivyo kwa sababu Uislamu ndiyo mfumo wa maisha yetu. Kama ni mfumo wa maisha basi haina shaka utasawiriwa katika fani mbalimbali za kifasihi ukiwemo ushairi. Hata hivyo, hii haimaanishi kwamba, ushairi wa Kiswahili maudhui yake yote ni dini ya Kiislamu na fasihi ya Kiarabu. Asili ya Ushairi wa Kiswahili ni Waswahili wenyewe na lugha yao ya Kiswahili.

Maelezo haya yanaonesha kwamba, Mswahili alitumia ushairi kudumisha utu wa mwanadamu hata kabla ya ujio wa wageni. Vile vile suala la mke na mume kuheshimiana ni jambo lililokuwepo tangu kale katika jamii mbalimbali duniani, na si ile ya Waarabu peke yake. Kwa msingi huu basi, ninaweza kueleza kwamba,

ushairi wa Kiswahili una asili na historia yake katika upwa wa Pwani ya Afrika Mashariki na si dini ya Kiislamu na Uarabu kama wanavyodai wanataalimu tuliowataja hapo awali.

5.3.7 Hitimishi

Katika sehemu hii tumeeleza sababu mbalimbali zilizowasukuma wanataalimu kadhaa kutoa hitimishi kwamba asili ya lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kiarabu. Sababu hizo ni pamoja na watafiti na waandishi wa mwanzo wa lugha ya Kiswahili kuwa ni wageni, kufundishwa lugha ya Kiarabu katika madrasa, Kiswahili kukopa msamiati mwingi kutoka lugha ya Kiarabu, lafudhi ya matamshi ya msamiati wa Kiswahili kuwa na lafudhi ya Kiarabu na asili ya Ushairi wa Kiswahili ni dini ya Kiislamu na fasihi ya Kiarabu. Athari hizi kwa hakika zimefafanuliwa na kuonesha kwamba, lugha ya Kiswahili inabaki kuwa lugha yenye asili yake katika upwa wa Pwani ya Afrika Mashariki.

Suala la lugha kuathiriwa bila lugha athiriwa nayo kiathiri hiyo nyingine si la kweli ila linawezekana kwa maneno tu hasa pale lugha moja inapochukuliwa kama lugha ya watwana na nyingine ya mabwana. Ile ya watwana inakandamizwa na kuonekana si lolote si chochote mbele ya ile ya mabwana. Hivi ndivyo namna Kiswahili kilivyoshushwa hadhi yake mbele ya Kiarabu. Hata hivyo, kwa kuwa Waarabu walikuwa wachache ukilinganisha na Waswahili bado Kiswahili kilibaki kuwa lugha ya matumizi mapana na Waarabu waliobaki katika eneo la Afrika Mashariki wamekuwa Waswahili na hawawezi tena kuzungumza Kiarabu. Maelezo zaidi kuhusu hali hii yameelezwa katika sehemu inayofuata.

5.4 Athari ya Lugha ya Matumizi Mapana (Kiswahili) kwa Waarabu Waishio katika Pwani ya Afrika Mashariki

5.4.1 Utangulizi

Katika sehemu hii tunaonesha athari ya lugha ya matumizi mapana yaani Kiswahili kwa Waarabu waliobaki na kufanya maisha yao katika upwa wa Pwani ya Afrika Mashariki. Kiswahili kama tulivyoona katika sehemu iliyopita kilifanywa kuwa lugha ya watwana na Kiarabu kuwa ndiyo lugha ya mabwana. Hata hivyo, baada ya utawala wa Sultani kuondolewa katika Pwani ya Afrika Mashariki wapo Waarabu waliobaki na kutumia Kiswahili kama lugha ya matumizi mapana. Hivyo basi, ni namna gani lugha hii ya matumizi mapana imewaathiri Waarabu na lugha yao ya Kiarabu katika upwa wa Pwani ya Afrika Mashariki ni jambo linalojadiliwa na kuwasilishwa katika sehemu hii.

5.4.2 Athari za Kidini

Waswahili kama ilivyo kwa Waafrika kwa ujumla walikuwa na dini zao na kuabudu katika mapango na chini ya mti mikubwa. Waandishi Penina Muhando na Ebrahimu Hussein wamesawiri katika tamthiliya zao namna Waswahili walivyokuwa wakiabudu miungu yao kabla ya ujio wa wageni na kwamba, mpaka leo wapo Waswahili wanaoendelea kutekeleza ibada hizo kupitia matambiko mbalimbali (Sengo 2012 katika mazungumzo). Ujio wa Waarabu katika karne ya 7 katika Pwani ya Afrika kwa minajili ya kufanya biashara kulileta dini ya Kiislamu. Tafauti na dini za Kiafrika, Uislamu unafunza kwamba, Mwenyenzi Mungu ni mmoja tu na ndiye anayepaswa kuabudiwa kwa haki na kuabudu miungu ya Kiafrika ni shiriki ambayo ni dhambi kubwa kupata kufanywa na mwanadamu. Hivyo, Waswahili ili

wasiendeleo kumshirikisha Mwenyezi Mungu na viumbe wake walipaswa kusilimu. Baada ya kusilimu wanapaswa kutekeleza ibada mbalimbali ikiwemo kuswali swala tano kwa siku pamoja na swala ya Ijumaa ambayo huwakutanisha Waislamu wengi kwa pamoja.

Kama ilivyo ada, swala ya Ijumaa hutanguliwa na hutuba ambayo ni mawaidha ya kuasa na kuionya jamii juu ya makatazo ya Mwenyezi Mungu na kutekeleza maamrishi yake. Waarabu kwa kuonesha kwamba, lugha yao ni bora kuliko lugha nyingine wakadai kwamba, hotuba ni lazima isomwe kwa Kiarabu ndiyo itakubalika mbele ya Mwenyezi Mungu. Hata hivyo, kwa kuwa Kiswahili ndicho kilikuwa lugha ya matumizi mapana ikalazimika kwamba, hotuba isomwe kwa Kiarabu halafu ifanyiwe tafsiri kwa Kiswahili ili waumini waweze kuelewa ni nini kinachozungumzwa katika hotuba ya Ijumaa. Nilifanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Unguja ambaye alinieleza kwamba:

Tunapoenda kusali swala ya Ijumaa tunasomewa hotuba ya Ijumaa na Khatibu ambaye hutumia lugha zote mbili yaani Kiarabu na Kiswahili. Atasoma aya fulani katika Qur'an halafu ataeleza kuelewa anasema nini. Mwanzo tu Waarabu walisisitiza sana matumizi ya Kiarabu kuliko Kiswahili lakini leo tunatumia lugha zote mbili huku Kiswahili kikichukua nafasi kubwa kuliko Kiarabu.

Maelezo haya yanaonesha kwamba, lugha ya matumizi mapana ambayo ni Kiswahili zimelazimisha ibada nazo ziiitambue lugha hii na kuipa nafasi ya kutumika sambamba na lugha ya Kiarabu. Kwa ilivyo sasa hivi ni kwamba, hotuba nzima inasomwa kwa Kiswahili huku nguzo za hotuba ndizo zisomwazo kwa Kiarabu.

Vile vile, mafundisho ya dini ya Kiislamu yanapinga utamaduni wa ngoma na nyimbo za Waswahili kwa madai kwamba, ni mambo ya kijahili na kishetani

yasiyopendwa na Mwenyezi Mungu. Itakumbukwa kwamba, Waswahili kama zilivyo jamii mbalimbali duniani wana mila na desturi zao ambazo wamekuwa wakizifuata kwa miongo mingi katika maisha yao. Ujio wa Waarabu na dini ya Kiislamu ukawataka kuachana na mila na desturi hizo. Baadhi ya wanajamii wamejitahidi sana kuachana na baadhi ya mila hizo ikiwemo ngoma, nyimbo na matambiko lakini wakashindwa na kujikuta wanaendelea kutekeleza mila hizo. Kutokana na Kiswahili kuwa ndiyo lugha ya matumizi mapana Waarabu nao wamejikuta wakicheza ngoma na nyimbo za Kiswahili ambazo hapo awali walizikataa. Waliokataa si wao bali mababu zao ila wao wamevutwa na nguvu ya lugha ya matumizi mapana. Nilifanya mahojiano na mtafitiwa kutoka Pemba ambaye alinieleza kwamba:

Tunapohudhuria katika sherehe mbalimbali za jamii ya Kiarabu kama vile ndoa/harusi tunaona nyimbo na ngoma zinazotawala ni zile za Waswahili. Ule Uarabu haupo tena kama kipindi cha utawala wa Sultani. Waarabu hawa hawajui tena kuzungumza Kiarabu wanazungumza Kiswahili tu na hata leo wakienda Uarabuni wao ni wageni na wanapata shida sana katika kuwasiliana na wenzao. Ninakueleza haya kwa kuwa ninaye rafiki yangu mmoja wa Kiarabu aliyenieleza haya. Kama hio haitoshi mimi mwenyewe nimesoma na Waarabu shuleni na kwa hakika hawajui Kiarabu wanajua Kiswahili.

Maelezo haya yanaonesha namna lugha ya matumizi mapana ilivyo na nafasi kubwa ya kuathiri wazungumzaji wa lugha nyingine katika jamii. Lugha ambayo ilionekana kuwa ni ya tabaka la watu wa juu leo haizungumzwi kwa upana uliotegemewa na badala yake lugha iliyodharauliwa leo ndiyo inayotumiwa na hata wale waliodharau. Utamaduni wa Waswahili kama vile ngoma na nyimbo ndio vitu vilivyotawala katika visiwa vya Pemba na Unguja na kufanywa na Waarabu kwa furaha na shangwe kubwa sana. Hali hii imewafanya Waarabu na Waswahili kuwa na Muungano mkubwa baina yao. Kwa mfano: katika mji wa Chakechake kuna

msikiti wa dhehebu la Ibadhi ambao unaswaliwa na Waswahili na Waarabu. Hii haikuwa rahisi katika kipindi cha utawala wa sultani. Imewezekana kuwa hivi kwa sasa kutokana na kuunganishwa na lugha ya matumizi mapana ambayo ni Kiswahili (Mhojiwa, Pemba). Baada ya kueleza namna lugha ya matumizi mapana ilivyochangia kuathiri dini ya Kiislamu ya Waarabu na kuwa ya Kiswahili kwa maana ya namna ibada zake zinavyoendelehwa tuzame sasa katika kipengele cha utamaduni ambacho nilikigusia hapo awali.

5.4.3 Athari za Kiutamaduni

Utamaduni ni kipengele kipana sana na hata dini ambayo nimeieleza hapo awali ni sehemu ya utamaduni. Hata hivyo, kwa minajili ya utafiti huu nimeaua kuvitenganisha ili niweze kukamilisha lengo kuu la utafiti huu. Katika kipengele hiki nitazungumzia suala la malezi ya watoto. Kiswahili ambacho ndiyo lugha pana ya matumizi katika ukanda wa Afrika Mashariki imeathiri wazungumzaji wa lugha ya Kiarabu katika kipengele cha malezi ya watoto. Waarabu wa Pemba na Unguja wanawalea watoto wao kama Waswahili kwa kuwafunza kuongea Kiswahili na kuwa wamilisi kama walivyo Waswahili. Nilipofanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Unguja alinieleza kwamba:

Waarabu hufanya shughuli za malezi ya watoto kama ilivyo kwa Waswahili. Kwanza wao wenyewe (wazazi) wanaongea Kiswahili na kisha watoto nao kujifunza lugha hiyohiyo wazungumzayo wazazi wao. Vile vile, aina ya mavazi wanayowavalisha watoto wao na wanayovaa wao ni yaleyale ya Waswahili na si ya Kiarabu. Pia shule wanazowapeleka watoto wao ni zile zile wanazosoma Waswahili na hivyo kujifunza maadili ya Waswahili. Si hivyo tu, bali pia watoto wao wanaoa na kuolewa na Waswahili na kadhalika.

Mawazo katika dondoo hapo juu yanasukuma mbele utafiti wangu kwa namna mbalimbali. Kwanza suala la Waarabu kuwafunza watoto wao kusema lugha ya Kiswahili ni athari ya lugha ya matumizi mapana kwa lugha ya Kiarabu na wazungumzaji wake ambao ni Waarabu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, wazazi hawa wametambua kwamba iwapo watoto wao hawatajifunza lugha ya Kiswahili itawawia vigumu kuwasiliana na Waswahili ambao nao Waarabu ni sehemu ya jamii lugha hiyo.

Si hivyo tu bali pia matumizi ya lugha pana na utamaduni wake vimewafanya Waarabu kuvaa mavazi ya Waswahili kwa kiasi kikubwa hata katika nyumba za Ibada hali ambayo haikutegemewa kutokea katika enzi za utawala wa Sultani. Mavazi yao makubwa ni shati na suruali kama wawaavyo Waswahili. Nguvu ya matumizi ya lugha pana imewafanya Waarabu kujinasibisha na Waswahili ili wasionekane kama watu baki yaani si miongoni mwa Waswahili. Kwa mujibu wa mtafitiwa mmoja kutoka Unguja anaeleza kwamba kuna Mwarabu mmoja aliyekuja Zanzibar mwaka 1938 na kuamua kujenga nyumba yake katikati ya Waswahili hali ya kuwa alikuwa na uwezo wa kujenga nyumba hiyo katika maeneo walioishi Waarabu. Mzee huyu ni Mswahili kwa kila kitu, yeye pamoja na watoto wake. Hii inatokana na ukweli kwamba, lugha aliyokuwa akizungumza pale ni Kiswahili, mavazi aliyokuwa akivaa ni ya Kiswahili na kwa watoto wake ikawa ni hivyo hivyo.

Suala jingine linalojitokeza katika dondoo hapo juu ni suala la Waarabu na Waswahili kuoana. Itakumbukwa kwamba, katika kipindi cha utawala wa Sultani ni Waarabu tu ndiyo waliokuwa wakioa Waswahili na Waswahili hawakuruhusiwa

kuoa Mwarabu. Kutokana na matumizi ya lugha pana yaani Kiswahili, Waarabu wamevutwa na kubadili mila hiyo na sasa wanaolewa na Waswahili. Hii imekuja kwa sababu wote wanazungumza Kiswahili, kisha wanafahamiana na kueleana vizuri tofauti na kipindi ambacho Waarabu walikuwa wanazungumza Kiarabu na Waswahili wakizungumza Kiswahili na hata shule kila jamii ilikuwa na shule zake. Kwa ujumla, ninaweza kusema kuwa, hiki kilikuwa ni kipindi cha ubaguzi na ukandamizaji.

Mambo haya ya ubaguzi na ukandamizaji bado yanasikika katika nchi za Kiarabu lakini si Afrika ya Mashariki kwa nini? Matumizi ya lugha pana yaani Kiswahili ndiyo yaliyosaidia kuondoa hali hiyo. Baada ya kutoa maelezo ya namna lugha ya matumizi mapana– Kiswahili kilivyoathiri utamaduni wa Waarabu na kuwaingiza katika utamaduni wa Waswahili ni vema sasa tuzungumzie kipengele cha siasa na utawala.

5.4.4 Athari za Kisiasa na Utawala

Lugha ya matumizi mapana yaani Kiswahili kimeathiri sana matumizi ya lugha katika masuala ya kisiasa na utawala katika visiwa vya Unguja na Pemba. Lugha ya Kiarabu ndiyo iliyokuwa lugha kuu ya utawala kipindi cha Sultani na Kiswahili nacho kilitumika lakini hakikupewa hadhi kama ilivyokuwa kwa Kiarabu. Baada ya utawala wa Waarabu kumalizika lugha ya Kiswahili ikawa ndiyo lugha rasmi ya kisiasa na utawala katika visiwa vya Pemba na Unguja. Siasa za Unguja na Pemba ni hai na maarufu sana duniani, umaarufu wake unatokana na upinzani mkali uliopo baina ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Wananchi (CUF). Katika

kipindi cha uchaguzi kila chama husimamisha mgombea uraisi na ubunge katika majimbo yote ya uchaguzi.

Wagombea wengi katika chaguzi hizo ni Waswahili wenye asili ya Kiafrika na wachache ni Waswahili wenye asili ya Kiarabu. Lugha kuu inayotumika katika Kampeni za Uchaguzi ni Kiswahili kwa wagombea wote bila kujali rangi zao.

Nilifanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Unguja ambaye alinieleza kwamba;

Waswahili wenye asili ya Kiarabu wanaogombea nafasi mbalimbali za uongozi wa Kisiasa wanatumia lugha ya Kiswahili katika kampeni za kuomba kura kwa wananchi. Ni jambo ambalo halikutegemewa kutokea katika kipindi cha utawala wa Kisultani katika visiwa vya Pemba na Unguja. Kiswahili wanachotumia ni kile cha kawaida kabisa kisicho na tofauti na Kiswahili waongeacho Waswahili wenye asili ya Kiafrika.

Maelezo haya yanaonesha namna lugha ya matumizi mapana inavyoweza kumiliki mawasiliano ya jamii na kuathiri lugha nyingine kutotumika hata kama zilikuwa na nguvu kubwa katika kipindi cha nyuma. Vile vile, lugha ya matumizi mapana inawafanya wanajamii kuungana na kuwa kitu kimoja na kusahau tofauti zao. Kwa mfano, Mswahili mwenye asili ya Uarabu kisha anapewa kura na Waswahili wenye asili ya Kiafrika na kushinda uchaguzi. Baada ya kushinda uchaguzi huwaongoza wananchi wote katika kipindi chake chote cha uongozi. Mswahili Mwafrika alibaguliwa na kunyimwa nafasi za juu za uongozi wa nchi. Lakini Mswahili huyo huyo anampatia uongozi Mswahili Mwarabu. Hii yote kwa hakika inatokana na lugha ya matumizi mapana yaani lugha ya Kiswahili kuwaunganisha na kujiona kama kitu kimoja.

Vile vile katika kuonesha nguvu ya matumizi ya lugha pana katika jamii, dondoo hapo juu linaeleza kwamba, Kiswahili kinachozungumzwa na Waswahili Waarabu katika kampeni za kisiasa ni Kiswahili cha kawaida sawa na kile wanachozungumza Waswahili Waafrika. Hii inaonesha namna Waswahili Waarabu walivyolazimika kujifunza lugha ya Kiswahili mpaka kuimudu na kuzungumza kama Waswahili wenyewe halisi ingawa huko nyuma Kiswahili kilionekana ni lugha ya tabaka la chini katika jamii.

Baada ya kuona namna lugha ya matumizi mapana yaani Kiswahili kilivyoweza kuwaathiri wazungumza lugha ya Kiarabu katika tasnia ya masuala ya kisiasa ni vema sasa tutazame kipengele cha kiuchumi.

5.4.5 Athari za Kiuchumi

Tunapozungumza juu ya masuala ya kiuchumi tuna maana ya jumla ya shughuli zote zifanywazo na mwanadamu kwa lengo la kumingizia kipato cha kuendeshea maisha yake ya kila siku. Lugha ya matumizi mapana ina mchango mkubwa sana katika kufanikisha shughuli za kiuchumi katika jamii husika. Jamii ya Waswahili wenye asili ya Kiarabu wameathiriwa na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika utendaji wao wa shughuli zao za kiuchumi. Nilifanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Pemba ambaye alinieleza kuwa:

Waswahili wenye asili ya Kiarabu wanamiliki mashamba huku utendaji wao wa kazi ukiwa ni ule wa utamaduni wa Mswahili Mwafrika. Kwa mfano, utawasikia wakisema misemo na methali mbalimbali kama vile *asiyelima na asile, mvumilivu hula mbivu, haba na haba hujaza kibaba* na kadhalika. Vile vile wanatumia wanyama kazi kama vile punda kama atumiwavyo na Mswahili Mwafrika. Pia wanashughulika na shughuli za ufuaji na ukwezi pamoja na usasi na uwindaji.

Shughuli hizo zote hufanywa sambamba na nyimbo na misemo na methali za lugha ya Kiswahili.

Maelezo katika dondoo hapo juu yanaonesha namna lugha ya matumizi mapana ilivyo na mchango mkubwa sana katika kuwaathiri wazungumzaji wa lugha tofauti tofauti katika jamii na kisha kujikuta nao wameimarika katika kutumia lugha hiyo katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Mswahili mwenye asili ya Kiafrika tangu kale alikuwa akitumia misemo na nyimbo mbalimbali katika utendaji kazi ili kuchapusha kazi yake. Itakumbukwa kwamba, enzi hizo hapakuwa na teknolojia iliyopo leo na nguvu kazi ya mwanadamu ndiyo iliyohitajika zaidi katika kufanikisha shughuli mbalimbali za kiuchumi. Hata hivyo, jamii ya Waarabu waishio katika visiwa vya Pemba na Unguja nao wameathiriwa na matumizi ya lugha pana – Kiswahili na kutenda shughuli mbalimbali za kiuchumi kama atendavyo Mswahili Mwafrika.

Vile vile, tunafahamu kwamba, Waarabu kwa kawaida ni wakulima wa tende na uchimbaji wa mafuta na ngamia ndiyo mnyama kazi muhimu katika kufanikisha shughuli za kila siku kama usafirishaji wa mizigo na kadhalika. Hata hivyo, leo kama inavyoonekana katika dondoo hapo juu wanajishughulisha na ufuaji na ukwezi wa nazi pamoja na usasi na punda akiwa ndiyo mnyama kazi muhimu katika kusukuma mbele shughuli hizi. Mambo haya kwa hakika ni ya utamaduni wa Mswahili ambayo leo yanafanywa na Mwarabu. Hii bila shaka inadhihirisha nguvu ya matumizi ya lugha ya matumizi mapana yaani Kiswahili katika jamii pale ambapo shughuli zote hizi hufanyika sambamba na misemo, methali na nyimbo za Kiswahili.

Si hivyo tu, bali pia mtafiti alifanya mahojiano na mtafitiwa mmoja kutoka Unguja na kuelezwa kwamba:

Waarabu hutumia mbinu za kukwepa kodi kwa njia ya biashara za magendo kama wafanyavyo Waswahili. Vitendo hivyo huambatana na misemo, nahau na methali za lugha ya Kiswahili. Kwa mfano utasikia wanasema: *chelewachelewa ukute mwana si wako* kwa maana ya kuwa usipokuwa makini unaweza kukamatwa na usiambulie kitu na kisha ukarudi nyumbani mikono mitupu.

Maelezo haya ni mwendelezo tu unaoonesha namna lugha ya matumizi mapana-Kiswahili ilivyokuwa na nguvu ya kuathiri wazungumzaji wa lugha nyingine ambapo huacha kutumia lugha yao na kutumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zao za kila siku za kiuchumi.

5.4.6 Hitimishi

Katika sehemu hii tumeonesha athari ya lugha ya matumizi mapana (Kiswahili) kwa Waarabu waishio katika visiwa vya Pemba na Unguja. Athari hizo zinajibainisha katika vipengele vya kiutamaduni, kidini, kisiasa na kiuchumi. Vipengele hivi vimedhihirisha kwamba, lugha ya matumizi mapana (Kiswahili) imewaathiri Waarabu waishio Pemba na Unguja na kujikuta wanazungumza lugha ya Kiswahili na si Kiarabu lugha ya mababa na babu zao. Waarabu hawa ambao sasa ni Waswahili hushiriki katika shughuli mbalimbali za vipengele tajwa hapo juu kwa kutumia lugha ya Kiswahili ambapo misemo, nahau, methali na nyimbo mbalimbali hutumika kusherehesha na kulainisha shughuli husika. Kwa msingi huu basi, ninaweza kusema kwamba, lugha ni chombo cha mawasiliano na hakuna lugha iliyokuwa bora kuliko lugha nyingine. Ninayasema haya kwa sababu, kipindi cha utawala wa Sultani, Kiarabu kilionekana kuwa ndiyo lugha bora na Kiswahili ni lugha duni. Iweje leo,

Waarabu hawa waishio Pemba na Unguja hawajui tena kuzungumza Kiarabu na badala yake wanazungumza Kiswahili? Jibu la swali hili ni rahisi tu! Kwamba siku zote mtawala – bwana hujikweza na kutaka kuonekana na kujulikana kwamba kila kitu chake ni bora kuliko cha watawaliwa. Ikiwa hivyo ndivyo, watawaliwa watamuheshimu sana, watamuogopa na kumtii kwa kila awaagizalo hata kama lina madhara kwao. Baada ya kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu athari za matumizi ya lugha pana (Kiswahili) kwa jamii ya Waarabu waishio Pemba na Unguja ni vema sasa nitazame maendeleo ya lugha ya Kiswahili katika karne ya ishirini na moja.

5.5 Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili Katika Karne ya Ishirini na Moja na Changamoto Zake

5.5.1 Utangulizi

Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa duniani zilizopata maendeleo makubwa tangu kuanza kwake mpaka leo katika karne ya ishirini na moja. Maendeleo ya lugha ya Kiswahili yanajibainisha katika nyanja mbalimbali kama vile; elimu, habari, matumizi katika mikutano ya Kimataifa na midahalo, muziki na kadhalika. Tumeamua kuzungumzia maendeleo ya lugha ya Kiswahili ili kuonesha nafasi yake halisi katika ulimwengu nafasi ambayo isingeweza kuwepo kama Kiswahili kingekuwa ni lugha ya vizalia ama asili yake ni Uarabuni. Kisha tumezungumza kuhusu changamoto zinazokabili maendeleo ya lugha ya Kiswahili duniani. Tunaanza na nafasi ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika tasnia ya Elimu.

5.5.2 Kiswahili katika Elimu

Kiswahili kama lugha ya matumizi mapana ni lugha adhimu inayotumika sana katika tasnia ya elimu duniani kote. Nchini Tanzania ambako ndio chimbuko la lugha hii ya Kiswahili kinatumika kufundishia elimu ya msingi na kufundishwa kama somo katika ngazi ya elimu ya sekondari na elimu ya juu. Kutokana na matumizi hayo Kiswahili kimeweza kukuza msamiati wake kwa kiasi kikubwa sana. Kutokana na utajiri wake wa msamiati, Kiswahili kinatumika sio tu katika elimu ya Tanzania bali pia nchi mbalimbali duniani. Mhochi na Wairuru (2004) wanasema:

Swahili has developed to become a very popular African language, taught in many leading academic institutions in Africa, Europe American and Asia. It is offered as subject of study in prestigious Universities like Havard, Yale, Stanford Priceton, the University of Penislavenia and others. It is estimated that, close to 100 institutions teach Swahili at the US alone, Swahili has been taught in SOAS at the Universituy of London since the 1930s. It is also taught in Canada, Germany, Poland, Mexico, Russia Japan, India and many others countries.

Kiswahili kimeendelea sana kiasi cha kuwa lugha maarufu duniani ya Kiafrika inayofundishwa katika vyuo vikuu huko Marekani, Ulaya, Asia na Afrika. Kiswahili kinafundishwa kama somo katika vyuo vikuu vya Kifahari kama vile Havard, Yale, Stanford, Princeton, Penislavenia na vinginevyo. Inakadiriwa kwamba, zaidi ya vyuo 100 huko Marekani vinafundisha somo la Kiswahili. Taasisi ya SOAS ya Chuo Kikuu cha London imekuwa ikifundisha Kiswahili tangu mwaka 1930. Pia kinafundishwa Canada, Ujerumani, Poland, Mexico, Russia, Japan, India na nchi nyingine nyingi (Tafsiri yangu).

Dondoo hili linaonesha namna lugha ya Kiswahili kama lugha ya matumizi mapana ilivyovuka mipaka na kutumika hata katika nchi za nje, tena kimataifa. Nilifanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Dar es Salaam kuhusu sababu zilizofanya Kiswahili kiweze kupiga hatua hii muhimu katika maendeleo yake. Mtafitiwa huyu alinieleza kwamba, “lugha ya Kiswahili ni lugha rahisi sana kueleweka na

inapendwa sana na wageni kutokana na sababu hiyo pale wanapojifunza Kiswahili wanaelewa haraka kuliko lugha nyingine yeyote ile duniani”. Kimsingi, ninaungana mkono na mawazo ya mhojiwa kwamba Kiswahili ni lugha rahisi sana kueleweka kwa wale wajifunzao lugha hiyo.

Vilevile, lugha ya Kiswahili ni lugha inayozungumzwa na Waafrika walio wengi katika nchi za Tanzania Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda, Zambia, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kwa msingi huo, mataifa ya Ulaya huona kuwa kwa kumfundisha mwananchi wake Kiswahili kutamwezesha kufanya mawasiliano na jamii izungumzayo lugha ya Kiswahili ambayo ni pana kabisa. Itakumbukwa kwamba, mataifa ya kibepari yana ari kubwa ya kuwekeza katika sekta mbalimbali hapa nchini na hivyo kuhitajika kufanya tafiti mbalimbali. Watafiti hao wanapokuwa wanafahamu lugha ya Kiswahili inakuwa ni bora zaidi kiasi cha kuwawezesha kufanikisha tafiti zao kwa ukamilifu na kuwezesha uwekezaji kuwa wa tija zaidi. Sababu hizi pamoja na nyingine ndizo zilizokifanya Kiswahili kuwa lugha ya Kiafrika inayofunzwa katika vyuo mbalimbali duniani kama nilivyokwisha onesha. Abdullah (1996) katika kushadidia hoja hii anafafanua kwamba:

It is currently estimated that well over 100 million people use Swahili for communication. It is the official language for Tanzania, Kenya and Uganda. The language enjoys a unique position particularly at primary and intermediate level education at which is the official medium of instruction in these countries.

Inakadiriwa kwamba, zaidi ya watu milioni 100 wanatumia lugha ya Kiswahili kwa mawasiliano. Kiswahili ni lugha rasmi kwa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu sana katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari ambapo hutumika kama lugha rasmi ya kufundishia (Tafsiri Yangu).

Dondoo hili linashadidia hoja kwamba, Kiswahili kinatumiwa na sehemu kubwa ya watu duniani katika shughuli zao za kila siku. Watumiaji zaidi ya milioni 100 hivi kwa uhakika zaidi wanatumia lugha ya Kiswahili kila siku. Hata hivyo, idadi hii bado ni ndogo sana ikilinganishwa na watumiaji halisi wa lugha ya Kiswahili katika nchi ambazo Kiswahili hakijafanywa kuwa lugha ya Taifa.

Lugha ya Kiswahili imepiga hatua kubwa ya maendeleo katika sekta ya elimu nchini Tanzania katika karne ya ishirini na moja. Vyuo vikuu nchini kikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania vimeanzisha shahada mbalimbali za awali, uzamili na uzamivu katika Kiswahili, ili kukikuuza na kukiendeleza Kiswahili. Kwa mujibu wa mtafitiwa mmoja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alinukuliwa akisema kwamba, “tumeamua kuanzisha shahada za awali, uzamili na uzamivu katika Kiswahili ili kuwezesha taifa kupata wataalamu watakaokiendeleza Kiswahili katika kufundisha na kufanya tafiti kuntu kuhusu lugha ya Kiswahili. Hii itasaidia kukuza zaidi lugha ya Kiswahili nje na ndani ya nchi”. Hata hivyo, wakati vyuo vyetu tajwa hapo juu vimefikia kufanya uamuzi wa kuanzisha shahada hizo hivi karibuni, nchini Kenya shahada hizo zilikwisha anzishwa miongo kadhaa iliyopita. Kwa kufanya hivyo, wataalamu mbalimbali wameweza kuzalishwa na kuwa walimu na wahadhiri wa lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani.

Kimsingi, kutokana na maendeleo haya yaliyopigwa na lugha ya Kiswahili ni dhahiri Kiswahili hakiwezi kuwa ni lugha ya vizalia wala asilia yake kuwa ni lugha ya Kiarabu, bali ni lugha yenye mizizi yake katika upwa wa Pwani ya Afrika

mashariki. Ni lugha yenye mashiko na mizizi ndiyo maana ikaweza kukuwa na kuenea kiasi hicho na kuwa lugha ya matumizi mapana. Kama ingekuwa ni lugha ya vizalia ni dhahiri kwamba ingekufa na kusambaratika mara tu baada ya utawala wa Kisultani kupinduliwa huko Zanzibar. Lugha ya Kiswahili, lugha adhimu yenye asili yake katika mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki inaendelea kukua na kuenea kwa kasi zaidi duniani kote hasa katika karne hii ya ishirini na moja.

5.5.3 Sekta ya Habari na Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili

Maendeleo ya lugha ya Kiswahili yanaonekana pia katika tasnia ya habari ambapo lugha ya Kiswahili inatumika katika kutolea habari katika vyombo mbalimbali vya habari vya nchini na vile vya nje ya nchi. Mhochi na Wairiru (2004) wanaeleza kwamba:

The broadcast media have also contributed immensely to the spread and populatization of Swahili. It is probably the most widely used African language in radio broadcasts in the world. You can tune in to Swahili programs in major broadcasting houses like VOA (America) BBC (England) and Deutschewelle (Germany). It is also heard in broadcasts in India, Japan, and China, not to mention the many that use of it in Africa.

Vyombo vya habari vimechangia sana katika kukuwa na kuenea kwa lugha ya Kiswahili. Inasadikika kwamba, Kiswahili ni lugha pekee ya Kiafrika inayotumika kwa kiasi kikubwa katika utangazaji wa redio ulimwenguni. Lugha ya Kiswahili inasikika katika matangazo ya redio kubwa duniani kama vile sauti ya Amerika, BBC (Uingereza) na DeutscheWelle (Ujerumani). Inasikika pia katika redio za India, Japan, China pamoja na nchi nyingi za Kiafrika (Tafsiri yangu).

Dondoo hili linaonesha kwamba, Kiswahili ni lugha inayokuwa kwa kasi kubwa sana hasa kutokana na matumizi yake katika utangazaji na upashanaji wa habari miongoni mwa wanajamii. Lugha hii kusikika katika vyombo tajwa vya habari. Kwa mfano,

kuna mtafitiwa mmoja katika kisiwa cha Unguja ambaye alieleza kwamba lugha ya Kiswahili kutumika katika vyombo vikubwa vya habari duniani. Vile vile, kutumika kwa lugha ya Kiswahili katika matangazo ya redio mbalimbali ulimwenguni kunaitangaza nchi ya Tanzania ambako ndiko chimbuko la lugha ya Kiswahili. Watu wasikiapo lugha hiyo huuliza lugha hii ni ya wapi na ni ya watu gani? Wanapata jibu kwamba, ni ya Tanzania katika ukanda wa Afrika ya Mashariki basi huvutiwa na kuja kutembea Tanzania kama watalii ambao, huliingizia taifa fedha nyingi za kigeni kupitia mbuga za wanyama mlima Kilimanjaro na vivutio vingine.

5.5.4 Fasihi na Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili

Kama tulivyokwisha ona hapo nyuma lugha ya Kiswahili imepiga hatua kubwa sana ya maendeleo na kutumika katika sekta mbalimbali. Fasihi ya Kiswahili kama sekta ya taaluma inayojitegemea imechangia sana katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili duniani kote. Katika ukanda wa Afrika ya Mashariki kwa mfano, lugha ya Kiswahili imetumika kuandika kazi nyingi za fasihi andishi kama vile tamthilia, riwaya, ushairi na hadithi fupi. Vile vile, Kiswahili kimeendelea kuwa ndiyo lugha kuu inayotumika katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. Nilizungumza na mwanafasihi mmoja kutoka Dar es Salaam ambaye alinieleza kwamba:

Fasihi ya Kiswahili imechangia kwa kiasi kikubwa katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Nitazamapo ukanda wa Afrika ya Mashariki hasa Kenya na Tanzania kuna kazi nyingi za riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi ambazo zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Kazi hizi zinasaidia sana katika kukuza msamiati wa lugha na pia kukieneza Kiswahili pale kazi hizo zinaposomwa na watu mbalimbali nje na ndani ha Afrika.

Dondoo hili linashadidia hoja kwamba, lugha ya Kiswahili imekuwa sana katika karne ya ishirini na moja kutokana na matumizi yake katika kuandika kazi

mbalimbali za fasihi ya Kiswahili. Kazi kama vile *Rosa Mistika* kwa mfano, si tu kwamba inasomwa na watu mbalimbali duniani bali pia imekuwa ikifanyiwa tafiti mbalimbali katika shahada za uzamili na uzamivu katika vyuo vikuu mbalimbali duniani. Tafiti hizo zimewezesha kuandikwa kwa vitabu, makala na mijadala ambayo nayo kwa njia moja ama nyingine imesaidia katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

Kazi mbalimbali za kifasihi zimesaidia pia kukuza utamaduni wa lugha ya Kiswahili katika pande mbalimbali duniani. Tunaposema utamaduni wa lugha ya Kiswahili tunamaanisha utamaduni wa Mswahili kuwa ni mtu mpole, mkarimu, mwenye busara, huruma, mvumilivu na mchangamfu. Watu mbalimbali wasomapo kazi hizi huwaelewa Waswahili kuwa ni watu wa aina gani na hivyo kuvutiwa kuja kuwaona Waswahili ana kwa ana katika maisha yao ya kila siku. Kwa kufanya hivyo, taifa linafanikiwa kuongeza idadi ya fedha za kigeni ambazo hutumika katika kugharimia huduma mbalimbali za kijamii kama vile maji, umeme, elimu, afya, nishati, barabara na kadhalika. Hivi ndivyo namna lugha ya Kiswahili inavyolisaidia taifa katika kukuza uchumi wake pamoja na wa watu wake.

Kimsingi, katika kushadidia hoja hii nilifanya mahojiano na mtafiti mmoja mwenye asili ya Libya na ambaye kwa sasa anasoma shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye alieleza kwamba, yeye alivutiwa kusoma shahada ya Kiswahili baada ya kufanikiwa kusoma riwaya ya *Kusadikika* (1951) ya Shaaban Robert. Anaeleza kwamba, alipoisoma riwaya hiyo na kuirudia zaidi ya mara tano, aliilewa vizuri na kisha akaona kuna haja na yeye kusoma lugha ya Kiswahili. Kwa

hivi sasa mwanafunzi huyu analipa fedha za kigeni katika kugharamia masomo yake ambapo chuo na taifa kwa ujumla kinanufaika. Hata hivyo, manufaa hayapo katika fedha tu kwani mwanafunzi huyu amalizapo masomo yake anarejea nchini Libya ambapo anakwenda kufundisha lugha ya Kiswahili kwa Walibya. Kwa kufanya hivyo, lugha ya Kiswahili inaendelea kukua zaidi na zaidi.

Matumizi ya lugha ya Kiswahili yamevuka mipaka na kutumika si tu katika fasihi ya Kiswahili bali pia katika fasihi mbalimbali ulimwenguni. Alli (2012) anasema:

The Swahili language is also making its presence in the art world – in songs, theatres, movies and television programs. For example, the Lyrics for the song titled “Liberian girl” by Michael Jackson has Swahili phrases’ “Nakupenda pia, nakutaka pia, mpenzi wee!” (I love you, and i want you, my dear. The well celebrated disney movies “The Lion King” flatures several Swahili words for example “Simba” (Lion), “rafiki” (friend), as the names of the characters. The Swahili phrase “hakuna matata” (No troubles or no problems) was also used in that movie.

Lugha ya Kiswahili inaonekana kutumika kati nyimbo na tamthilia/filamu za kimataifa katika televisheni. Kwa mfano, katika wimbo uitwao “Liberian girl” wa Michael Jackson una maneno ya Kiswahili. “Nakupenda pia, nakutaka pia, mpenzi wee! Vile vile, katika filamu maarufu ya Disney Movie, “The Lion King” ina matumizi ya msamiati mwingi wa lugha ya Kiswahili. Maneno hayo ni “Simba”, “rafiki” ambayo ni majina ya wahusika. Vile vile, maneno “hakuna matata” yametumika katika filamu hiyo. (Tafsiri Yangu).

Matumizi ya maneno tajwa katika nyimbo na filamu za kimataifa ni dalili tosha za kuonesha kwamba, lugha ya Kiswahili inakubalika kimataifa. Haya kwa hakika ni maendeleo makubwa, sana kupata kufikiwa na lugha ya Kiswahili inakubalika kimataifa; pia ni maendeleo makubwa sana kupata kufikiwa na lugha ya Kiswahili katika karne hii ya ishirini na moja. Kutokana na hatua hii tunaweza kueleza kwamba, iwapo Kiswahili kingekuwa ni lugha ya vizalia basi isingeweza kufikia

hatua hiyo ya maendeleo iliyoifikia badala yake ingekuwa imekwisha kufa. Hata hivyo, kwa kuwa si lugha ya vizalia imeendelea kukuwa na kukuwa zaidi kiasi cha kuwa lugha ya matumizi mapana katika ukanda wa Afrika Mashariki na matumizi madogomadogo katika nchi mbalimbali kimataifa.

Si hivyo tu, bali pia kwa upande wa filamu za hapa nchini, Kiswahili ndiyo lugha pekee inayotawala katika tasnia hiyo. Filamu zinazotengenezwa hapa nchini huoneshwa katika televisheni za ndani ya nchi na zile za digitali zinazoonekana dunia nzima. Shirika la DSTV la Afrika ya Kusini limeanzisha stesheni maalumu inayotumika kurusha matangazo ya filamu za Tanzania zilizoandaliwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hali hii filamu hizi zinaonekana dunia nzima na kwa namna ile ile zinakuza lugha ya Kiswahili na utamaduni wake. Kwa mfano, msanii maarufu wa filamu hapa nchini ambaye kwa sasa ni marehemu Steven Kanumba alifanikiwa kutengeneza filamu pamoja na wacheza filamu wakubwa wa Nigeria ambao ni maarufu duniani baada ya michezo yake kadhaa kwa lugha Kiswahili kuonekana katika DSTV. Waigizaji hao wa Nigeria walivutiwa na uigizaji wa Kanumba pamoja na lugha aliyoitumia yaani lugha ya Kiswahili.

5.5.5 Hitimishi

Katika sehemu hii nimefanya ufafanuzi juu ya namna Kiswahili kilivyofanikiwa kukuwa na kuenea duniani kwa kasi kubwa hasa katika karne ya ishirini na moja. Maendeleo haya yameonekana katika sekta za elimu, habari na mawasiliano, fasihi ya Kiswahili na ile ya ulimwengu. Tasnia hizi zimeonesha mafanikio makubwa katika lugha ya Kiswahili ambayo imesaidia kutoa nafasi nyingi za ajira hapa nchini.

Hoja kuu iliyoibuliwa katika sehemu hii ni kwamba, Kiswahili kingekuwa ni lugha ya vizalia basi ni dhahiri kwamba, lugha hii isingeliweza kupata maendeleo iliyoyapata katika karne ya ishirini na moja. Maendeleo haya yanaonesha kwamba, Kiswahili ni lugha yenye asilia yake katika Pwani ya Afrika ya Mashariki tangu kale kabla ya ujio wa Waarabu. Ujio wa Waarabu kwa mtazamo wetu ulisaidia kuikuza lugha ya Kiswahili kwa kuiongezea msamiati ambao ulihitajika kwa wakati ule na sasa lakini sio kwamba, ujio wa Waarabu ndio ulioanzisha Kiswahili. Hata hivyo, imebanika kwamba lugha ya Kiswahili itaendelea kukuwa kwa kasi kubwa sana katika miongo michache ijayo. Haya yamedhihirishwa na watafitiwa waliosailiwa na kuhojiwa katika utafiti huu.

5.6 Changamoto Zinazokabili Maendeleo ya Lugha ya Kiswahili Duniani

5.6.1 Utangulizi

Lugha ya Kiswahili kama tulivyoonesha hapo awali imepiga hatua kubwa sana ya maendeleo kiasi cha kutumika kama chombo cha mawasiliano katika sehemu mbalimbali duniani. Pamoja na maendeleo hayo zipo changamoto kadhaa ambazo zinaikabili lugha ya Kiswahili ambapo bila shaka zinakwamisha kasi ya maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa changamoto hizo ni hizi zifuatazo:

5.6.2 Upungufu wa Vitabu vya Kufundishia Wageni

Miongoni mwa mambo yaliyochangia katika kukuwa na kuenea kwa Kiswahili kwa kasi katika karne ya Ishirini na moja ni ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Ufundishaji wa lugha hii hufanywa katika nchi mbalimbali duniani huku Tanzania na Kenya zikiwa zinaongoza kwa idadi ya wanafunzi kwa upande wa nchi za Afrika.

Kwa upande wa dunia, nchi ya Marekani ndiyo inayoongoza katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Hata hivyo, ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni unakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vitabu vya Kiada na Ziada vyenye ubora unaostahili. Akizungumza katika shirika la Utangazaji la Uingereza kutokea Korea anapofundisha Kiswahili, Mahenge (2012, Septemba) anasema:

Ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni unakuwa mgumu sana kwa sababu hakuna vitabu vya kiada na ziada vya kutosha. Mpaka sasa kuna kitabu kimoja tu ambacho kimechapishwa na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho ndicho kinachotumika katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni. Kitabu hiki pamoja na mapungufu yake kinasaidia sana katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Hivyo basi, wataalamu wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni wanapaswa kuandika vitabu vya kutosha kwa ajili ya kufundishia lugha ya Kiswahili.

Tunakubaliana na mawazo ya Mahenge (ameshatajwa) kuwa ni kweli kuna uhaba mkubwa wa vitabu vya kufundishia Kiswahili kwa wageni. Ukweli huu unatoa pingamizi kwa wanafunzi wengi duniani kujifunza lugha ya Kiswahili kwa sababu wanaiona kuwa ni lugha ngumu sana. Iwapo wangukuwa na vitabu vya kutosha tena vilivyoandikwa kwa umahiri mkubwa basi ni dhahiri kwamba, wangukiona Kiswahili kuwa ni lugha rahisi na hivyo kuvutiwa kujifunza lugha hii adhimu.

Kimsingi, tunakubaliana na mawazo ya Mahenge (2012) kwa sababu mimi mwenyewe (mwandishi wa tasinifu hii) nimejifunza Kiswahili kama mgeni na nimekutana na shida hizo. Nilipata taabu sana kujifunza Kiswahili kwa kuwa hakukuwa na aina mbalimbali za vitabu vya kujifunzia kule nchini Libiya. Hata hivyo, nilijitahidi sana na baadaye nikaweza kuzungumza na kuandika kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Upungufu wa vitabu vya kiada na ziada katika kufundishia Kiswahili kwa wageni unakwenda sambamba na kutofanyika kwa utafiti wa kina ili kubaini mahitaji ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama wageni. Utafiti unaweza kufanyika wakati wanafunzi wanajifunza Kiswahili kwa wageni na kisha kuainisha mahitaji yao na hatimaye kuyajumuisha katika vitabu vipya vya kiada na ziada vinavyotungwa ama vitakavyotungwa. Kwa kufanya hivyo itawezesha kupatikana kwa vitabu ambavyo havina mushkeli katika ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni.

5.6.3 Upungufu wa Wataalamu wa Kufundisha Lugha ya Kiswahili kwa Wageni

Ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa ageni unahitaji wataalamu wakutosha ili kukidhi mahitaji ya soko la ufundishaji wa lugha ya Kiswahili. Hali ilivyo sasa ni kwamba, wataalamu wa lugha ya Kiswahili kwa wageni ni wachache sana. Kwa mujibu wa mtafiti mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam anasema kwamba:

Kiswahili kwa wageni hasa katika nchi zilizoendelea kama vile Marekani kinafundishwa na watu ambao kimsingi hawana taaluma ya Kiswahili kwa wageni. Mswahili yeyote hasa kutoka Kenya anapoingia Marekani basi anajidai kuwa yeye ni mwalimu wa lugha ya Kiswahili na kupewa jukumu la kufundisha lugha ya Kiswahili. Hii imechangiwa sana na kukosekana kwa wataalamu stahiki wa lugha ya Kiswahili hasa Kiswahili kwa wageni.

Mawazo haya ni muafaka katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba, maendeleo ya lugha ya Kiswahili hayatakuwa kwa kasi inavyostahili kutokana na ukosefu wa wataalamu wabobezi wa lugha ya Kiswahili. Kiswahili kwa wageni kinapofundishwa na mtu ambaye si mtaalamu huwakwaza wanafunzi kwa namna mbalimbali. Mosi, mwalimu anakuwa hajaiva katika nadharia za ufundishaji wa lugha na hivyo kushindwa kutambua mapungufu ya kila mwanafunzi na kisha

kumsaidia kila mwanafunzi kulingana na mahitaji yake kwa kuongozwa na nadharia ya ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni. Pili, wanafunzi wengi hasa wanaojifunza lugha ya Kigeni hupenda kuuliza maswali mengi kwa mwalimu. Walimu wengi hasa wale ambao si wabobezi wa Kiswahili kwa wageni hushindwa kujibu maswali hayo. Kwa hali hiyo mwanafunzi hukata tamaa ya kujifunza lugha ya Kiswahili na hivyo kupunguza kasi ya maendeleo ya lugha ya Kiswahili duniani.

Vilevile, wanafunzi wa Kiswahili kwa wageni wanapouliza maswali na mwalimu kushindwa kuyajibu hutoa picha mbaya kwa walimu na wanataalimu wa Kiswahili kwamba ni wababaishaji tu na hawana lolote. Hii haishii hapo tu bali pia, hushusha hadhi ya lugha ya Kiswahili mbele ya wageni na kuonekana kuwa ni lugha ya ajabu ajabu ambayo haifundishiki. Tunasema hivi kwa sababu, wanafunzi wa kigeni hawatatambua kwamba huyu mwalimu anavyofundisha si mbobezi bali watamuona kwamba ni mbabaishaji tu asiye na utaalamu wa mbinu na nadharia za ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni. Wao watafahamu kwamba, huyu ndiye mtaalamu tena mbobezi lakini alichobobea hakionekani. Hii kwa hakika inachangia sana katika kurudisha nyuma kasi ya ukuaji na ueneaji wa lugha ya Kiswahili duniani.

Kimsingi ni dhahiri kwamba, watu mbalimbali hasa Watanzania ambako ndiko chimbuko la lugha ya Kiswahili wanapaswa kujitokeza kwa wingi katika kujifunza lugha ya Kiswahili na kisha kujaza nafasi nyingi zilizoko katika soko la ajira. Vijana wadogo wanaomaliza shule za msingi na wale wanaomaliza shule za sekondari wanapaswa wabadili mtazamo wao juu ya lugha ya Kiswahili. Wengi wa vijana

hawa huacha kusoma somo la Kiswahili kwa madai kwamba, hawataweza kunufaika kiuchumi watakapoboea katika Kiswahili kama ambavyo watanufaika kwa kuboea katika taaluma nyingine kama vile sheria, uchumi, udaktari uhasibu na kadhalika. Kutokana na hali hiyo lugha ya Kiswahili inakosa wataalamu ambao wangesaidia katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili kwa kasi zaidi. Mtazamo huu si sahihi hata kidogo na unapaswa ukomeshwe kwa kuwafafanulia vijana faida ambazo wanaweza kuzipata wao binafsi na taifa kwa ujumla iwapo watafanya uamuzi wa kusoma na kuboea katika taaluma ya Kiswahili.

5.6.4 Sera ya Lugha ya Taifa

Sera ya lugha ya taifa ndiyo muongozo unaofafanua nafasi ya lugha katika matumizi ya mawasiliano ya jamii ya kila siku pamoja na uendeshaji wa shughuli mbalimbali za utawala na maisha ya jamii. Nchini Tanzania ambako ndiko chimbuko la lugha ya Kiswahili hakuna sera maalumu ya lugha ya Kiswahili na badala yake Kiswahili kimeunganishwa na utamaduni katika sera moja. Ni ukweli usioplingika kwamba, lugha ni sehemu ya utamaduni na lugha ndicho chombo kinachotumika katika kuufasili ama kuelezea utamaduni wa jamii husika. Hata hivyo, kwa hadhi iliyo nayo lugha ya Kiswahili na nafasi yake katika mawasiliano duniani kinapaswa kuwa na sera yake inayojitegemea. Kiswahili kuunganishwa katika sera ya utamaduni kinapata changamoto zifuatazo:

Sera ya lugha ndiyo inayobainisha umuhimu wa jambo na ukipaumbele wake katika kupatiwa fedha na rasilimali stahiki katika kuendeleza jambo hilo. Kwa hali hii nafasi ya lugha ya Kiswahili katika sera hii imejificha sana kiasi cha kutoonekana

umuhimu wake na ukipaumbele wake katika masuala ya bajeti na hivyo kuzuia kasi ya ukuaji na ueneaji wake duniani. Tulipofanya usaili na mtafitiwa mmoja kutoka Unguja kuhusiana na jambo hili alieleza kwamba:

Kutokuwapo kwa sera maalumu ya lugha ya Kiswahili kumechangia sana katika kudumaza harakati za kuikuza lugha ya Kiswahili. Hii inatokana na ukweli kwamba, Wizara inapoandaa bajeti inatazama sera zake. Kwa kuwa Kiswahili kipo katika sera ya utamaduni basi fedha zinazotengwa ni za kuendeleza utamadunina Kiswahili kikiwepo. Kimsingi, utamaduni unahusisha mambo mengi sana na hivyo kiasi kinachotengwa kwa ajili ya kuendeleza lugha ya Kiswahili ni kidogo sana.

Dondoo hili, kimsingi linashadidi hoja yetu ya awali kwamba, Kiswahili hakitaweza kukuwa na kuenea kwa kasi inavyotegemewa kama hakitakuwa na sera yake inayojitegemea ili kukiwezesha kutengewa bajeti yake stahiki.

Vilevile, lugha ya Kiswahili kukosa sera yake maalumu kunakifanya kukosa ufuatiliaji na uangalizi wa karibu kama vile kingekuwa na sera yake inavyojitegemea. Kwa mfano, katika kutathmini sera ya utamaduni na lugha ni dhahiri mtathimini atatoa tathmini ya jumla kuhusu utamaduni na kisha kwa ufupi kuhusu lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni sehemu ya sera hiyo. Uchambuzi na uhakiki wa kina kuhusu lugha ya Kiswahili hautafanywa kama inavyopasa kama Kiswahili kingekuwa na sera yake inayojitegemea. Kimsingi, kukosekana kwa uchambuzi na uhakiki wa kina kuhusu lugha ya Kiswahili na maendeleo yake kisera kunadumaza kasi ya ukuaji na ueneaji wake duniani kote.

Si hivyo tu, bali pia, kukosekana kwa sera ya lugha ya taifa kumechangia kutotiliwa maanani kwa matamko mbalimbali yanayotolewa katika sera ya utamaduni na lugha kwa ukaribu unaostahili. Kwa mfano imesemwa kwamba, Kiswahili ndiyo lugha kuu

ya mawasiliano ambayo pia ndiyo lugha rasmi ya taifa. Kwa hivyo, lugha hii ndiyo inayopasa kutumika katika sehemu mbalimbali za mawasiliano rasmi kama vile bugeni na sehemu nyinginezo. Kwa hakika, hali haiko hivyo pale ambapo lugha ya Kiingereza inatawala uandishi wa sera na mipango mbalimbali ya maendeleo inayowasilishwa bungeni. Kimsingi, miswaada hii ilipaswa iandikwe kwa lugha ya Kiswahili ili hata wale wanaoijadili waweze kuielewa na kuijadili vizuri ili ilete tija kwa taifa. Hii yote pamoja na mambo mengine yanachangiwa sana na kutokuwepo kwa sera ya lugha ya Kiswahili inayojitegemea.

5.6.5 Utashi wa Kisiasa katika Masuala ya Lugha

Changamoto nyingine inayoikabili lugha ha Kiswahili na maendeleo yake ni utashi wa kisiasa ambao bado hauridhishi kwa kiwango kikubwa. Kukosekana kwa utashi wa kisiasa katika kukiendeleza Kiswahili kunatokana na mambo mengi ila hapa tumetafiti mawili tu. Mambo hayo ni uwoga na pili ni mawazo ya kikoloni waliyonayo wengi kati ya viongozi wakuu wa kisiasa nchini. Uwoga unaozungumzwa hapa ni ule kwamba, iwapo Kiswahili kitafanywa kuwa ndiyo lugha ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi mbalimbali za elimu mpaka Chuo Kikuu basi wahitimu hawataweza kupata ajira katika soko la ajira la kimataifa. Tunasema huu ni woga kwa sababu, yapo mataifa ambayo yameamua kutumia lugha zao za taifa katika kufundisha na kujifunza taaluma mbalimbali na kufanikiwa kupiga hatua kubwa ya maendeleo. Mfano wa nchi hizo ni China, Japan na Korea. Nchi ya Korea kwa mfano, ilikuwa chini kimaendeleo kuliko Tanzania katika miaka ya 1960 lakini leo ni nchi ambayo ipo katika orodha ya nchi 10 tajiri duniani na Tanzania ipo katika orodha ya nchi 10 masikini duniani. Mfano wa nchi hizi unatosha kabisa kuwafanya

viongozi wa Tanzania nao kuona haja ya kukifanya Kiswahili kuwa ndiyo lugha ya ufundishaji na ujifunzaji wa taaluma mbalimbali ili kuwezesha taifa kupata wataalamu wabobezi watakaoliletea taifa maendeleo endelevu.

Vilevile, mawazo ya kikoloni bado yamewaathiri viongozi wa serikali kiasi cha kuamini kwamba, Kiingereza ndiyo lugha pekee yenye ubora duniani na hivyo kuanzisha ustaarabu wa kutumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia elimu ya juu kutaifanya elimu yetu kukosa hadhi duniani na nchini pia. Hali hii haipo kwa viongozi peke yake bali hata baadhi ya wasomi ambao ni maprofesa wa vyuo vikuu katika taaluma mbalimbali.

Mkoloni aliamua kuzishusha hadhi lugha za jamii walizozitawala ili kuweza kuwatawala vizuri kwa kuwafanya waone na kuamini kila kitu chao ni duni na hakina hadhi ila kile cha wageni ndicho bora na chenye hadhi katika jamii. Kwa hili waliweza kufanikiwa sana na kuweza pamoja na mambo mengine kunyonya rasilimali za Watanzania na Waafrika kwa ujumla. Hata hivyo, viongozi na wasomi wetu hawakuliona jambo hili na badala yake wanaendeleza utumwa huu wa kifkira.

Kwa mujibu wa mtafitiwa mmoja kutoka Dar es Salaam anasema kwamba:

“Si jambo la ajabu kumkuta profesa anamsema vibaya mwanafunzi au mwalimu mwenzake kwa kutokujua kuzunguza Kiingereza kwa ufasaha. Swala la msingi hapa la kujiuliza ni kwamba, hivi kujua kuzungumza Kiingereza kwa ufasaha ndiyo ujuzi na wingi wa maarifa. Wapo watu wanaojua kuzungumza Kiingereza vizuri lakini kichwani hamna kitu ukilinganisha na wale wasiojua kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha.

Mawazo haya yanashadidia hoja yetu ya msingi kwamba, utashi wa kisiasa ndio unaotakiwa kuchukua mkondo wake ili kufuta mawazo haya ya kikoloni kuhusu

lugha ya Kiswahili dhidi ya lugha ya Kiingereza. Iwapo Kiswahili kitakuwa ndiyo lugha ya kufundishia katika ngazi zote za elimu nchini ni dhahiri kwamba, taifa litapata wataalamu wengi wenye ubora unaotakiwa lakini pia hata watu wa mataifa mbalimbali wataona kwamba sisi tunakipa Kiswahili thamani kubwa na wao bila shaka watazidi kukipenda Kiswahili. Ikiwa hivyo ndivyo, lugha ya Kiswahili itaendelea kukua na kuenea kwa kasi kubwa zaidi katika sehemu mbalimbali duniani.

Si hivyo tu bali pia, baadhi ya wananchi nao wamekuwa na kasumba hasi juu ya lugha ya Kiswahili. Si jambo la kawaida kumkuta mzazi akimuhimiza mwanae asome ama ajifunze taaluma zinazohusiana na somo la Kiswahili. Wazazi wengi huwahimiza watoto wao kusoma masomo yanayohusiana na sheria, biashara, udaktari, uchumi na uhasibu ili waweze kupata masilahi mazuri ya kifedha. Na unapolitazama hili unaona kwamba, wazazi hawa hawajatoa kasumba dhidi ya somo la Kiswahili na lugha ya Kiswahili kwa ujumla katika vifua vyao bali kutoka kwa viongozi na wanataaluma wetu ambao ndio wa kwanza katika kuidharau lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, kasumba hii inaanza kuisha taratibu pale ambapo wageni kutoka nje ya nchi hii wanapokuja kusoma na kujifunza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania na ndipo watu mbalimbali wakiwemo viongozi kuanza kuona kwamba, lugha hii ni njia ya kuleta maendeleo kwa taifa na mtu mmojammoja. Haya yanaonekana pale ambapo lugha ya Kiswahili inatoa ajira nyingi duniani na hao wanaajiriwa huko wananufaika wao binafsi, familia zao na taifa kwa ujumla.

5.6.6 Kukosekana kwa Chombo Rasmi cha Kusimamia Uendelezaji wa lugha ya Kiswahili katika ukanda wa Afrika ya Mashariki

Waswahili walisema, umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Methali hii inajidhihirisha pale ambapo kumekuwa hakuna chombo rasmi chenye dhima ya kusimamia uendelezaji wa lugha ya Kiswahili katika ukanda wa Afrika ya Mashariki ambako ndiko chimbuko la lugha ya Kiswahili. Kila nchi iliyopo katika ukanda wa Afrika ya Mashariki unafanya mikakati yake binafsi ya kukiendeleza Kiswahili huku kukiwa hakuna umoja katika hili. Kwa mfano, nchini Tanzania serikali ilianzisha Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kama chombo cha kuratibu na kusimamia maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini.

Baraza hili linatekeza majukumu mbalimbali yakiwemo yale ya kuishawishi serikali kukuza utamaduni wa Kiswahili, kuwapa mori na motisha watunzi wa vitabu vya Kiswahili, kupitia na kuhakiki majarida mbalimbali ya kuendeleza Kiswahili kutunza utamaduni wa Kiswahili, kuandaa Kamusi mpya zinazokwenda na wakati ili kukidhi mahitaji ya walengwa, kuandaa mikakati mbadala juu ya mfumo wa lugha ya Kiswahili na kuandaa semina za kuelimisha walimu wa Kiswahili.

Nchini Kenya kuna taasisi ijulikanayo kama Chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA) ambacho kimeanzishwa mwaka 1998. Chama hiki cha Kiswahili kina wanachana mbalimbali kutoka katika vyuo vikuu, vyombo vya habari, wachapishaji waandishi wa vitabu na watumishi mbalimbali wanaojihusisha na uendelezaji wa lugha. Kazi zilizofanywa na chombo hiki hazitofautiani sana na zile za BAKITA ila CHAKITA imepiga hatua kubwa ya kuhakikisha kwamba, Kiswahili kinaingizwa

katika katiba ya nchi na kutangazwa kama lugha ya Taifa na lugha rasmi. Hili lilifanikiwa pale katiba mpya ilipoundwa mnamo mwaka 2010.

Kimsingi, tulichotaka kuonesha hapa ni kwamba, harakati za kukiendeleza Kiswahili zinafanywa kipeke peke hali ya kuwa ni lugha kubwa inayotumika katika sehemu kubwa ya Afrika ya Mashariki. Iwapo kungekuwa na baraza ama taasisi maalumu inayoratibu maendeleo ya lugha ya Kiswahili Afrika ya Mashariki na Kati ni dhahiri kwamba, zingetungwa sera na mipango endelevu ya kukiendeleza Kiswahili. Taasisi tunayoizungumza hapa ni ile ambayo itakuwa ni kamisheni katika Shirikisho la Afrika ya Mashariki na itapangiwa bajeti yake maalumu. Hata hivyo, hivi karibuni amesikika afisa mmoja kutoka ngazi za juu za jumuiya ya Afrika ya Mashariki akisema kwamba:

Jumuiya ya Afrika ya Mashariki inakusudia kuanzisha kamisheni kadhaa za jumuiya hiyo huku kamisheni ya Kiswahili ikiwa ni mojawapo. Kamisheni hii itakuwa ni chombo rasmi cha kusimamia na kuratibu shughuli mbalimbali za kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Vilevile, kamisheni hii inategemewa kuwa na makao makuu yake huko Zanzibar ingawa bado haijapitishwa rasmi.

Dondoo hili linatoa matumaini kwamba, huenda lugha ya Kiswahili ikapata chombo maalumu cha kuisimamia na kuiratibu kwa namna ya umoja zaidi kuliko kuiachia kila nchi kufanya uratibu huo kipeke peke. Hatusemi kwamba taasisi zilizoanzishwa katika kila nchi zifutwe la! Kwani taasisi hizi zimetoa na zinaendelea kutoa mchango mkubwa sana katika kuiendeleza lugha ya Kiswahili. Tunachosema hapa ni kwamba, kuwepo kwa Kamisheni ya Afrika ya mashariki ya kuratibu lugha ya Kiswahili kutasaidia kuunganisha taasisi zilizopo katika nchi wanachama ili kuleta ufanisi na tija katika kukiendeleza Kiswahili. Tunayasema haya kwa sababu, harakati

mbalimbali za kukiendeleza Kiswahili zimefanywa katika nchi mbalimbali lakini bado kuna kusuasua katika utekelezaji ambao tunaamini uanzishaji wa kamisheni ya lugha utasaidia kukuza lugha. Kwa mfano; inaelezwa kwamba:

Uongozi wa Awamu ya Kwanza uliweka mwongozo na vyombo vya kukuza lugha ya Kiswahili Kitaifa. Hata hivyo, mwishoni mwa “Awamu” hiyo pamekuwa na kulegalega katika juhudi za kukuza Kiswahili. Sera “mpya” ya elimu ya juu haikuipa nafasi lugha ya Kiswahili, bali imesisitiza zaidi matumizi ya lugha ya Kiingereza. Kiswahili kimelaumiwa kuwa kimesababisha kushuka kwa kiwango cha elimu nchini... hakuona sera kamili ya lugha ya taifa. Wakuzaji wa Kiswahili hawajaeleza sababu wala kupewa malengo ya kufikia katika shughuli zao. Kila siku wanaunda istilahi na kuandika vitabu vya kitaaluma lakini hawaelezi istilahi na vitabu hivyo vitatumiwa lini na wapi! Ukosefu wa Sera ya lugha nchini ndicho kikwazo kikubwa cha maendeleo ya lugha ya Kiswahili leo (TUKI, 1985:vii).

Dondoo hili linatoa uhalisia wa mambo ulivyo pale kila nchi inapoachiwa jukumu la kuendeleza lugha ya Kiswahili kipeke hivyo basi kuanzishwa kwa kamisheni ya lugha ya Kiswahili nchini ya jumuiya ya Afrika Mashariki itasaidia sana kusukuma mbele changamoto zinazoikabili lugha ya Kiswahili katika nchi wanachama.

5.6.7 Hitimishi

Katika sehemu hii tumeleza changamoto mbalimbali zinazoikabili lugha ya Kiswahili na maendeleo yake duniani, Afrika na Afrika ya Mashariki. Changamoto zote zilizo rodheshwa zinaonekana kwamba ziko katika uwezo wa mwanadamu katika kuzitatua. Kwa mfano, suala la ukosefu wa vitabu vya kiada na ziada katika kufundisha Kiswahili hasa kwa wageni. Tatizo hili ni rahisi sana kutatulika iwapo wanataaluma watakuwa tayari kukaa chini na kuandika vitabu vya kiada na ziada kwa wingi kwa ajili ya kufundishia Kiswahili kwa wageni.

Suala la ukosefu ama upungufu wa walimu na wataalamu wa kufundisha somo la Kiswahili nalo litatatuliwa pale ambapo wanafunzi kutoka sekondari watakapoamua kwa dhati kabisa kufanya ubobezi katika taaluma za Kiswahili huku wazazi wakiwahimiza kufanya hivyo. Changamoto nyingine ni zile za kisera ambazo ziko katika uwezo wa Serikali ambapo utashi wa kisiasa ndio unaotakiwa ili kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili inazidi kukua na kuenea zaidi na zaidi duniani kote.

SURA YA SITA

MUHTASARI, HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

6.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho katika utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu ndogo ndogo tatu za muhtasari, hitimishi na mapendekezo. Katika sehemu ya kwanza imelezwa kwa kifupi hoja za msingi za kila sura. Matokeo ya utafiti kulingana na malengo ya utafiti yaliyokuwa yamefafanuliwa katika sehemu ya pili. Katika sehemu ya tatu, rai kuhusu fursa za kiutafiti zitakazosaidia kuimarisha masuala ya kiutafiti zimejadiliwa.

6.2 Muhtasari

Utafiti huu umejengwa na sura sita zilizo imara na madhubuti. Sura ya kwanza inahusu masuala ya kiutangulizi, sura ya pili ni mapitio ya kazi tangulizi, sura ya tatu inahusu nadharia zilizoongoza utafiti na sura ya nne imewasilisha mbinu na njia mbalimbali za utafiti zilizomuongoza mtafiti katika kukamilisha utafiti wake. Vile vile, sura ya tano imewasilisha uchambuzi wa data na sura ya sita ikifanya hitimisho la utafiti mzima pamoja na kutoa mapendekezo. Ufuatao ni muhtasari wa kila sura.

Sura ya kwanza imewasilisha vipengele mbalimbali ambavyo kwavyo ndivyo vilivyotoa ithibati ya kufanyika kwa utafiti huu. Vipengele hivyo ni pamoja na mada husika ya utafiti ambayo ni “Mtazamo wa Kilughawiya jamii katika kuathiriana kwa lugha za Kiswahili na Kiarabu na hatma ya Maendeleo ya lugha ya Kiswahili”. Sura hii pia imefafanua vipengele vingine kama vile usuli wa mada, tatizo la utafiti, usuli wa tatizo la utafiti ambapo ndani mwake kuna; maendeleo ya Kiswahili na

mahusiano baina ya Kiswahili na Kiarabu. Vipengele vingine vilivyowasilishwa katika sura hii ni pamoja na lengo la utafiti lililojumuisha malengo mahususi matatu, maswali ya utafiti kulingana na malengo mahususi ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, vikwazo vya utafiti na utatuzi wa vikwazo.

Vipengele tajwa hapo juu vilionesha kwamba ipo haja ya msingi ya kufanyika utafiti wa kina katika kuchunguza juu ya kuathiriana kwa Kiswahili na Kiarabu kwa kutumia mtazamo wa Kiisimu jamii ili kuziba pengo la kiutafiti linaloonekana kupwaya katika tafiti tangulizi zilizo tangulia. Kwa msingi huo basi, sura iliyofuata imewasilisha nadharia mbalimbali zilizomwongoza mtafiti katika kutimiza malengo yake ya kiutafiti.

Sura ya pili ya utafiti huu imefanya tahakiki ya nadharia mbalimbali na kufanya uteuzi wa nadharia chache zilizoongoza utafiti katika kufanikisha malengo yake. Nadharia hizo ni pamoja na lugha kama mfumo wa Kiishara na Kimuundo, lugha kama nyenzo ya Kiuamilifu, lugha kama Muundo Jamii, nadharia ya lugha za Kipijini na nadharia ya kwamba Kiswahili ni Krioli. Nadharia nyingine ni pamoja na Kiswahili asili yake ni Kongo, Kiswahili ni lugha ya Vizalia na nadharia ya mwisho ni ile isemayo Kiswahili ni Kiarabu. Mwishoni mwa sura hii nimeteua nadharia tatu ambazo ndizo zilizoningoza katika utafiti wangu. Nadharia hizo ni, lugha kama Muundo Jamii, Kiswahili ni Kiarabu na Kiswahili ni lugha ya Vizalia. Nadharia hizi teule zimesaidia kuniongoza katika kufikia lengo la utafiti kama ilivyowasilishwa katika sura ya tano ya tasnifu hii. Sura iliyofuata imewasilisha kazi tangulizi kuhusiana na mada ya utafiti.

Sura ya tatu ya tasnifu hii imefanya mapitio ya kazi tangulizi kadhaa ambazo kwazo ithibati ya utafiti huu kufanyika ikapatikana. Miongoni mwa masuala yaliyowasilishwa katika sura hii ni lahaja za lugha ya Kiswahili, mahusiano baina ya Kiswahili na Kiarabu, suala la lugha kukopa msamiati kutoka lugha nyingine na fasihi ya Kiswahili na ile ya Kiarabu. Masuala mengine yaliyopitiwa ni Kiswahili na Uislamu. Mapitio ya kazi tangulizi kupitia vichwa vya habari vilivyoenezwa katika aya hii yameonesha kwamba hakuna utafiti wa kina uliofanywa kuhusiana na kuathiriana kwa lugha ya Kiswahili na Kiarabu kwa mtazamo wa Kiisimu jamii. Hali hii ikasababisha kuibuka kwa mada kwamba Kiswahili pekee ndicho kilichoathiriwa na Kiarabu. Sura iliyofuata imewasilisha mbinu na njia mbalimbali za utafiti.

Sura ya nne ya tasnifu hii imefanya uwasilishaji juu ya mbinu na njia mbalimbali za utafiti ambazo kwazo, ukusanyaji na uchambuzi wa data ukaweza kufanikiwa. Vipengele vilivyoenezwa katika sura hii ni pamoja na usanifu wa utafiti, vyanzo vya data; data za msingi na upili, mbinu za utafiti; mbinu ya ushiriki, mbinu ya mahojiano, upitiaji wa nyaraka na uchambuzi wa kimaudhui. Vipengele vingine vilivyojadiliwa ni pamoja na uteuzi wa watafitiwa, usahihi wa data, kuaminika kwa data na maadili ya utafiti. Njia na mbinu hizi za utafiti ndizo zilizowezesha yote yanaonekana katika sura ya tano ya tasnifu hii kuwa kama yanavyoonekana.

Sura ya tano ya tasnifu hii imefanya uchambuzi wa data pamoja na mjadala ambao umewezesha kujibu maswali ya utafiti huu. Uchambuzi wa data ulifanywa kufuatana na malengo ya utafiti. Masuala yaliyochambuliwa katika sura hii ni pamoja na chimbuko la Kiswahili na sababu mbalimbali zilizowafanya wataalamu mbalimbali

wa lugha kudai kwamba, Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu. Sababu hizo ni pamoja na watafiti wa mwanzo wa lugha ya Kiswahili kuwa ni wageni, Kiarabu kufundishwa katika madrasa, Kiswahili kimekopa msamiati mwingi kutoka lugha ya Kiarabu, lafudhi ya matamshi ya Kiswahili kufanana na Kiarabu na ushairi wa Kiswahili asili yake ni Uarabu na Uislamu. Sababu hizi zimechambuliwa na kufafanuliwa kwa kina kwa kutumia mtazamo wa Kilughawiya jamii.

Mambo mengine yaliyojadiliwa katika sura hii ni athari ya lugha ya matumizi mapana (Kiswahili) kwa Waarabu waishio katika Pwani ya Afrika Mashariki. Athari hizo ni zile za Kidini, Kiutamaduni, Kisiasa na utawala na athari za Kiuchumi. Masuala mengine yaliyojadiliwa ni pamoja na maendeleo ya lugha ya Kiswahili katika karne ya ishirini na moja. Maendeleo haya yameangaliwa katika Nyanja za elimu, habari na mawasiliano pamoja na fasihi ya Kiswahili na maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Vilevile, katika sura hii kumeelezwa changamoto mbalimbali inazokabili lugha ya Kiswahili katika maendeleo yake. Mambo haya yote yamefanikisha kukamilika kwa malengo mahususi ya utafiti huu ambayo kwayo lengo kuu la utafiti limeweza kufikiwa. Sura inayofuata imetoa hitimishi, muhtasari, matokeo ya utafiti na mapendekezo.

6.3 Matokeo ya Utafiti

Katika sehemu iliyopita hapo juu muhtasari wa tasinifu nzima umetolewa na katika sehemu hii tunaonesha matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba, chimbuko la lugha ya Kiswahili limeelezwa kwa kupotosha sana na baadhi ya wanataaluma waliotafiti kuhusu lugha ya Kiswahili katika karne ya kumi tisa.

Upotoshaji huo kwa hakika unaonesha kwamba, hakuna sababu za msingi zinazoonesha kuwa, Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu. Hii inatokana na ukweli kwamba waliofanya utafiti huo na kutoa mahitimishi hayo si wataalamu halisi wa lugha ya Kiswahili. Wengi kati ya watafiti hao walikuwa ni wageni ambao hawakuwa na usuli wa kutosha kuhusiana na lugha ya Kiswahili na masuala ya lugha kwa ujumla wake. Kwa mfano, wapo waliodai kwamba, Kiswahili kinatokana na Kiarabu kwa sababu Waswahili wanatamka maneno ya Kiswahili kwa lafudhi ya hati za Kiarabu. Hii kwa hakika haiwezi kuwa hoja ya msingi ya kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa na asili yake katika Kiarabu eti kwa kuwa na lafudhi ya Kiarabu. Hii ni namna moja tu ya kuonesha namna wataalamu hao wa mwanzo kuandikia lugha ya Kiswahili walivyokuwa na utaalamu finyu kuhusiana na lugha, si tu ya Kiswahili bali lugha kwa ujumla.

Kimsingi, haimuhitaji mtu kuwa na shahada ya Kiswahili ama lugha yoyote ile kuweza kutambua kwamba, wazungumzaji wa lugha mbili tofauti wanapokutana na kuishi pamoja kwa kipindi kirefu ni dhahiri kutakuwa na kuathiriana kwa lugha husika, si hivyo tu bali pia, lugha ya watwana itasemekana kuathiriwa zaidi na lugha ya mabwana kwa sababu mabwana ni tabaka la juu, watu bora, wenye hadhi, wasiopenda kushindwa daima. Haya yote ndiyo yamefanya Kiswahili kielezwe namna kinavyoelezwa na wataalamu hao ambao hawakupevuka kilughawiya jamii.

Matokeo ya utafiti yanaendelea kuonesha kwamba, madai kwamba lugha ya Kiswahili ina asili ya Kiarabu kwa sababu hata fasihi yake inatokana na fasihi ya Kiarabu na dini ya Kiislamu. Mawazo haya yameongozwa na mtazamo kwamba,

maudhui ya dini ya Kiislamu pamoja na fani ya ushairi wa Kiarabu ndivyo vilivyotawala katika ushairi wa Kiswahili. Katika muendelezo uleule wa kuonesha kwamba, wataalamu hao waliofanya tafiti za mwanzo na kuibua mawazo hayo hawakuwa wameiva katika taaluma ya lugha ni kushindwa kutambua kwamba, ni dhahiri kwamba mfumo wa maisha uliokuwa au unaotawala katika jamii fulani ndiyo haswa hurejelewa katika kazi mbalimbali za kifasihi kwa kuwa fasihi ni zao la jamii. Hivyo, si ajabu kuona maudhui ya dini ya Kiislamu yakielezwa katika ushairi wa Kiswahili. Vile vile, wataalamu hawa walifanya uchambuzi wao kwa kuzingatia mashairi machache yenye kueleza zaidi maudhui ya dini ya Kiislamu huku wakiyapa kisogo mashairi na kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili zinazozungumzia na kuwasilisha maudhui kuhusu ya maisha ya Waswahili.

Vile vile, matokeo ya utafiti yanaendelea kuonesha kwamba, Kiswahili kama lugha ya matumizi mapana kimeweza kuwaathiri Waarabu waishio katika Pwani ya Afrika ya Mashariki. Athari hizo zinaonekana katika vipengele vya kidini, kiutamaduni, kisiasa na utawala pamoja na kiuchumi. Waarabu waishio katika upwa wa Afrika ya Mashariki wamejikuta wakikifanya Kiswahili kuwa ndiyo lugha yao kuu ya mawasiliano na si Kiarabu lugha ya babu na bibi zao. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, lugha kuu inayozungumzwa katika upwa wa Afrika ya Mashariki ni Kiswahili na wao ni sehemu ya jamii hiyo na hivyo kulazimika kujifunza Kiswahili ili waweze kuwasiliana na wenzao. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu imebainika kwamba, Waarabu wengi waishio katika Pwani ya Afrika ya Mashariki hawajui kuzungumza lugha ya Kiarabu na itokeapo mmoja wao akasafiri kwenda Uarabuni hushindwa kuwasiliana na wenzake na hivyo kupata taabu.

Katika masuala ya dini matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, tofauti na mafundisho ya dini ya Kiislamu yanavyoelekeza, kwamba Kiarabu ndiyo lugha pekee ya kuendelea masuala ya kidini/ Ibada, Kiswahili kwa sasa ndicho kilichoshika hatamu. Katika Ibada kama vile swala ya Ijumaa hotuba husomwa kwa lugha ya Kiswahili huku nguzo za hotuba zikisomwa kwa lugha ya Kiarabu. Hii ni athari ya matumizi ya lugha ya Kiswahili. Vile vile, hata kaswida nyingi zinazoimbwa katika madrasa mbalimbali ni zile zilizotungwa kwa lugha ya Kiswahili kuliko zile za Kiarabu.

Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, katika kipengele cha utamaduni, Waarabu waishio katika upwa wa Afrika ya mashariki wamekuwa wakifanya mambo mbalimbali kwa kupitia utamaduni wa Mswahili. Wafanyapo masuala ya ndoa kwa mfano, huimba nyimbo mbalimbali za Kiswahili na si Kiarabu. Kwa kufanya hivyo, wamekuwa ni Waswahili na sio Waarabu tena kwa maana ya utamaduni. Shughuli mbalimbali kama vile, kilimo, uvuvi, ufugaji, uwindaji na kadhalika navyo hufanywa na Waarabu kama wafanyavyo Waswahili. Shughuli hizi hufanywa kwa kuambatana na nyimbo, misemo methali na nahau za lugha ya Kiswahili. Hii ni athari ya lugha ya Kiswahili kwa Waarabu waishio katika upwa wa Pwani ya Afrika ya Mashariki.

Si hivyo tu, bali pia matokeo ya utafiti yanaendelea kuonesha kwamba, lugha ya Kiswahili imepiga hatua kubwa sana ya maendeleo kitaifa na kimataifa. Maendeleo haya yanaonekana katika nyanja za kielimu, kimawasiliano na fasihi kwa ujumla. Katika sekta ya elimu kwa mfano Kiswahili kimekuwa kikifundishwa katika nchi mbalimbali duniani. Kwa mfano, nchini Marekani peke yake Kiswahili

kinafundishwa katika vyuo zaidi ya 100. Katika nchi nyingine kama vile Uingereza, China Japan, Urusi, Mexico na nchi mbalimbali za Kiafrika nako Kiswahili kinafundishwa na kusomwa na wanafunzi wengi. Kwa matokeo haya ya utafiti, ni dhahiri kwamba Kiswahili si lugha ya vizalia wala si Kiarabu na kama ingekuwa ni kinyume chake basi Kiswahili kisingeweza kufikia hatua hiyo kubwa ya maendeleo kupata kufikiwa na lugha ya Kiafrika.

Vile vile, Kiswahili kinatumika kuhabarisha watu mbalimbali wazungumzao au wajua lugha ya Kiswahili katika nchi mbalimbali duniani. Kiswahili kinatumika kutangaza habari katika redio za BBC, redio Japan, Sauti ya Amerika, Deuchewelle, Redio China na sauti ya Urusi. Kutumika kwa Kiswahili katika redio hizi za Kimataifa ni namna mojawapo ya kuonesha namna lugha hii ilivyoweza kupiga hatua kitaifa na kimataifa. Kama lugha hii ingekuwa ni lugha ya vizalia ama ni Kiarabu isingeweza kupiga hatua hii ya maendeleo iliyofikia ambayo pia huitambulisha jamii ya Waswahili kimataifa na kuwezesha kuongeza pato la taifa kupitia utalii na kadhalika.

Hali kadhalika matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba, lugha ya Kiswahili inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo kwa hakika zinapunguza kasi ya ukuaji na ueneaji wa lugha ya Kiswahili duniani. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na upungufu wa vitabu vya kiada na ziada kwa ajili ya kufundishia Kiswahili kwa wageni, upungufu wa wataalamu wa kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni, kukosekana kwa sera maalumu ya lugha nchini Tanzania, utashi wa kisiasa na kukosekana kwa chombo maalumu cha kuratibu lugha ya Kiswahili katika ukanda

wa Afrika ya Mashariki. Utatuzi wa changamoto hizi ni suala la muhimu sana ambalo limeelezwa katika sehemu ya mwisho ya kila changamoto.

6.4 Mapendekezo

Pamoja na matokeo mazuri niliyoyapata katika utafiti huu tunapenda kutoa rai zifuatazo kuhusiana na tafiti za baadaye.

Mosi, utafiti huu ulifanyika katika maeneo ya Pemba, Unguja na Dar es Salaam tu. Hivyo basi, ninapendekeza kwamba utafiti kama huu ufanywe katika maeneo mengine ya upwa wa Afrika Mashariki yaliyosalia.

Pili, katika uhakiki na uteuzi wa nadharia tuliona nadharia moja ikidai kwamba Kiswahili ni Kikongo. Utafiti kama huu unaweza kufanyika katika maeneo ya Kongo ili kuona namna Kiswahili kilivyowaathiri Wakongo katika vipengele mbalimbali kama vile nilivyovitumia katika utafiti huu.

Tatu, utafiti kama huu unaweza kufanywa katika uwanja wa Kilughawiya ili kuona athari ya lugha ya Kiswahili kwa lugha ya Kiarabu. Kwani utafiti wetu ulijikita katika Lughawiya jamii tu.

AREJELEO

Abdulaziz, M.H., (1992), *Arabic Borrowings in Kiswahili in The Relation Between African languages and Arabic languages*, Dakar Conference (8-11 Rajab 1402/9-12 April 1984), Dakar, Senegal.

Abdullah, A.M. (1996) “Swahili and its Development in the World” katika <http://www.languages.net> saa 4:00 asubuhi, tarehe 14 January, 2012.

Abdul-Latif, A.M. (1998), **The Arabian Africa**, Tripoli World Islamic Call Society.

Adam, M., (2000), *Cultural History: Arabic Hausa, Kiswahili and the Unity and Development of Africa*, National Kiswahili Seminar Presentation: Mbale Islamic University in Uganda.

Adam, Mahdi., (2000), *Rector’s Remarks during the National Seminar on Kiswahili in Uganda*, Mbale: Islamic University in Uganda

Affirifah, Kofi., (1998), *Towards the Eliminations of Inferiority Complex in Africans*, in conference Proceedings on Education for Liberation in Africa. **The Sebha Research Centre for African Studies** 20th – 25th March (1988) vol. 2.

Ali, M., (1966), *Maendeleo ya maandishi ya Kiswahili*, **Katika Kiswahili Juzuu 36/2/ Dar es Salaam**. TUKI:

Alli, B.C. (2012) “Swahili Language and the World Literature”. Katika Journal of Language Studies Moscow.

- Babbie, E., (1999), **The Basics of Social Research**. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Berg B.C., (2007), **Qualitative Research Methods for the Social Sciences** (6th ed) California: Pearson Education Inc.
- Best J.W and Khan J.V., (2006), **Research in Education**. (10th ed.), New York: Pearson Education Inc.
- Bickerton, D., (1981), *Discussion of two perspectives on indigenization as language acquisition*, Katika **New Dimension's in second language Acquisition Research Rowlye**: Newbury House.
- Bogdan, R.C and Biklen, S.K., (1992), **Quantitative Research for Education: An Introduction to Theory and Methods**, (2nd ed.), Boston: Allyn and Bacon.
- Chomi, E.W., (1988), *European Linguistic Imperialism and the Dilemma Facing Africa's Educational Policy-Makers*, in Sebha Proceedings (3), Sebha: Research Centre for African Studies.
- Chomsky, N., (1965), **Aspects of the Theory of Syntax**. Cambridge MA M.I.T. Press
- Cohen, L. *et. al.*, (2000), **Research Methods in Education** (5th ed). London: Rontledge Press.
- Creswell, J.W., (2009), **Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches**. Los Angeles: SAGE Publications.

- Druckman, D., (2005), **Doing Social Research: Methods of Inquiry for Conflict Analysis**, London: Thousands (Calif) SAGE.
- Ewan, C. And Calvert, D., (2000), **The Crisis of Scientific Research**, in Garrick J.R. and Carl C. (2000), CAL Sage Publications
- Furlong, N., *et.al.*, (2000), **Research Methods and Statistics: An Integrated Approach**. New York: Harcourt College Publishers.
- Ghanem, K.S.M., (2005), *Kiswahili kuwa lugha rasmi ya Kidiplomasia katika Umoja wa Afrika*. Tasnifu ya uzamivu, chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Guthrie, M., (1948), **The classification of Bantu Language**. London: Oxford University Press.
- Harris, L., (1962), **Swahili Poetry**. London: OUP
- Isaac and Michael., (1981), **Handbook of research and evolution: A collection of principles, methods and strategies useful in the planning, design and behavioural science**, San. Diago: Edips.
- John, L., (2004), **Critical Reading: A Guide**. in <http://www.brocku.ca/english/jlge/criticalreading.html>. Accessed, 30th October, 2006.
- Khalidi, J.I. (2005) “Msamiati wa Kiarabu katika Kiswahili” *Journal of Nordic Studies and Languages*. University of Upsala. Uppsala.
- Kigume, R.A., (2010), *Syllable Structure in Kingindo: The case of Kimangindo Variety*: M.A Linguistics Dissertation, University of Dar es Salaam

Kihore, Y.M., (1984), *Kiswahili katika Hati za Kiarabu katika Mulika* Na. 16, TUKI: Dar es Salaam, uk. 38-45.

Kihore, Y.M., (2003), *Maandishi ya Kiarabu yaliyo na umuhimu kwa Kiswahili katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III*, TUKI: Dar es Salaam, uk. 166-185.

Kihore, Y.M., na wenzie (2003), **Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu** (SAMAKISA. Dar es Salaam: TUKI.

Kitala, (2006), *Mapitio ya ripoti ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania*. Dar es Salaam: Haijachapishwa.

Kothari, C.R., (1992), **Research Methodology: Methods and Techniques**. New Delhi: Wiley Eastern Limited.

Kothari, C.R., (2008), **Research Methodology: Methods and Techniques**. New Delhi: New Age International Publishing Ltd.

Kumar, R., (1999), **Research Methodology: A step-by-guide for beginners**. New Delhi: SAGE Publicationand Co

Maganga, C. (1997) *Historia ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Maganga, C., (1991), *A study of the morphophonology of Standard Kiswahili, Kipemba, Kitumbatu and Kimakunduchi*, Ph.D Thesis University of Dar es Salaam.

- Massamba D.P.B., (2002), **Historia ya Kiswahili**, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation
- Mbaabu (2003), *Sheng English Dictionary: Diciphering East Africa Underworld Language*. Dar es Salaam: Unpublished Phamphlet
- Mekacha, R.D.K., (2000), **Isimujamii: Nadharia na Muktradha wa Kiswahili**. Minocity: Osaka University of Foreign Studies.
- Mhochi and Wairiru (2004) “Maendeleo ya Kiswahili Duniani”, katika <http://www.maendeleo> ya Kiswahiliduniani/mhw/net, saa 6.00 mchana, tarehe 16/3/2012
- Mlacha, S.A.K., (1984), *Riwaya za Visiwani (1970-1980) na Ujenzi wa Jamii Mpya*, katika **Mulika** Na 16, TUKI : Dar es Salaam, uk. 4-31.
- Mlacha, S.A.K., (1996), *Utamaduni wa Mwafrika katika Riwaya ya Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka*, katika **Mulika** Na 23, TUKI: Dar es Salaam.
- Mohamed, A.A., (1994), **Zanzibar Facts, Figures and Fiction**. Zanzibar: Alkayria Press Ltd.
- Mohamed, M.O.A., (2006), *The Teaching of Kiswahili in Libyan Educational Institutions: Problems and challenges*, Ph.D Thesis Open University of Tanzania.
- Mosha, P.T., (2004), *Investigative Journalism and Anti-corruption struggle: Challenges and Prospects within Post Reform Print Mass Media in*

Tanzania, Un published Master of Arts Development Studies Thesis:
University of Dar es Salaam.

Msanjila, Y.P. (2006), *Nadharia katika Isimu Jamii. Mjadala unaoendelea* Katika
Mulika Na. 27, TUKI, Dar es Salaam uk. 40-48.

Mulokozi, M.M. and T.S.Y. Sengo, (1995), **History of Kiswahili Poetry [AD 1000-
2000]**. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M., (1996), **Fasihi ya Kiswahili**: OUT. Dar es Salaam.

Mwansoko, H.J., (1991), **Mitindo ya Kiswahili Sanifu**. Dar es Salaam: DUP.

Nabhany, A.S., (1978), *Lugha Tungo na msamiati wa Kiswahili* Katika **Mulika** Na
14. TUKI: Dar es Salaam uk. 12-14.

Newman, W.L., (2006), **Social Research**. Sixth Edition, Boston: Pearson.

Nicholson, R.A., (1969), **Literary History of the Arabs**, Cambridge University
Press.

Njogu, K. Na Rocha C., (1999), **Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu**.
Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ohly, R., (1977), *Swahili Studies*, Ph.D in Journal of the Institute of Kiswahili
Research, Kiswahili Vol 47/1 IKR: Dar es Salaam.

Omari, S., (2009), **Tanzania Hip Hop As Poplar Literature**, Unpublished Ph.D
Thesis, University of Dar es Salaam.

- Omary, M., (2011), *Siasa katika Ushairi wa Kezilahabi: Uchunguzi wa Karibu Ndani (1988) na Dhifa (2008)*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Owhida, B.O.A., (2006), *Ushairi wa Kiswahili na Ushairi wa Kilibya: Kufanana na kutofautiana*, Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Polome, E., (1967), **Swahili Language Hand book** Washington Dc;; Centre for Applied Linguistics.
- Robson, C., (2007), **How to do a research project: A guide for Undergraduate Students**, Cariton Victoria: Blackwell Publishing
- Sengo, T.S.Y., (1985), *The Indian Ocean Complex Culture: The Case Study of folkutale Performances of Zanzibar and Pemba*, Unpublished Ph.D Thesis, IAAS, University of Khartoum.
- Sengo, T.S.Y., (2000), *Utotozi wa Uwisilamu katika Kiswahili: Chuki za Kisirisiri*, Maoni ya Semina ya Kiswahili nchini Uganda, Mbale, Ndaki ya Kiislamu iliyoko Uganda.
- Senkoro, F.E.M.K., (1976), *Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili*, Katika **Kiswahili** Juzuu 46/2 TUKI: Dar es Salaam uk. 74-82.
- Senkoro, F.E.M.K., (1997), *The Sigificance of the Journey in Folk Tales from Zanzibar*, Ph.D Thesis, University of Dar es Salaam.
- Shariff, I.N., (1973), *Waswahili and their language: Some misconceptions*, Katika **Kiswahili** Juzuu 43/2. Dar es Salaam.

Steere, E., (1870), **A handbook of Swahili Language as Spoken at Zanzibar,**

London: Sheldon Press.

Swaleh, A., (1999), *Lugha ya Kiswahili Pijini au Krioli?* Katika, **Mulika**, Na. 25

TUKI Dar es Salaam, uk, 92-100.

TUKI (1985), "Tahariri". *Kiswahili*, 54(1/2): v-vi.

Wamitila, K.W., (2002), **Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele vyake,**

Nairobi:Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K.W., (2008), **Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi,**

Nairobi: Vide-Muwa

Whiteley, W.H., (1969), **Swahili: The Rise of National language.** London Methuen.

Yin, R.K., (1994), **Case Study Research: Design and Methods**, (2nd eds.) thousand

Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P.V., (1984), **Scientific Social Survey and Research,** Englewood Cliffs:

Pren

Zukov M.C. (2004) "Islam and adoption of trational forms" *International Journal*

of OLanguage Studies. Moscow

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO NA. 1

**DODOSO KWA WAZUNGUMZAJI WA LUGHA YA KISWAHILI NA
KIARABU**

JINA.....

UMRI.....

JINSI

KIWANGO CHA ELIMU.....

Je wewe ni mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili? (a) ndiyo (b) hapana []

Eleza kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa ufahamu
wako.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Taja sababu mbalimbali zinazotumiwa na wanataluma kadhaa kutoa madai kwamba

Kiswahili ni

Kiarabu.....

.....

.....

.....

Ni yapi maendeleo ya lugha ya Kiswahili katika karne ya ishirini na moja

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Toa maoni yako juu ya namna bora ya kutatua changamoto zinazokabili maendeleo ya lugha ya Kiswahili Duniani

.....

.....

.....

.....

ASANTE SANA KWA USHIRIKIANO WAKO

KIAMBATISHO NA.2

DODOSO KWA WATAALAMU WA KISWAHILI NA KIARABU

JINA KAMILI.....

UMRI.....

JINSI (me/ke).....

KIWANGO CHA ELIMU

TAASISI.....

CHEO

Inasemekana kuwa kuwa Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu huku maelezo juu ya Kiswahili kukiathiri Kiarabu yakikosekana? (a) ndiyo (b) hapana Toa sababu za kuwapo kwa hali hii

.....
.....
.....
.....
.....
.....

Fafanua kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili

.....
.....
.....
.....
.....
.....

.....
.....
.....

3. Matumizi ya lugha ya Kiswahili yameiathiri vipi jamii ya Kiarabu iishio katika mwambao wa Pwani ya Afrika ya Mashariki?

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

4. Ni changamoto zipi zinazokabili maendeleo ya lugha ya Kiswahili duniani?.....

.....
.....
.....
.....
.....

5. Toa maoni yako juu ya utatuzi wa changamoto zinazkabili maendeleo ya lugha ya

Kiswahili duniani.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

ASANTE SANA KWA USHIRIKIANO WAKO